TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

RIPOTI YA MAPITIO WA SHERIA

YA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR

NAMBA 12 YA MWAKA 2019

NAMBA 4/2022

INAWASILISHWA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

FEBRUARI, 2022

MHESHIMIWA MWALIM HAROUN ALI SULEIMAN,

WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS- KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA,

ZANZIBAR.

MHESHIMIWA DKT. MWINYI TALIB HAJI,

MWANASHERIA MKUU WA ZANZIBAR,

ZANZIBAR.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya Mwaka 1986, kwa heshima, Tume inawasilisha Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Serikali Mtandao Zanzibar Nam. 12 ya mwaka 2019.

………………………

KHADIJA SHAMTE MZEE
MWENYEKITI,
TUME YA KUREKEBISHA SHERIA,
ZANZIBAR

02 FEBRUARI, 2022.

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

MHE. KHADIJA SHAMTE MZEE
MWENYEKITI

BW MUSSA KOMBO BAKARI
KATIBU

MWENYEKITI

Mhe. Khadija Shamte Mzee	Mwenyekiti

WATAFITI

Nd. Mussa Kombo Bakari	Katibu wa Tume
Nd. Ali Salum Ali	Mtafiti wa Sheria
Nd. Sabra Mahmoud Iddi	Mtafiti wa Sheria

Tume ya Kurekebisha Sheria

Vuga, Zanzibar-

P.O BOX 2539,

Simu +255 24 2231143,

Nukushi +255 24 2231137,

barua pepe info@lrcz.go.tz.

tovutiwww.lrcz.go.tz

VIFUNGU VYA UTANGULIZI

Mpangilio wa vifungu……………………………………………………………………..vi

Rejea……………………………………………………………………………………………..x

Shukrani………………………………………………………………………………….xviii

Vifupisho vya Maneno……………………………………………………………………xx

Muhtasari……………………………………………………………………………………..xxi

SURA YA KWANZA

1.0 **UTANGULIZI**……………………………………………………………………………..1

1.1 **Mamlaka ya Tume**……………………………………………………………………..1

1.2 Chimbuko la Utafiti……………………………………………………………………..2

1.3 Maelezo ya Tatizo………………………………………………………………………..2

1.4 Historia ya Serikali Mtandao……………………………………………………………3

1.5 Hadidu Rejea……………………………………………………………………………...8

1.6 Malengo ya Utafiti………………………………………………………………………9

1.7 Umuhimu wa Utafiti…………………………………………………………………... 9

1.8 Njia za Utafiti……………………………………………………………………………10

1.9 Upeo wa Utafiti…………………………………………………………………….......10

SURA YA PILI

2.0 **DHANA YA SERIKALI YA MTANDAO**……………………………………………..11

2.1 Utangulizi…………………………………………………………………………………..11

2.2 Maana ya Serikali Mtandao…………………………………………………………….11

2.3 Umuhimu wa Serikali Mtandao………………………………………………………...14

2.4Maeneo ya Kuzingatiwa……………………………………………………………………...16

2.5 Maeneo ya mabadiliko ya Serikali Mtandao…………………………………………....17

2.6 Lengo la Serikali Mtandao………………………………………………………………..17

2.7 Matumizi ya Serikali Mtandao…………………………………………………………...18

2.8 Faida za Serikali Mtandao………………………………………………………………..19

2.9 Hatua za Serikali Mtandao………………………………………………………………21

2.10 Tofauti ya Mawasiliano ya habari na Serikali Mtandao…………………………………..23

2.11 Aina za Serikali Mtandao……………………………………………………………………………..23

2.12 Utekelezaji wa shughuli za Serikali Mtandao …………………………………………………..25

SURA YA TATU

3.0 **UCHAMBUZI WA SERA NA SHERIA MBALI MBALI……………………………………26**

3.1 Utangulizi………………………………………………………………………………………………26

3.2 Sera na Muongozo……………………………………………………………………………………27

3.3 Sheria………………………………………………………………………………………………...32

SURA YA NNE

4.0 **MAONI YA WADAU**…………………………………………………………………………………..44

4.1 Utangulizi……………………………………………………………………………………………...44

4.2 Maoni ya Kisheria………………………………………………………………………….............44

4.3 Maoni ya Kiutendaji……………………………………………………………………………...47

SURA YA TANO

5.0 **MIKATABA YA KIMATAIFA NA UZOEFU WA NCHI NYENGINE…………………………51**

5.1Utangulizi…………………………………………………………………………………………….51

5.2 Mikataba ya Kimataifa……………………………………………………………………………51

5.3 Mikataba ya Barani Afrika………………………………………………………………………...54

5.4 Mikataba ya Kikanda…………………………………………………………………………...57

5.5 Uzoefu wa nchi nyengine…………………………………………………………………………60

5.5.1 Sheria za nchi mbalimbali……………………………………………………………………...61

5.5.2 Uzoefu wa Hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa malengo ya Ianzishwaji wa Serikali Mtandao ………………………………………………………………...80

5.5.3 Hitimisho la nchi mbali mbali………………………………………………………………86

SURA YA SITA

6.0 MATOKEO YA UTAFITI………………………………………………………………………….89

6.1Utangulizi…………………………………………………………………………………………89

6.2 Njia zilizotumika katika Utafiti…………………………………………………………………89

6.3 Upeo wa Utafiti……………………………………………………………………………………....90

6.4 Ukomo wa Utafiti……………………………………………………………………………………90

6.5 Sampuli ya Utafiti……………………………………………………………………………………..91

6.6 Hadidu Rejea……………………………………………………………………………………………94

6.7 Ukomo wa Utafiti……………………………………………………………………………………..95

6.8 Matokeo ya Utafiti…………………………………………………………………………………....95

6.8.1 Mapendekezo ya Kisera…………………………………………………………………………95

6.8.2 Kisheria…………………………………………………………………………………………………...96

6.8.3 Mapendekezo ya Kikanuni……………………………………………………………………...98

6.8.4 Kiutendaji……………………………………………………………………………………………...98

SURA YA SABA

7.0 **MAPENDEKEZO NA HITIMISHO**…………………………………………………………...105

7.1 Utangulizi……………………………………………………………………………………………...105

7.1.1 Mapendekezo ya Kisera……………………………………………………………………...105

7.1.2 Mapendekezo ya Kisheria……………………………………………………………………..106

7.1.3 Mapendekezo ya Kikanuni……………………………………………………………………109

7.1.4 Mapendekezo ya Kiutendaji…………………………………………………………………..110

7.2 HITIMISHO……………………………………………………………………………………………111

MPANGILIO WA VIFUNGU

MPANGILIO WA JADUELI NA CHATI

Jadueli Nam. 1: Idadi ya washiriki wote wa Utafiti.

Chati Nam.1: Mchanganuo wa washiriki kwa Jinsia

Chati Nam. 2: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu

Chati Nam. 3: Idadi na asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri

SERA NA SHERIA

Sera ya Serikali Mtandao ya mwaka 2015

Sera ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010

Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011

Sera ya Mawasiliano ya Habari ya mwaka 2013

Dira ya 2050

MKUZA III

SHERIA

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984

Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Nam. 16 ya mwaka 1986

Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Nam. 12 ya mwaka 2019;

Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011;

Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba Nam. 12 ya mwaka 2016;

Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 11 ya mwaka 2016;

Sheria ya Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Nam. 15 ya mwaka 2020;

Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar Nam. 1 ya mwaka 2017;

Sheria ya kuanzisha Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia Nam. 2 ya mwaka 2009;

Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Tanzania Nam. 14 ya mwaka 2015; na

Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Mawasiliano ya Habari Tanzania namba 12 ya mwaka 2003.

SHERIA ZA NCHI NYENGINE

Mauritius - Sheria ya Habari na Mawasiliano (Information and Communication) Nam. 44 ya mwaka 2001

Sheria ya Huduma za Kielekroniki yam waka 2000(Information and Communication) Nam. 44 ya mwaka 2001

Sheria ya Electronic Government Activities Nam. 680 ya mwaka 2007 -Malaysia

Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya Tanzania namba 14 ya mwaka 2015

Sheria ya Serikali Mtandao.namba 10 ya mwaka 2019 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Sera ya Mawasiliano ya mwaka wa 2000 - Tonga

Sheria ya Mawasiliano Nam. 13 ya mwaka 2015- Tonga

Electronic Communication Abuse Offences Nam. 23 ya mwaka 2020- Tonga

Computer Crimes Act Nam. 14 ya mwaka 2003- Tonga

Sheria ya makosa ya matumizi ya kielektroniki ya Nam. 23 ya mwaka 2020- Tonga

Sheria ya Miamala ya Kielektroniki Nam. 24 ya mwaka 2000 -Vanuatu

Sheria ya Biashara ya e-Business Nam. 25 ya mwaka 2000 - Vanuatu

The Electronic Transaction Act Nam. 26 ya mwaka 2008 -Fiji

Sheria ya Huduma za kielektroniki Nam. 26 ya mwaka 2008- Fiji

Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki ya Samoa (SAMOA Electronic Transactions ACT), Sheria Nam. 15 ya mwaka 2008

Electronic Transactions ACT- Sheria Nam. 15 ya mwaka 2008 -SAMOA

EU the Digital Markets Act (DMA)
EU the Digital Services Act (DSA)

MIKATABA, MAAZIMIO NA MIPANGO YA KIMATAIFA

Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948)

2030 ya Maendeleo Endelevu yaliyopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN) mwaka 2015

United Nations. (2013). United Nations E-government Survey 2012. New York: United Nations

The Convention for the Protection of Individuals with regard to Automatic Processing of Personal Data, 1981 ETS 108,

World Bank International Development Association Report, PAD2863 Kingdom of Tonga , April, 2019

Mkataba wa Uhalifu wa Mtandao
Zanzibar Electronic Government Agenda; A Way Forward; 18 November 2011

Zimbabwe National Policy for Information and Communications Technology (ICT) (2016)

UNCTAD
The e-Government Imperative. Paris: OECD (2003) e-Government Studies. ISBN 92-64-10117-9

Miongozo ya Ulinzi wa Faragha na Mtiririko wa Data ya Kibinafsi ilipitishwa kama Pendekezo la Baraza la OECD,
Azimio la mwaka 1985 kuhusu Mtiririko wa Data ya Kuvuka Mipaka,

Tamko la Mawaziri kuhusu Ulinzi wa Faragha kwenye Mitandao ya Kimataifa

Mkataba wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa taarifa (Data) 2014

Mkataba wa Usalama Mtandaoni na Ulinzi wa Data ya Kibinafsi

AGENDA ya Afrika 2063

Mfumo wa EAC wa Sheria za Mtandao wa mwaka 2010

Sheria ya Kielelezo kuhusu Miamala ya Kielektroniki na Mwongozo wa Utungaji mwaka 2010 COMESA

Mradi unaoendelea wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS)

REJEA

MAKALA NA VITABU

Abdulrazaq Kayode Abdulkareem "Challenges of E-Government Implementation in the Nigerian Public Service, Journal Of Creative Writing Volume 1, ISSUE 4 2015, PP 45-56,

Åke Grönlund; "Ten Years of E-Government: The End of History and New Beginning;" Swedish Business School Fakultetsgatan 1, 701 82 Örebro, Sweden

Ali KE, Mazen SA, Hassanein EE. A proposed framework for the organization readiness assessment of IT innovation adoption in e-government environment. *Int. J. Intell. Comput. Inf. Sci.* 2017;17(2):33–50

Anttiroiko, A i-Veikko. and Malkia, Matti. 2006. Encyclopedia of digital government. Hershey, PA: Idea Group Reference (IGI)

Ahn MJ, Bretschneider S. Politics of e-government: e-government and the political control of bureaucracy. *Public Adm. Rev.* 2011;71(3):414–424.

Aziz NAA, Manab NA, Othman SN. Critical success factors of sustainability risk management (SRM) practices in Malaysian environmentally sensitive industries. *Soc. Behav. Sci.* 2016;2016(219):4–11.

Boaz Chean and David Rashty, e- government in Israel, Ministry of Finance General Acountant Office, September 2002

Cook, M., & Harrison, T. M. (2015). Using public value thinking for government IT planning and decision making: A case study. Information Polity, 20(2/3), 183–197

David Brown "Electronic government and public administration" International Review of Administrative Sciences, 2005 IIAS, SAGE Publications (London, Thousand Oaks, CA and New Delhi) Vol 71(2):241

Ebrahim Z, Irani Z. e-Government adoption: architecture and barriers. *Bus. Process Manag. J.* 2005;11(5):589–611. doi: 10.1108/14637150510619902

Gore, Albert (1993). "Reengineering Through Information Technology. Accompanying Report of the National Performance Review" Washington: Office of the Vice President

Gregory G. Curtin, Michael Sommer&Veronika Vis-Sommer (2003), The World of E-Government, Routledge

Heeks, Richard. and Bailur, Savita. 2007. Analyzing e-governmen research: perspectives, philosophies, theories, methods, and practice. Government Information Quarterly, 24(2):243- 265

Hanna NK. Transforming Government and Building the Information Society: Challenges and Opportunities for the Developing World. New York: Springer; 2010
Savoldelli A, Codagnone C, Misuraca G. Understanding the e-government paradox: learning from literature and practice on barriers to adoption. *Gov. Inf. Q.* 2014;31:63–71.

Isabel Bosman (2021) “COVID-19 and E-Governance: Lessons from South Africa” South African Institute of International Affairs Stable

J. Pengur. 2018;2018(53):73–82. doi: 10.17576/pengurusan-2018-53-07

Latifa Alzahrani, Wafi Al-Karaghouli, Vishanth Weerakkody
Analysing the critical factors influencing trust in e-government adoption from citizens' perspective: A systematic review and a conceptual framework, 2016 Published by Elsevier Ltd.

Layne, K. & Lee, J. (2001). "Developing Fully Functional E-Government: A Four Stage Model." Government Information Quarterly. 18, 122

Leon J. Osterweil, Lynette I. Millett, and Joan D. Winston, (Eds)Social Security Administration Electronic Service Provision; A Strategic Assessment; The National Academies Press, 2007, N.W., Washington, DC 20055

Ligita zailskaitic E- government implementation in Lithuania, Kauns University of Technology Institute of Europe, Lithuania

Michael P, et al. e-Government implementation challenges in developing countries: the project manager's perspective. *Int. J. Public Adm. Manag. Res. (IJPAMR)* 2018;4(3):1–17]

Manjot Kaur1 , Dr. Amitoj Singh, E-Government: Study of Factors significantly affects Adoption and Acceptance in State of Punjab, (IJCSIT) International Journal of Computer Science and Information Technologies, Vol. 6 (5) , 2015, 4542-4548

Melitski, J. (2003). "Organizational Capacity and E- government Performance." Public Performance and Management Review. 26, 325

Meiyanti, R., et al.: Systematic review of critical success factors of e-government: definition and realization. In: 2017 International Conference on Sustainable Information Engineering and Technology (SIET), Malang, Indonesia. IEEE (2018)

Moon, M. J. (2002). "The Evolution of E-government Among Municipalities: Rhetoric or Reality?" Public Administration Review. 62, 42

M Backus "E-governance in developing countries", IICD Research Brief No 1, March 2001, website: www.iicd.org; see also P Norris 'The worldwide digital divide: information poverty, the Internet and development' Harvard University, 2000.

Nancy J. Hafkin "-Government in Africa: An Overview of Progress Made and Challenges Ahead" Prepared for the UNDESA/UNPAN workshop on electronic/mobile government in Africa: Building Capacity in Knowledge Management through Partnership, held at the United Nations Economic Commission for Africa, 17-19 February 2009

Naome Rajah; E- Government in Zimbabwe: An Overview of Progress made and Challenges Ahead; Volume 6, No. 12, December 2015; Journal of Global Research in Computer Science, Research Paper,

Napitupulu D, Sensuse DI. (2014) "The critical success factors study for e-government implementation." *Int. J. Comput. Appl.* 2014;89 (16):23–32.,

Pardo TA, Nam T, Burke GB. (2012) E-government interoperability interaction of policy, management, and technology dimensions. *Soc. Sci. Comput.Rev.* 2012;30(1):7–23.

Nkohkwo QN, Islam MS. Challenges to the successful implementation of e-government initiatives in Sub-Saharan Africa: a literature review. *Electron. J. E-Gov.* 2013;11:253–267

Ndou. V, (2004) E-government for developing countres: opportunities and challenges. The Electronic Journal on Information Systems in Developing Countries. Vol. 18 no 1. PP 1-24

OECD 'The E-government imperative', in OECD E-Government Studies. OECD, Paris, 2003,

Olowu 2004 Quoted in "Chapter 12 :Elecgtronic Government and Rural Development in Anglophone West Africa, by Kehinde David Adejuwon, Sodhi, Inderjeet Singh (ed) (2014) "Emerging Issues and Prospects in African E-Government, IGI Global.

Olaniyi, E.: (2018) "Digital government: ICT and public sector management in Africa. In: New Trends in Management: Regional and Cross-Border Perspectives," London Scientific Publishing, London

Othman MH, Razali R. Whole of government critical success factors towards integrated e-government services: a preliminary review

Øystein Sæbø; E-government in Tanzania: Current Status and Future Challenges; University of Agder, Norway,

Prakash, N., Jaiswal, M., & Gulla, U. (2009). A conceptual framework for measuring public value of enterprise applications. Electronic Government, an International Journal, 6(3), 307–326.

Richard Heeks (2001) "Understanding e-Governance for Development, Institute for Development Policy and Management" , Paper No. 11
Understanding e-Governance for Development Richard Heeks1 IDPM, University of Manchester, UK 2001

Richard Amaechi Onuigbo electronic governance & administration in nigeria: prospects &challenges Arabian Journal of Business and Management Review (OMAN Chapter) Vol. 5, No.3; October. 2015

Spinello, R. (2002). Regulating Cyberspace. Westport, CT: Quorum Books

Shareef MA, Yogesh NA, Dwivedi K. Examining adoption behavior of mobile government. *J. Comput. Inf. Syst.* 2012;53:39–49

Siddique W. Critical success factors affecting e-government policy implementation in Pakistan. *E-J. E-Democr. Open Gov.* 2016;8(1):102–126

Thomas A. Horan Introducing e-Gov: History, Definitions, and Issues, volume 15, June 2005

Watson and Mundy, 2001. Watson, Richard. T and Mundy, Bryan. 2001. A strategic perspective of electronic democracy Communication of the ACM 44(1):27-

West, D.M. (2005a). Digital Government: Technology and Public Sector Performance. Princeton, NJ: Princeton University Press

Xu X, Zhang W, Barkhi R. IT infrastructure capabilities and IT project success: a development team perspective. *Inf. Technol. Manag.* 2010;11:123–142.

Yadav J, Saini AK, Yadav AK. Measuring citizens engagement in e-Government projects – Indian perspective. *J. Stat. Manag. Syst.* 2019;22(2):327–346.

Ziemba E, Papaj T, Żelazny R. A model of success factors for e-government adoption – the case of Poland. *Issues Inf. Syst.* 2013;14:87–100

Ziemba E, et al. Factors influencing the success of e-government. *J. Comput. Inf. Syst.* 2016;56(2):156–167

Zoo H, de Vries HJ, Lee H. Interplay of innovation and standardization: exploring the relevance in developing countries. *Technol. Forecast. Soc. Chang.* 2017;118:334–348.

WEBSITE/TOVUTI

LNCS 7443 - E-government in Tanzania: Current Status and Future Challenges (springer.com)
http://rroij.com/global-research-in-computer-science.php
Zanzibar Social Security Fund – Zanzibar Social Security Fund | Key to the future (zssf.or.tz)
Zanzibar eGovernment Agenda - A Way Forward | Mzalendo Mtanzania - Academia.edu
https://www.jstor.org/stable/resrep29596

http://pbzbank.co.tz/about-us-2/
https://au.int/en/treaties/african-union-convention-cyber-security-and-personal-dataprotection
https://www.eac.int/infrastructure/communications-sector/ongoing-projects
https://www.eac.int/infrastructure/communications-sector/ongoing-projects
http://www.ohada.com/content/newsletters/1403/Comprendre-l-Ohada-en.pdf
http://www.comesa.int/what-we-do/#information-networking
http://www.ecowas.int/wp-content/uploads/2015/02/46th-ECOWAS-Summit-Abuja-15-Dec 2014 1.pdf
http://www.pulse.ng/news/local/ecowas-biometric-ids-senegal-benin-begin-issuance-of-cardsid4651170.html
http://www.au.int/en/decisions/assembly
http://www.coe.int/en/web/conventions/full-list/-/conventions/treaty/108/signatures
http://reports.weforum.org/global-information-technology-report-2016/P
http://www.ict.go.ke/wp-content/uploads/2016/04/The-National-ICT-Masterplan.pdf
http://mtci.govmu.org/English/Documents/eGovStrategyfinalv201393.pdf
https://www.e-spincorp.com/definition-and-type-of-e-government/
https://www.coe.int/en/web/conventions/full-list/-
http://www.integratedjustice.gov.on.ca/

SHUKRANI

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na viongozi wengine wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Uongozi huo wa wizara umekuwa na msaada mkubwa katika kufanikisha ripoti hii. Aidha, tunapenda kuushkuru Wakala wa Serikali Mtandao kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika hatua mbali mbali za utafiti wakati wa mapitio ya Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao.

Shukrani zetu pia tunazitoa kwa wataalam mbali mbali wa masuala ya TEHAMA na Mifumo ya Teknolojia akiwemo Naibu Katibu Mkuu katika Ofisi ya Rais, Fedha na Uchumi anayeshughulikia Mifumo pamoja, Mkurugenzi wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA na Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Mifumo katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na wataalam wa TEHAMA kutoka taasisi za Serikali na taasisi binafsi. Maoni na utaalamu wao umeisaidia sana Tume katika kufanikisha ripoti hii.

Aidha, tunamshkuru Katibu wa Tume Ndg. Mussa Kombo Bakari na wataalam wa Sheria, Utafiti na Mipango, walioongoza zoezi la utafiti huu mdogo na kufanya uchambuzi yakinifu na uandishi wa ripoti

Pia tunatoa shukrani za dhati kwa wadau wengine mbali mbali waliotoa michango mikubwa ya kiutalaamu na kiutendaji wakati wa vikao vya wadau kujadili mapitio ya Sheria hii ya Wakala wa Serikali Mtandao, Nam. 12 ya mwaka 2019. Wadau hao wanajumuisha taasisi mbali mbali za Serikali na binafsi. Tunathamini sana michango yao ambayo imechangia sana katika kufanikisha utafiti huu na hatimaye uandishi wa ripoti hii.

VIFUPISHO VYA MANENO

AU	African Union
CAG	Controller and Auditor General
COMESA	The Common Market for Eastern and Southern Africa
ECA	Excess Crude Account
ECOWAS	*The* Economic Community of West African States
EU	European Union
ICT	Information and Communication Technology
ID	Identification
IT	Information Technology
MKUZA	Mpango wa Kupunguza Umaskini
OECD	The Orgabisation for Economic Cooperation and Development
OHADA	The Organisation for the Harmonization of Business Law
PBZ	People's Bank of Zanzibar
SMS	Short Message Service
TCRA	Tanzania Communication Regulatory Authrity
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
UN	United Nations
UNDP	United Nations Development Programme
UNPAN	United Nations Public Administration Network
WAEMU	The West African *Economic and* Monetary Union
ZRB	Zanzibar Revenue Board
ZSSF	Zanzibar Social Security Fund

MUHTASARI

Tunapitia Mapinduzi ya Kidijitali ya kimataifa ambayo kutegemea Habari na Teknolojia ya Mawasiliano (ICT), na huduma wanazounga mkono ni kuwezesha maendeleo endelevu na ukuaji shirikishi.

Kuna fursa za kipekee za kutumia ICT kwa ukuaji wa uchumi, tija kuongezeka na utoaji huduma bora. Ni wakati muafaka zaidi kwa Serikali kuongeza nguvu, kuwezesha mifumo ya utawala wa kielektroniki. Serikali zinapaswa kuhakikisha matumizi bora zaidi ya teknolojia za kidijitali kwa manufaa ya watu, fanya kazi kama wawezeshaji, wawezeshaji na wadhibiti, kuwashirikisha wadau wote kwa ushirikiano wa uwazi.

Utekelezaji wa utawala wa kielektroniki unapaswa kuwa mchakato wa kina, ambaomasuala ya shirika na udhibiti yanashughulikiwa pamoja na teknolojia, kuna haja ya kutambua nini wakala mtandao (e-governance) ili kuweka uwazi juu ya dhana hii muhimu kwa taasisi za umma, na wanachi kwa ujumla. Kwa ujumla, inapaswa kujumuisha mwingiliano fulani kwa kuongeza ufikiaji wa kielektroniki wa habari.

Hatua husika zinazohitajika kufikia utawala wa kielektroniki zimeelezwa katika utafiti huu na kuchambuliwa, na kutoa mapendekezo ya jinsi gani

shughuli hizi zinavyoweza kufanyika. Kila nchi itahitaji idadi tofauti ya hatua, kwa mpangilio tofauti, kulingana na upatikanaji na matumizi ya ICT, hali ya utawala wa kielektroniki na muundo kwa ujumla.Masuala ya ukusanyaji wa data, mbinu na shughuli zilizopo, ikijumuisha viwango vinavyofanywa na mashirika pamoja na ukusanyaji huru wa data na uchanganuzi wa kitaalamu na wataalam wa Wakala Mtandao.

Utafiti umependekeza mambo mbali mbali ya kufanywa wakati wa utekelezaji wa Serikali Mtandao. Hivyo ni muhimu kuzingatiwa katika sheria mpya inayokusudiwa kutungwa, ikiwemo uundwaji wa miundombinu ya Serikali;uanzishwaji wa miradi ya TEHAMA; kuanzishwa mifumo mipya ya serikali mtandao;utunzaji wa rasilimali za TEHAMA za serikali; utambuzi wa huduma za seriakli matandao;utoaji wa huduma za serikali mtandao kwa serikali na jamii; upunguzaji wa matumizi ya karatasi na uchapishaji wa nayaraka kwa njia za kieletroniki baina ya Taasisi moja kwenda Taasisi nyengine.

Aidha kwa upande wa vyombo vya utekelezaji wa maeneo mengine, sheria za nchi mbalimbali zimeonesha kuundwa kwa mamlaka au chombo ambacho kitasimamia utekelezaji wa uendeshaji wa Serikali Mtandao. Chombo hicho kinakuwa na nguvu ya kisheria ya kusimamia taasisi nyengine za Serikali.

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Mamlaka ya Tume

Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar imeundwa na Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria.[1] Sheria hiyo inaipa uwezo Tume ya Kurekebisha Sheria kuzifanyia mapitio sheria zote za Zanzibar kwa nia ya kuzirekebisha ili ziende sambamba na maendeleo na mabadiliko ya kimfumo.[2]

Tume ya Kurekebisha Sheria katika kufanya mapitio ya sheria inaweza kufanya mapitio kwa kutumia njia tatu zilizoainishwa katika sheria. Njia ya kwanza, Tume inaweza kufanya mapitio ya Sheria ikiona ipo haja ya kufanya hivyo,[3] njia ya pili ni kwa maelekezo ya Waziri anaehusika na mambo ya sheria,[4] na njia ya tatu ni kwa maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar (AG).[5]

Kutokana na uwezo iliyopewa kwenye Sheria, na katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Tume imefanyia mapitio Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao[6] kwa ajili ya kuainisha mapungufu ya sheria hiyo na kupendekeza Serikalini marekebisho yake.

Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar, ikiwa kama chombo kinachojitegemea[7] kilichopewa mamlaka ya kutafiti na kupitia sheria zote za

[1]Nam.16 ya mwaka 1986
[2]Kifungu cha 4(1) cha sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Nam. 16 ya mwaka 1986
[3]Ibid kifungu 4(2)
[4] Ibid Kifungu cha 7
[5]Ibid kifungu cha 8
[6] Nam. 12 ya mwaka 2019
[7]*Op cit* kifungu cha 12

Zanzibar, inafanya mapitio haya kwa madhumuni ya kutambua mapungufu na kupendekeza Marekebisho yake ili kwenda sambamba na nia ya Serikali katika kuwajibika kwa wananchi, kuboresha huduma kwa wananchi, kuboresha huduma kwa taasisi za Serikali na kupunguza urasimu Serikalini.

1.2 Chimbuko la Utafiti

Mnamo mwaka 2019 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepitisha Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao kwa madhumuni ya kurahisisha na kusimamia mawasiliano kwa njia ya mtandao kwa watumishi wa Umma, Taasisi za Serikali Zanzibar, na jamii kwa ujumla. Hata hivyo lengo hilo halikuweza kufikiwa kutokana na muundo, kazi, uwezo na utawala wa Wakala wa Serikali Mtandao ambao umeainishwa katika sheria husika.

Baada ya kubaini kasoro hizo, Tume ya Kurekebisha Sheria inafanya utafiti kugundua sababu za kushindwa kufanyakazi kwa Wakala wa Serikali Mtandao na kupendekeza kwa Serikali mambo muhimu yatakayoisaidia taasisi hiyo kuweza kufanyakazi kiufanisi. Tume ya Kurekebisha Sheria, baada ya utafiti inaweza kupendekeza chombo kipya kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya Serikali Mtandao au kufanya maboresho ya taasisi hiyo ili iweze kufanyakazi iliyokusudiwa.

1.3 Maelezo ya Tatizo

Wakala wa Serikali Mtandao ulioundwa na Sheria Nam. 12 ya mwaka 2019 imeshindwa kutekeleza malengo yake kiufanisi ya kusimamia uwepo wa Serikali Mtandao Zanzibar. Sababu za kushindwa kusimamia malengo yaliyokusudiwa na Serikali zinatokana na muundo, pamoja na uwezo wa

Wakala wa kusimamia kisheria. Hivo utafiti huu utajikita zaidi katika kutafuta suluhisho la usimamizi wa uwepo wa serikali mtandao Zanzibar.

1.4 Historia ya Serikali Mtandao

Serikali mtandao inatafsiriwa kuwa ni matumizi ya taarifa na mawasiliano ya teknolojia katika shughuli za uendeshaji wa shughuli za umma ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa umma pamoja na demokrasia katika nchi.[8] Matumizi ya Serikali mtandao kwa maana ya kuwafikia wananchi kupitia njia za kielektroniki, yaliibuka na kuanza kutumika duniani mwishoni mwa miaka ya 1990 baada ya kuimarika kwa intanenti na kuenea kwa kasi kupitia makongamano yaliyowashirikisha wataalamu kutoka maeneo mbali mbali.[9] Hata hivyo, matumizi ya kompyuta ndani ya taasisi za Serikali yameanza muda mrefu zaidi katika miaka ya 1970 lakini matumizi hayo hayakuwa yakilenga kufikisha huduma kwa wananchi badala yake yalikuwa ni kwa matumizi ya ndani tu.[10]

Kuanzishwa kwa serikali mtandao katika miaka ya 1990 kulilenga kutumia mifumo ya intanenti na teknolojia ya mawasiliano ya habari kwa Serikali kutoa huduma kwa umma kwa urahisi zaidi, kwa uhakika, kwa gharama nafuu na kwa wakati wowote bila ya kujali muda maalum ambao watumishi wa umma

---

[8] Åke Grönlund; Ten Years of E-Government: The 'End of History' and New Beginning; Swedish Business School Fakultetsgatan 1, 701 82 Örebro, Sweden; inapatikana Title (springer.com).

[9] Introducing e-GOV: History, Definitions, and Issues; Åke Grönlund Örebro University, ake.gronlund@esi.oru.se Thomas A. Horan, Claremont Graduate University, Communications of the Association for Information Systems (Volume 15, 2004)713-729 ukurasa wa 713, inapatikana (PDF) Introducing e-Gov: History, Definitions, and Issues (researchgate.net)

[10] Gore, Albert (1993). Reengineering Through Information Technology. Accompanying Report of the National Performance Review. Washington: Office of the Vice President

watakuwa kazini.[11] Mbali ya kutumia teknolojia katika kuwafikia wananchi katika utoaji wa huduma, pia Serikali mtandao ilikusudia kuimarisha utoaji bora wa huduma za umma kwa wananchi kuliko ilivyokuwa awali, kuongeza na kuimarisha ufikiaji wa wananchi kwa karibu zaidi na kuimarisha utendaji wa serikali ili kuleta ufanisi.[12]

Historia inaonesha kuwa mpaka miaka ya 1990, Serikali ya Marekani ambayo ni katika nchi za mwanzo kuingia kwenye serikali mtandao, ilijikita zaidi katika kutumia teknolojia ya habari kwa ajili ya matumizi ya watendaji na hakukuwa na mtizamo wa matumizi hayo ya teknolojia katika kutoa huduma au hata taarifa kwa umma.[13] Mwishoni mwa miaka ya 1990, mtizamo wa matumizi ya teknolojia ya habari ulibadilika na Serikali ya nchi hiyo iliweka mkazo zaidi wa matumizi ya teknolojia hiyo katika kutoa huduma kwa wananchi.[14]

kwa upande wa Afrika, Zimbabwe ilikuwa ni moja ya nchi za mwanzo barani Afrika zilizopata msaada wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa ajili ya kutathmini namna ya kuingia katika serikali mtandao mwaka 1999 na tathmini hiyo ilibaini na kupendekeza maeneo ya kuanza serikali mtandao kama mfumo wa malipo ya watumishi wa umma, usajili wa wananchi, mfumo

[11] Leon J. Osterweil, Lynette I. Millett, and Joan D. Winston, (Eds)Social Security Administration Electronic Service Provision; A Strategic Assessment; The National Academies Press, 2007, N.W., Washington, DC 20055, inapatikana http://www.nap.edu ukurasa wa 149

[12] Naome Rajah; E- Government in Zimbabwe: An Overview of Progress made and Challenges Ahead; Volume 6, No. 12, December 2015; Journal of Global Research in Computer Science, Research Paper, ukurasa wa 11. inapatikana http://rroij.com/global-research-in-computer-science.php

[13] Leon J. Osterweil, Lynette I. Millett, and Joan D. Winston, (Eds)Social Security Administration Electronic Service Provision; A Strategic Assessment; The National Academies Press, 2007, N.W., Washington, DC 20055, inapatikana http://www.nap.edu ukurasa wa 149

[14]Ibid, ukurasa wa 150

wa malipo ya pencheni, mfumo wa biashara wa kielektroniki.[15] Hata hivyo, utekelezaji wa wazo la kuingia kwenye serikali mtandao lilikumbwa na changamoto kubwa kutokana na ukosefu wa umeme katika maeneo mengi ya pembezoni mwa nchi.[16]

Kwa upande wa Tanzania, kumekuwa na jitihada za kuimarisha serikali mtandao ambazo zimekuwa zikitumika ili kuimarisha utoaji huduma kwa umma na kupunguza umasikini na kuimarisha utawala bora kwa kuwashirikisha wananchi kwa urahisi, kwa uwazi, kwa haraka na kwa wingi zaidi.[17] Hili linathibitishwa na Sera ya TEHAMA ya mwaka 2003 ambayo inaitambua serikali mtandao kama moja ya nyenzo muhimu ya kupunguza umasikini.[18]

Kwa upande wa Zanzibar, historia ya serikali mtandao ilianza kwa utungaji wa Sera ya Serikali Mtandao ya mwaka 2015. Sera hiyo iliweka msingi na mwelekeo wa Serikali kuanza matumizi ya serikali mtandao na kuelekeza kutungwa kwa Sheria mahsusi itakayosimamia suala la serikali mtandao. Mnamo tarehe 04 Disemba, 2019, Zanzibar iliandika historia mpya kwa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kupitisha Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao ambayo ilianzisha Wakala wa Serikali wa kusimamia masuala ya serikali mtandao, pamoja na kuweka msingi wa matumizi ya serikali mtandao katika

[15] Naome Rajah; E- Government in Zimbabwe: An Overview of Progress made and Challenges Ahead; Volume 6, No. 12, December 2015; Journal of Global Research in Computer Science, Research Paper, ukurasa wa 11. inapatikana http://rroij.com/global-research-in-computer-science.php
[16] Ibid, ukurasa wa 13.
[17] Øystein Sæbø; E-government in Tanzania: Current Status and Future Challenges; University of Agder, Norway, ukurasa wa 198-199 inapatikana LNCS 7443 - E-government in Tanzania: Current Status and Future Challenges (springer.com)
[18] *Ibid*.

taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mswada wa Sheria hiyo ulisainiwa na Rais wa Zanzibar tarehe 31 Disemba 2019 na hivyo kuwa Sheria.

Kabla ya kutungwa kwa Sera na Sheria hiyo ya Kuanzisha Wakala wa Serikali Mtandao mwaka 2015 na mwaka 2019, historia ya Zanzibar katika suala hilo la serikali mtandao inaonesha kuwepo kwa jitihada za kuanza matumizi ya serikali mtandao katika taasisi mbali mbali ikiwemo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), ZRB na ZSSF kwa kuweka mifumo mbalimbali ya upatikanaji wa taarifa. Kwa mfano, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), kwa kutambua changamoto ya upatikanaji wa taarifa kwa wanachama wa Mfuko huo hasa walio maeneo ya mbali na ofisi za Mfuko huo, ilianza kutumia Serikali mtandao kwa maana ya kutumia teknolojia kuwafikia wanachama wake bila ya wanachama hao kuhitajika kufika ofisi za Mfuko huo.[19] ZSSF imeweka mfumo ambao wanachama wake kwa kutumia kompyuta au hata simu ya mkononi (smart phone), wanaweza kupata taarifa zao za Mfuko popote walipo na hivyo teknolojia hiyo kurahisisha namna ya kuwafikia wananchi kwa urahisi.[20]

Aidha, Benki ya Watu Zanzibar ambayo ni benki ya Serikali, nayo ilianza kutumia teknolojia ya mawasiliano kuwafikishia huduma wananchi hata kabla ya kupitishwa kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao ambapo wananchi wanaweza kupata huduma za kibenki ikiwemo kufanya miamala ya kibenki kwa kupitia simu ya mkononi bila ya kuhitajika kufika katika matawi ya benki[21].

[19] Zanzibar Social Security Fund – Zanzibar Social Security Fund | Key to the future (zssf.or.tz)
[20] Ibid.
[21] ABOUT US – PBZ BANK LTD

Aidha, tangu Novemba 2011, kumekuwa na Ajenda ya Zanzibar kuelekea Serikali Mtandao,[22] ambayo ilikuwa ikisisitiza haja ya kuelekea kwenye Serikali mtandao kwa malengo yafuatayo:

(a) Kuwezesha wazanzibari kupata huduma za Serikali kupitia teknolojia ya mawasiliano katika wakati wowote;

(b) Kuondoa ulazima wa wananchi kusafiri kufuata huduma katika ofisi za Serikali, mbali na maeneo wanayoishi;

(c) Kuongeza uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi wake;

(d) Kurahisisha uwekaji wa kumbukumbu katika taasisi za Serikali;

(e) Kuwaondolea wananchi wenye ulemavu au wagonjwa usumbufu wa kulazimika kufuata huduma za umma katika ofisi za Serikali;

(f) Kuwawezesha wazanzibari wanaoishi nje ya nchi (diaspora) kupata taarifa wanazozihitaji na kuwasiliana kwa urahisi na taasisi za umma wakiwa nje ya nchi hasa katika masuala ya kiuchumi.

Historia ya Serikali mtandao duniani iliingia katika hatua nyengine baada ya mlipuko wa maradhi ya Korona yaliyosababisha uzuiaji wa mikusanyiko ya watu katika taasisi za huduma ikiwemo taasisi za umma. Pamoja na nchi mbali mbali kufunga taasisi zinazotoa huduma zikiwemo ofisi za Serikali, bado kumekuwa na umuhimu wa wananchi kupatiwa huduma na taasisi za umma na hivyo matumizi ya serikali mtandao kuonekana ni mbadala mzuri katika kufikisha huduma kwa wananchi.[23] Nchi ya Afrika Kusini ambayo ni miongoni mwa nchi zilizoathirika zaidi na maradhi hayo ya Korona katika Bara la Afrika

[22] Zanzibar Electronic Government Agenda; A Way Forward; 18 November 2011 Available at (1) (PDF) Zanzibar eGovernment Agenda - A Way Forward | Mzalendo Mtanzania - Academia.edu

[23] COVID-19 and E-Governance: Lessons from South Africa Author(s): ISABEL BOSMAN South African Institute of International Affairs (2021) Stable URL: https://www.jstor.org/stable/resrep29596 Accessed: 29-01-2022 02:01 UTC, ukurasa wa 2.

na hivyo kuzuia mikusanyiko ya watu kwa muda mrefu, ilipiga hatua kubwa zaidi katika matumizi ya serikali mtandao.[24] Kuongezeka kwa matumizi ya Serikali mtandao duniani wakati wa maradhi hayo ya korona kunatokana na ukweli kuwa pamoja na haja iliyokuwepo ya kuzuia mikusanyiko ya watu ili kuyadhibiti maradhi hayo, bado isingewezekana kusitisha utoaji wa huduma kwa umma.

1.5 Hadidu Rejea

Katika kufanya utafiti huu Hadidu Rejea zifuatazo zilizingatiwa:

(a) Kufanya utafiti wa kina katika taratibu za usimamizi wa Serikali mtandao;

(b) Kuangalia uzoefu wa sheria za nchi mbali mbali kuhusiana na masuala ya Serikali mtandao na kuangalia namna uzoefu huo huo unavyoweza kutumika kwa mazingira ya Zanzibar;

(c) Kuangalia sera na sheria mbali mbali za Zanzibar zinazohusiana na Serikali mtandao na utafiti wa Serikali mtandao unavyoweza kusaidia kuweka mazingira mazuri ya sheria katika matumizi ya mitandao na maeneo mengine ya kitehama;

(d) Kupitia mikataba ya kimataifa na uzoefu wa nchi mbalimbali inayohusiana na eneo hili la utafiti na kuangalia mambo ya msingi yanayoweza kuzingatiwa katika Sheria itakayopendekezwa.

(e) Kutoa mapendekezo yanayofaa ya kisheria na kisera kwa ajili ya kutatua changamoto zinazokwaza na namna ya kuweka mfumo wa kisheria utakaoimarisha masuala ya Serikali mtandao.

[24] Ibid, ukurasa wa 3.

1.6 Malengo ya Utafiti

Lengo la kufanya utafiti huu ni kuangalia mapungufu ya Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Nam. 12 ya mwaka 2009 na kupendekeza marekebisho yake Serikalini. Mapendekezo hayo yatazingatia:

(a) Kupendekeza utaratibu wa kisheria ili kuziwezesha taasisi za Serikali ziweze kujiendesha shughuli zake kimtandao kwa ufanisi zaidi;

(b) Kupendekeza utaratibu utakaoziwezesha taasisi za Serikali ziweze kutoa huduma kwa njia ya haraka na ufanisi;

(c) Kusaidia utoaji wa huduma na upatikanaji wa huduma kwa urahisi na haraka kwa muda mfupi;

(d) Kuwezesha Serikali kufanya mawasiliano ya kibiashara kwa uwazi na kupunguza uwezekano wa rushwa katika taasisi za umma

(e) Kuimarisha misingi ya utawala bora.

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu wa kuanzishwa kwa Serikali Mtandao Zanzibar utasaidia katika mambo yafuatayo:

(a) Utasaidia kuleta mapendekezo ya kuanzishwa kwa taasisi imara itakayoweza kusimamia uanzishwaji wa Serikali mtandao katika taasisi za Serikali;

(b) Kutakuwa na maendeleo endelevu katika sekta mbali mbali katika uchumi wa nchi;

(c) Kuwepo mawasiliano ya haraka ya kibiashara baina ya Serikali na wafanyabiashara, waajiri na waajiriwa, watumishi wa umma na Serikali, wananchi na Serikali, Serikali moja na nyengine;

(d) Kuboresha uaptikanaji wa huduma katika taasisi za Serikali na kusaidia katika kuleta maendeleo katika taasisi hizo;

(e) Itasaidia kuziba miaya ya rushwa;

(f) Itarahisisha mawasiliano kutoka taasisi moja kwenda nyengine kwa ufanisi, uwazi na kwa muda mfupi.

1.8 Njia za Utafiti

Katika utafiti huu njia zifuatazo zilitumika kukusanya maoni na kupata taarifa zilizoweza kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika utafiti.

1. Kufanya mikutano na wadau walioainishwa kwa ajili ya kutoa maoni.
2. Kuhoji baadhi ya wadau mbali mbali wakiwemo wataalam wa sekta ya mawasiliano ya habari.
3. Kupitia Sheria mbalimbali na Rejea ambazo zinazungumzia masuala ya Serikali mtandao.
4. Kukusanya taarifa mbali mbali za Serikali na taasisi zake zinazohusiana na utafiti huu na kuzilinganisha na malengo ya hadidu rejea za utafiti pamoja na kuangalia uzoefu wa nchi nyengine.

1.9 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kupendekeza namna ya kuimarisha Serikali mtandao kwa taasisi za umma pekee Zanzibar, na haugusi masuala ya kimtandao kwa sekta binafsi. Aidha, pamoja na utafiti huu kuangalia uzoefu wa maeneo mbali mbali, utafiti huu umejikita kwa upande wa Zanzibar pekee. Vilevile utafiti huu ulichukuwa muda wa miezi mitatu mpaka kufikia mwisho wake lakini kutokana na kuwepo kwa changamoto zilizo nje ya uwezo wa watafiti hivyo muda uliongezeka zaidi ya vile ulivyopangwa.

SURA YA PILI

2.0 DHANA YA SERIKALI MTANDAO

2.1 Utangulizi

Serikali Mtandao (e-government) ni mojawapo ya vipaumbele muhimu vya Serikali duniani kote ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na kuendeleza mwingiliano na ushirikiano katika idara za serikali.[25] Serikali Mtandao inatumika kuweka mchakato ambao Serikali hutumia kufikia ufanisi Serikalini, kuruhusu wananchi kupata huduma zaidi, huku ikileta uwajibikaji zaidi wa Serikali kwa umma.[26] Utekelezaji wa Serikali Mtandao pia unachukuliwa kuwa mfumo mgumu wa kijamii unaojumuisha masuala ya kijamii na kiuchumi. [27]

2.2 Maana ya Serikali Mtandao

Serikali mtandao maana yake ni matumizi ya mawasiliano kama vile kompyuta na mtandao katika kutoa huduma kwa raia au watu wengine katika nchi.[28] Maana nyengine ya Serikali mtandao ni mawasiliano ya kieletroniki katika kutoa huduma kwa jamii ili kufikia Serikali yenye ufanisi.[29]

---

[25] Pardo TA, Nam T, Burke GB. E-government interoperability interaction of policy, management, and technology dimensions. *Soc. Sci. Comput. Rev.* 2012;30(1):7–23. doi: 10.1177/0894439310392184

[26] Napitupulu D, Sensuse DI. The critical success factors study for e-government implementation. *Int. J. Comput. Appl.* 2014;89(16):23–32.,

[27] Siddique W. Critical success factors affecting e-government policy implementation in Pakistan. *E-J. E-Democr. Open Gov.* 2016;8(1):102–126

[28]Sera ya serikali mtandao ya mwaka 2015 uk 3

[29] The e-Government Imperative. Paris: OECD (2003) e-Government Studies. ISBN 92-64-10117-9 ukurasa wa 23

Maana ya Serikali mtandao ni dhana pana na inahusu matumizi ya teknolojia na utoaji wa huduma katika uendeshaji wa shughuli za Serikali. Ingawa dhana hii kiujumla inahusisha matumizi ya mtandao Serikalini, au teknolojia na huduma za kielektroniki zisizo za mtandao kama vile simu, nukushi n.k.[30] Serikali Mtandao inaweza kutekelezwa kwa mafanikio ikiwa inadhibitiwa na mfumo wa kisheria, masuala ya kisheria yanayohusu usalama wa mtandao, ulinzi na usahihi wa taarifa za kidijitali, usiri wa taarifa (data) binafsi. Sheria zinazoweka ukomo na uwezo wa Serikali dhidi ya mtu binafsi katika suala la udhibiti wa taarifa za kibinafsi zinapaswa kupitishwa.[31]

Prof. Dele Olowu, akiandikia ECA, anafafanua Serikali Mtandao kama majukwaa yote ya teknolojia ya habari na mawasiliano na maombi katika sekta ya umma ya matumizi ya mtandao kwa ajili ya kuwasilisha taarifa na huduma za serikali kwa wananchi.[32] Aidha, dhana ya serikali ya mtandao ni serikali iliyojidhatiti kutoa huduma kwa njia ya kieletroniki kwa wananchi wake ili kuharakisha juhudi za maendeleo kwa taifa na wananchi kwa ujumla.[33] Maana yake serikali kuachana na mfumo au tabia ya kuwasiliana kwa njia ya maandishi kupitia karatasi (paper based system).

Ingawa serikali ya mtandao mara nyingi hufafanuliwa kama “Serikali ya mtandaoni” au “Serikali ya mtandao”, teknolojia nyingi zisizo za mtandao za

---

[30] *Gregory G. Curtin*, *Michael Sommer*&*Veronika Vis-Sommer* (2003), The World of E-Government, Routledge

[31] Layne, K. & Lee, J. (2001). "Developing Fully Functional E-Government: A Four Stage Model." Government Information Quarterly. 18, 122-1

[32] Olowu 2004 Quoted in “Chapter 12 :Elecgtronic Government and Rural Development in Anglophone West Africa, by Kehinde David Adejuwon, Sodhi, Inderjeet Singh (ed) (2014) “Emerging Issues and Prospects in African E-Government, IGI Global. ukurasa 160

[33] Thomas A. Horan Introducing e-Gov: History, Definitions, and Issues, volume 15, June 2005 pg 718

Serikali ya kielektroniki kama vile simu, faksi, huduma ya ujumbe mfupi (SMS), huduma ya ujumbe na mitandao isiyo na waya inahusika.[34] Aidha huduma za televisheni na uwasilishaji wa huduma za serikali kwa njia ya redio zinaweza kutumika katika muktadha wa serikali mtandao.[35] Utayari wa Serikali ya kielektroniki katika nchi zinazoendelea unategemea hali nzuri za kisiasa, kitamaduni, kijamii, kiuchumi na kiteknolojia ambazo zinahitaji kuwepo ili mabadiliko ya dhana ya serikali ya kielektroniki ichukuliwe.[36]

Kwa maneno mengine, Serikali mtandao maana yake ni msaada wa kuchochea utawala bora. Kwa hivyo, malengo ya utawala wa kielektroniki ni sawa na malengo ya utawala ubora. Utawala bora unaweza kuonekana kama utekelezaji wa kiuchumi, kisiasa, na mamlaka ya utawala ili kusimamia vyema masuala ya nchi katika ngazi zote.[37]

Katika OECD, neno Serikali mtandao linafafanuliwa kama matumizi ya taarifa na teknolojia ya mawasiliano na hasa mtandao, kama chombo cha kufikia taarifa za Serikali.[38]

Neno Serikali Mtandao halina jibu rahisi kwakuwa linachukua pande nyingi katika Uongozi, sera, uchumi ushindani, elimu, huduma za kidijitali za raia,

[34] Anttiroiko, A i-Veikko. and Malkia, Matti. 2006. Encyclopedia of digital government. Hershey, PA: Idea Group Reference (IGI)
[35] Heeks, Richard. and Bailur, Savita. 2007. Analyzing e-governmen research: perspectives, philosophies, theories, methods, and practice. Government Information Quarterly, 24(2):243- 265
[36] Aziz NAA, Manab NA, Othman SN. Critical success factors of sustainability risk management (SRM) practices in Malaysian environmentally sensitive industries. *Soc. Behav. Sci.* 2016;2016(219):4–11.
[37] M Backus 'E-governance in developing countries', IICD Research Brief No 1, March 2001, website: www.iicd.org; see also P Norris 'The worldwide digital divide: information poverty, the Internet and development' Harvard University, 2000. Available from http://www.ksg.harvard.edu/iip/governance/psa2000dig.pdf.
[38] OECD 'The E-government imperative', in OECD E-Government Studies. OECD, Paris, 2003, ukurasa wa 22

shughuli za ndani za serikali, dijitali demokrasia, na teknolojia wezeshi kwa kila mwelekeo.[39]

2.3 Umuhimu wa Serikali Mtandao

Serikali mtandao inatoa fursa mpya ya upatikanaji wa taarifa moja kwa moja kwa raia na inasaidia huduma kwa raia. Kwa ufupi Serikali mtandao ni matumizi ya taarifa za kimawasiliano ya kimtandao ili kuzifanya huduma kwa jamii ziwe bora zaidi.[40] Ni vigumu kutambua ukuaji wa Serikali, ingawa ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini, ustawi wa wananchi pamoja na uendelevu wa taifa, hauwezi kufikiwa bila ya kuwa na Serikali Mtandao inayofanya kazi kwa ufanisi.[41] Marekebisho ya sekta ya umma, na mabadiliko yake katika sekta ya umma ya kidigitali, yanaonekana wazi kupitia Serikali Mtandao,[42] na katika sekta ya umma ni muhimu ili kutambua mambo yanayoathiri ufanisi wa Serikali na hali ilivyo Serikalini. [43]

Katika ushirikiano wa kiuchumi wa kimataifa na ushindani, utekelezaji wa ICT unazidi kuwa muhimu kwa ukuaji endelevu wa uchumi wa nchi zinazoendelea hasa usambazaji wa uvumbuzi wa serikali,[44] katika nchi zinazoendelea

---

[39] Presented at the Seville European Council on 21 and 22 June 2002.
[40] Shareef MA, Yogesh NA, Dwivedi K. Examining adoption behavior of mobile government. *J. Comput. Inf. Syst.* 2012;53:39–49
[41] Hanna NK. *Transforming Government and Building the Information Society: Challenges and Opportunities for the Developing World.* New York: Springer; 2010
[42] Savoldelli A, Codagnone C, Misuraca G. Understanding the e-government paradox: learning from literature and practice on barriers to adoption. *Gov. Inf. Q.* 2014;31:63–71.
[43] Xu X, Zhang W, Barkhi R. IT infrastructure capabilities and IT project success: a development team perspective. *Inf. Technol. Manag.* 2010;11:123–142. doi: 10.1007/s10799-010-0072-3
[44] Zoo H, de Vries HJ, Lee H. Interplay of innovation and standardization: exploring the relevance in developing countries. *Technol. Forecast. Soc. Chang.* 2017;118:334–348.

umuhimu wa Serikali mtandao ulionekana katika miongo miwili iliyopita baada ya kuwanufaisha wananchi na Serikali.[45]

Kwa wananchi, umuhimu mwengine ni kuboresha utoaji wa huduma kwa umma na kupanua njia za mawasiliano, na kuongeza huboresha ufanisi pamoja na kupunguza urasimu.[46] Serikali inaruhusu upatikanaji wa huduma za kisasa zinazoleta ufikiaji na urahisi kwa raia, na hivyo kuwawezesha kuwa na maendeleo ya kidijitali na kukuza uthamini wa raia wa teknolojia ya habari.[47]

Kipimo cha thamani ya umma kinazingatia uimarishaji wa huduma tofauti zinazotolewa na Serikali mtandao. Kwa mfano, kupitishwa kwa majukwaa ya kidijitali kwa madhumuni ya kuboreshwa kwa mapendekezo ya huduma za umma na zinazoweza kuwasilishwa, kufikiwa kwa utoaji wa huduma za umma,[48] Uboreshaji unaowezeshwa na Serikali ya mtandao ni kwa mfano, katika suala la huduma bora kwa raia, muitikio, ufanisi, na kupunguza gharama na ushirikiano katika utoaji wa huduma za umma.[49]

---

[45] Ali KE, Mazen SA, Hassanein EE. A proposed framework for the organization readiness assessment of IT innovation adoption in e-government environment. *Int. J. Intell. Comput. Inf. Sci.* 2017;17(2):33–50

[46] Olaniyi, E.: Digital government: ICT and public sector management in Africa. In: New Trends in Management: Regional and Cross-Border Perspectives, pp. 269–286. London Scientific Publishing, London (2018)

[47] Ahn MJ, Bretschneider S. Politics of e-government: e-government and the political control of bureaucracy. *Public Adm. Rev.* 2011;71(3):414–424.

[48] Latifa Alzahrani, Wafi Al-Karaghouli, Vishanth Weerakkody
Analysing the critical factors influencing trust in e-government adoption from citizens' perspective: A systematic review and a conceptual framework, 2016 Published by Elsevier Ltd.
https://tarjomefa.com/wp-content/uploads/2018/05/9076-English-TarjomeFa.pdf

[49] Richard Heeks (2001) "Understanding e-Governance for Development, Institute for Development Policy and Management" , Paper No. 11
Understanding e-Governance for Development Richard Heeks1 IDPM, University of Manchester, UK 2001
https://deliverypdf.ssrn.com/delivery.php?ID=348094069068098088118090123125012024022087061054024018026094003006065026028028103106002063005047108007015084101078094065122029046053082082007100065091067111003123030095085017074118113089083085110066109073099121006127095084000123071099076068004025101119&EXT=pdf&INDEX=TRUE

Utumishi wa umma, mwelekeo wa raia, na kiwango cha huduma, ni mambo ya msingi katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Aidha, mtazamo wa wananchi ni kupata huduma bora na za haraka kwa umma na mwelekeo wa watumiaji na usimamizi mpya wa Serikali mtandao kwa umma.[50]

2.4 Maeneo ya Kuzingatiwa

Kuna mambo kadhaa yanayopaswa kushughulikiwa kwa ufanisi wa utekelezaji wa huduma za umma za kielektroniki,[51] ikiwemo uwepo wa rasilimali, kama vile miundombinu duni ya ICT, na mtaji wa kutosha wa Teknolojia ya Habari (IT) ili kuendeleza maendeleo na uboreshaji wa ICT,[52] umuhimu wa kimkakati na miundombinu ya msaada wa IT.[53]

Aidha eneo jengine ni kuongezeka kwa ushiriki wa umma katika michakato ya kufanya maamuzi na kwa kutumia TEHAMA kwa upitishaji wa mafanikio wa utawala na huduma za serikali,[54] hali ya kisiasa, vipimo vya kitamaduni, maendeleo ya kiteknolojia, na mabadiliko ya taasisi za umma yamewekwa kusaidia na kuendesha mabadiliko katika idara za Serikali,[55] uratibu wa shughuli nyingi Taasisi za umma, ushirikiano wa karibu kati ya wafanyakazi, wataalamu wa IT, pamoja na matumizi ya ICT.[56]

---

[50] Prof. Manjot Kaur1 , Dr. Amitoj Singh, E-Government: Study of Factors significantly affects Adoption and Acceptance in State of Punjab, (IJCSIT) International Journal of Computer Science and Information Technologies, Vol. 6 (5) , 2015, 4542-4548
[51] Ziemba E, et al. Factors influencing the success of e-government. *J. Comput. Inf. Syst.* 2016;56(2):156–167
[52] Michael P, et al. e-Government implementation challenges in developing countries: the project manager's perspective. *Int. J. Public Adm. Manag. Res. (IJPAMR)* 2018;4(3):1–17]
[53] Othman MH, Razali R. Whole of government critical success factors towards integrated e-government services: a preliminary review
[54] Yadav J, Saini AK, Yadav AK. Measuring citizens engagement in e-Government projects – Indian perspective. *J. Stat. Manag. Syst.* 2019;22(2):327–346. doi: 10.1080/09720510.2019.1580908
[55] *J. Pengur.* 2018;2018(53):73–82. doi: 10.17576/pengurusan-2018-53-07
[56] Ziemba E, Papaj T, Żelazny R. A model of success factors for e-government adoption – the case of Poland. *Issues Inf. Syst.* 2013;14:87–100

Zaidi ya hayo, wakala mtandao ni mradi wa muda mrefu ambao unahitaji mbinu shirikishi ya utekelezaji, zaidi katika nchi zinazoendelea.[57]

2.5 Maeneo ya mabadiliko ya Serikali Mtandao

Eneo la ndani ni matumizi ya ICT kuboresha ufanisi wa kazi za ndani na michakato ya Serikali. Kwa mfano, Serikali mtandao huunganisha idara na wakala mbalimbali, hivyo kufanya taarifa kutiririka kwa haraka na kwa urahisi zaidi kati ya idara mbalimbali za Serikali na hata taasisi binafsi zitakazounganishwa na mfumo.[58]

Eneo la nje linamaanisha ni jinsi ICT inavyofungua uwezekano mpya kwa serikali kuwa wazi zaidi kwa raia na wafanyabiashara na wananchi wengineo kupitia usambazaji, na ufikiaji wa taarifa nyingi zaidi zinazokusanywa na kutolewa na Serikali. Uhusiano unaelezea jinsi matumizi ya ICT yanavyoweza kuleta mabadiliko ya kimsingi katika uhusiano kati ya raia na Serikali, na athari kwa mifumo na miundombinu ya Serikali.[59]

2.6 Lengo la Serikali Mtandao

Lengo la Serikali Mtandao limegawika katika sehemu mbili (2), sehemu ya kwanza ni ya uwasilishaji wa huduma kwa jamii ambapo kwa huduma, ni muhimu kuendeleza lengo la malipo ya Serikali ambayo yanaruhusu kupokea fomu za maombi mtandaoni pamoja na malipo ya ada mbalimbali kwa huduma

[57] Ebrahim Z, Irani Z. e-Government adoption: architecture and barriers. *Bus. Process Manag. J.* 2005;11(5):589–611. doi: 10.1108/14637150510619902
[58] Cook, M., & Harrison, T. M. (2015). Using public value thinking for government IT planning and decision making: A case study. Information Polity, 20(2/3), 183–197
[59]Prakash, N., Jaiswal, M., & Gulla, U. (2009). A conceptual framework for measuring public value of enterprise applications. Electronic Government, an International Journal, 6(3), 307–326.

za Serikali na sehemu ya pili ni utekelezaji wa utoaji huduma ambapo programu muhimu, maswali ya takwimu na uwasilishaji yanafanyika.[60]

Tafiti kuhusu serikali Mtandao zimeeleza kuwa lengo kubwa ni kuleta mageuzi kwa wadau na wananchi, na zinazingatia kile ambacho Layne na Lee wameeleza kama vielelezo vya hatua za ukuaji kwa serikali mtandao inayofanya kazi kikamilifu.[61] Lengo jengine ni kuwa na mfumo mzuri wa usimamizi wenye kuimarisha usimamizi wa taarifa, kuimarisha utoaji huduma na kuimarisha upatikanaji na ushiriki wa wadau mbalimbali.[62] Malengo kama vile ufanisi, ufanisi, na uwezekano wa serikali kwa kiwango cha juu zaidi hutegemewa katika Serikali Mtandao.[63]

2.7 Matumizi ya Serikali Mtandao

Utafiti unaonesha kuwa dhana ya Serikali mtandao ina matumizi mengi kwa mfano, katika kufanya maamuzi ya kimahkama, katika kutoa huduma na utoaji thamani ya bidhaa. Hata hivyo dhana ya Serikali mtandao kwa sasa inakwenda mbali zaidi ikihusisha huduma bora za Serikali kwa jamii na kurahisisha mabadiliko katika taasisi na kuonesha wajibu wa Serikali kwa raia zake.

---

[60] Ndou. V, (2004) E-government for developing countres: opportunities and challenges. The Electronic Journal on Information Systems in Developing Countries. Vol. 18 no 1. PP 1-24

[61] Layne, K. & Lee, J. (2001). "Developing Fully Functional E-Government: A Four Stage Model." Government Information Quarterly. 18, 122-1

[62] Abdulrazaq Kayode Abdulkareem
Challenges of E-Government Implementation in the Nigerian Public Service, Journal Of Creative Writing Volume 1, ISSUE 4 2015, PP 45-56, https://www.researchgate.net/profile/Abdulrazaq-Abdulkareem/publication/292151098_Challenges_of_E-Government_Implementation_in_the_Nigerian_Public_Service/links/56ab3eb308aed5a0135abe91/Challenges-of-E-Government-Implementation-in-the-Nigerian-Public-Service.pdf?origin=publication_detail

[63] Nkohkwo QN, Islam MS. Challenges to the successful implementation of e-government initiatives in Sub-Saharan Africa: a literature review. *Electron. J. E-Gov.* 2013;11:253–267

Serikali mtandao inaweza kutekelezwa kwa mafanikio ikiwa inadhibitiwa na mfumo wa kisheria, masuala ya kisheria yanahusu usalama wa mtandao, ulinzi na usahihi wa taarifa za kidijitali, usiri wa taarifa (data) binafsi. Sheria zinazoweka ukomo na uwezo wa Serikali dhidi ya mtu binafsi katika suala la udhibiti wa taarifa za kibinafsi zinapaswa kupitishwa.[64] Serikali mtandao pia inaangazia uwezekano wa kuleta mabadiliko kwa utawala na kuimarisha utoaji wa huduma.[65]

2.8 Faida za Serikali Mtandao

Serikali kupunguza gharama za uendeshaji na kusaidia kukuza pato la nchi, ili kufikia lengo hilo Serikali inapaswa kuanzisha njia mpya za utoaji wa huduma kwa njia ya mtandao na njia za kieletroniki ili wananchi waweze kupata huduma moja kwa moja bila ya kufuatilia Mamlaka zinazohusika kutoa huduma hizo kama ulipaji wa kodi na shughuli nyengine za kijamii.[66] Mbali na faida hizi, faida nyengine ni pamoja na:

(a) Kupata mawasiliano kwa urahisi katika taasisi za Serikali na kwa umma.

Maendeleo ya kibiashara yatakuwa kwa urahisi kutokana na kuwepo kwa mawasiliano ya haraka. Kwa mfano mikataba ya kibiashara yanaweza kufanywa moja kwa moja kwa njia ya mtandao. Vile vile Serikali ikitangaza zabuni kwa njia ya mtandao itawezesha wafanyabiashara wakubwa na wadogo kuweza kushindania zabuni hiyo, hali hii itapunguza muda na gharama za

[64] Layne, K. & Lee, J. (2001). "Developing Fully Functional E-Government: A Four Stage Model." Government Information Quarterly. 18, 122-1
[65] United Nations. (2013). United Nations E-government Survey 2012. New York: United Nations
[66]ibid

ufatiliaji. Aidha biashara inayoweza kufanywa kwa njia ya mtandao inafanyika kwa uwazi, haraka zaidi, na katika hali ya ubora. Na pia inaweza kuondosha upendeleo na ubaguzi. Kwa upande wa biashara inayohusiana na zabuni inaweza kusaidia kupunguza uwezekano wa mianya ya rushwa.

(b) Kurahisisha mawasiliano baina ya taasisi moja na nyengine.

Maendeleo ya Serikali yanategemea muunganiko wa taasisi zake kutoa huduma kwa jamii na kuhakikisha malengo ya Serikali yanafikiwa kwa kiasi kikubwa. Muunganiko wa taasisi hizi katika mawasiliano utazifanya taasisi hizi kufanyakazi bila ya mgongano wa kiutendaji na migongano ya kimaslahi baina ya taasisi za Serikali. Kila taasisi itakuwa inajua majukumu yake ya kimsingi ya kazi. Vile vile itawasaidia raia kujua aina gani za huduma zinaweza kupatikana katika taasisi husika. [67]

Muelekeo wake ni kurahisisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa mfano wananchi wataweza kupata huduma mbalimbali kwa njia ya kieletroniki kama kulipa ada za umeme, leseni, huduma za shule, wafanyakazi kuweza kujua maeneo yao ya kazi, mishahara. Kwa upande wa biashara wananchi wanaweza kuingia katika mikataba na serikali kwa njia ya kieletroniki.[68]

Serikali ya kimtandao itawapa fursa wananchi zaidi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiserikali pia wananchi watashirikishwa kwa uwazi zaidi kwa kutumia njia ya kieletroniki kutoa maoni yao juu ya uendeshaji wa serikali au kutoa maoni juu ya huduma zinazotolewa na serikali kwa wananchi.[69]

[67] The Advantages and Disadvantages of E-Government | E-SPIN Group (e-spincorp.com)
[68] ibid
[69] ibid

Wananchi watapata fursa za wazi kwa kuishauri serikali kwa kutumia Serikali mtandao na kupata nafasi ya kupendekeza mambo yanayoweza kusaidia taifa katika huduma za uzalishaji mali, elimu, matibabu na maeneo mengine ya maendeleo.

Serikali kwa upande wake itapata fursa ya kujua mambo mengi kuhusu wananchi wake, kwa mfano kujua makaazi ya raia zake, pamoja na mambo yote yanayohusu wananchi katika eneo husika. Mbali na kutoa huduma kwa urahisi na ubora kwa njia ya mtandao. Serikali mtandao inaweza kuwawezesha wananchi kupata taarifa kwa haraka, urahisi na kwa wakati. Upelekaji wa taarifa kwa wananchi kwa haraka na kwa wakati ni moja ya misingi ya utawala bora ambayo ndio msingi mkuu wa demokrasia.[70]

2.9 Hatua za Serikati Mtandao

Hatua ya kwanza ya msingi imetawala mfumo wa kinadharia unaotumika katika mifumo ya serikali mtandao, ingawa, miundo hii inaonekana kuwa ya kimaeneo na kutoa mwelekeo au kutathmini maendeleo kielektroniki katika eneo fulani.[71] Benin, Burkina Faso, Cameroon, Cote d'Ivoire, Ghana, Kenya, Mauritania, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Rwanda, Senegal, Sierra Leone, Swaziland, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe wanaonekana kuwa katika hatua hii. [72]

[70] ibid

[71] Moon, M. J. (2002). "The Evolution of E-government Among Municipalities: Rhetoric or Reality?" Public Administration Review. 62, 42

[72] Watson and Mundy, 2001. Watson, Richard. T and Mundy, Bryan. 2001. A strategic perspective of electronic democracy Communication of the ACM 44(1):27-

Hatua ya Pili ni taarifa za mtandaoni zenye nguvu na zilizoimarishwa hutolewa kwa raia, hatua ambayo inahitaji mawasiliano kama njia moja muhimu.[73] Tovuti za Mtandao kwa mfano zimeundwa ili kuunganisha shughuli na michakato ya serikali na kuwezesha muingiliano wa mtandaoni kati ya wananchi, wafanyabiashara na wadau wengine. Benin, Burkina Faso, Cameroon, Cote d'Ivoire, Ghana, Kenya, Mauritania, Msumbiji, Namibia, Nigeria, Rwanda, Senegal, Sierra Leone, Swaziland, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe wanaonekana kuwa katika hatua hii.[74]

Hatua ya tatu hutoa muingiliano na muonano kati ya wadau wote. Katika hatua hii, Serikali inaunganisha huduma kamili za serikali, hutoa njia ambayo inategemea mahitaji na kazi. Kwa mfano, wananchi wanaweza kusajili taarifa za vizazi, kutuma maombi ya malipo, kulipa kodi, kufikia sheria za serikali na kupata taarifa kuhusu shughuli za wawakilishi wao bungeni na Serikali za mitaa bila kuondoka katika nyumba na ofisi zao.[75] Nchi za Mauritius na Afrika Kusini zipo katika hatua hii.

Ili hatua hizi zifanyekazi vizuri, Serikali inapaswa kuweka miundo mbinu itakayosaidia mawasiliano ya kimtandao ili huduma kwa Serikali na kwa jamii ziweze kufanyika kwa urahisi.[76] Serikali katika kuhakikisha lengo hilo linafikiwa itahitajika kuandaa wataalamu wa kutosha wenye fani za kieletroniki, kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya

---

[73] Spinello, R. (2002). Regulating Cyberspace. Westport, CT: Quorum Books

[74] Layne, K. & Lee, J. (2001). "Developing Fully Functional E-Government: A Four Stage Model." Government Information Quarterly. 18, 122-1

[75] Melitski, J. (2003). "Organizational Capacity and E- government Performance." Public Performance and Management Review. 26, 325

[76] ibid

kieletroniki na fedha kwa ajili ya matengenezo ya vifaa hivyo. Pia serikali italazimika kununua vifaa vya kieletroniki vitakavoweza kutoa mawasiliano hayo kwa nji ya mtandao.

2.10 Tofauti ya Mawasiliano ya Habari na Serikali Mtandao

Tofauti inapaswa kuwekwa kati ya wakala mtandao na teknolojia ya habari Serikalini. Matumizi ya kompyuta, mageuzi ya kazi za ndani za Serikali kwa uchambuzi wa taarifa (data) hasa taarifa za fedha, imekuwa ikitekelezwa katika sehemu nyingi katika Serikali za Kiafrika kwa karibu miaka 50. [77]

Mfumo wa Serikali mtandao ni tafauti na mtizamo wa zamani kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, ambayo sio tu inasaidia kubadilisha utendaji kazi wa Serikali kwa kuchambua taarifa, kuwasiliana na kupata takwimu pekee bali pia Serikali Mtandao ipo katika mwelekeo wa mawasiliano ya taarifa, uwekaji wa data na kupelekea kuwa kiunganishi cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii na utawala bora kinyume na michakato ya kazi peke yake.[78]

2.11 Aina za Serikali Mtandao

Miundo inayotumiwa kuonesha serikali ya mtandao inapendekeza kuwa kuna aina kadhaa tofauti katika ukuzaji wa serikali mtandao, Serikali kutokana na aina ya huduma ya Serikali inayotoa kwa jamii husika.[79]

[77] West, D.M. (2005a). Digital Government: Technology and Public Sector Performance. Princeton, NJ: Princeton University Press

[78] E-government in Africa: An Overview of Progress Made and Challenges Ahead By Nancy J. Hafkin Consultant Prepared for the UNDESA/UNPAN workshop on electronic/mobile government in Africa: Building Capacity in Knowledge Management through Partnership, held at the United Nations Economic Commission for Africa, 17-19 February 2009, p/2

[79] https://www.e-spincorp.com/definition-and-type-of-e-government/

(a) Serikali kwa Mwananchi (G2C): hii inajumuisha kuzungumza na wananchi kwa kuwapatia maelezo ya shughuli za sekta ya umma, kuongeza mchango wa wananchi katika kutoa maoni, kufanya maamuzi na kuboresha huduma za umma zinazotolewa kwa wananchi, kuweka uwazi katika upatikanaji wa huduma zinazotolewa na Serikali na upatikanaji wa huduma kwa gharama nafuu. Muundo huu unajumuisha maeneo kama "e-banking, e-procurement, e-education na e–health" na maeneo mengineyo. Miongoni mwa huduma za muundo ni usambazaji wa habari, kutoa leseni, vyeti vya kuzaliwa/vifo/ndoa, taarifa za kodi na ufunguaji wa jalada mahakamani, matokeo ya ufaulu katika mitihani katika ngazi mbali mbali za elimu na utoaji wa huduma za maktaba kimtandao. Mfano wa nchi zinazotumia muundo huu na kupata mafanikio ya hali ya juu katika bara la Afrika ni Serikali ya Mtandao ya Rwanda na Kituo cha Mtandao cha Serikali ya Mauritius.[80]

(b) Serikali na taasisi za Biashara (G2B): Muundo huu unajumuisha huduma zinazotolewa na Serikali zinawahusu wafanyabiashara katika harakati zao za kibiashara. Mfano wa huduma hizo ni kama vile kupakua fomu za maombi ya leseni, malipo ya kodi, manunuzi ya vifaa kati ya Serikali na wasambaji.

(c) Serikali kwa Serikali (G2G): Muundo huu pia unajulikana kama Utawala wa kielektroniki, muundo unahusisha kutumia teknolojia ili kuimarisha utawala wa umma kwa utoaji wa huduma bora. Vile vile muundo huu unatumika hasa katika ugatuaji wa shughuli za Serikali kutoka Serikali kuu kwenda Serikali za mitaa.

---

[80] Richard Amaechi Onuigbo electronic governance & administration in nigeria: prospects &challenges Arabian Journal of Business and Management Review (OMAN Chapter) Vol. 5, No.3; October. 2015

Kwa kuongezea pia kuna miradi ya Serikali kwa Mfanyakazi (G2E), ambayo ni midogo na inahusisha huduma maalum kwa wafanyakazi wa serikali, na Serikali kwa Yeyote (G2X) ambayo Serikali hutoa huduma zinazowezeshwa matumizi ya ICT kwa wasio raia kama vile utoaji wa viza, wawekezaji wa kigeni kupata taarifa za uwekezaji wakiwa nje ya nchi.

2.12 Utekelezaji wa shughuli za Serikali Mtandao

Utekelezaji wa shughuli za Serikali mtandao unapaswa kuwa na uangalifu wa hali ya juu ambapo masuala shirikishi katika maeneo ya udhibiti na ulinzi yanashughulikiwa ipasavyo. Madhara ya kutokufanyika umakini katika maeneo hayo kunaweza kuleta athari mbaya katika miamala ya fedha na maeneo mengine yatakayotumia huduma za Serikali mtandao.

SURA YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA SERA NA SHERIA MBALI MBALI

3.1 Utangulizi

Masuala ya Serikali mtandao yametajwa katika Sera na Mipango mbalimbali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiwemo Sera ya Serikali Mtandao ya mwaka 2015, Sera ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010, Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011, Sera ya Mawasiliano ya Habari ya mwaka 2013 na Dira ya 2050, na MKUZA III. Aidha Katiba na Sheria zifuatazo zimezingatiwa:

(a) Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984;

(b) Sheria ya wakala wa Serikali Mtandao Nam. 12 ya mwaka 2019;

(c) Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011;

(d) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2016;

(e) Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 11 ya mwaka 2016;

(f) Sheria ya Wakala wa Miundo Mbinu ya Tehama Nam. 15 ya mwaka 2020;

(g) Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar Nam. 1 ya mwaka 2017;

(h) Sheria ya kuanzisha Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia Nam. 2 ya mwaka 2009;

(i) Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Tanzania Nam. 14 ya mwaka 2015; na

(j) Sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Mawasiliano ya Habari Tanzania Nam.12 ya mwaka 2003.

3.2 Sera na Miongozo

1. Sera ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2015

(a) Utangulizi

Malengo makuu ya Sera ya Serikali Mtandao ni kutoa miongozo juu ya utaratibu wa uanzishwaji na usimamizi wa kisheria wa Serikali mtandao Zanzibar. Sera hii pia imeonesha umuhimu wa kuanzishwa Serikali mtandao kwa faida na maendeleo ya watu wa Zanzibar. Katika kufikia lengo hilo sera imeweka mikakati ikiwemo uanzishwaji wa taasisi ya usimamizi na uratibu wa Serikali mtandao, uimarishaji wa miundo mbinu katika taasisi za umma, upatikanaji wa wataalamu wa ICT katika taasisi za Serikali pamoja na wananchi. Vile vile wananchi kupata taalumu juu ya umuhimu na faida za Serikali mtandao kwa jamii.

Sera pia imependekeza uanzishwaji wa chombo kitakachosimamia utekelezaji wa Serikali mtandao Zanzibar kitakachokuwa na wataalamu wa kutosha wenye uwezo katika usimamizi wa Serikali mtandao na kubainisha kukuza matumizi ya Mtandao katika sekta za umma,[81] kuwa na gharama nafuu na muunganiko kati ya Serikali na taasisi zake,[82] uwazi na uwajibikaji,[83] kukuza na kuendeleza ukuaji wa raslimali watu.[84]

(b) Misingi iliyozingatiwa katika Sera ya Serikali Mtandao

Sera imeelekeza kuandaliwa kwa sheria itakayosimamia Serikali mtandao Zanzibar ambayo itaonesha kazi, majukumu na uwezo wa chombo hicho na

[81] Sera ya serikali mtandao ya mwaka 2015, ukurasa wa 5
[82]Sera ukurasa wa 5-6
[83] Sera ya Utawala Bora ukurasa wa 6
[84]Ibid ukurasa 6-7

kwa taasisi nyengine za Serikali. Aidha sera imeelekeza upatikanaji wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya matumizi katika uendeshaji wa Serikali mtandao. Katika kufikia lengo hilo sera imeelekeza.

(c) Majukumu ya Taasisi za Serikali katika kuendeleza Serikali Mtandao

Sera ya serikali mtandao katika kuhakikisha kwamba Serikali inafikia malengo yaliokusudiwa katika kuwahudumia wananchi imezielekeza wizara mbali mbali na taasisi za Serikali kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba utekelezaji wa mipango ya uwepo wa Serikali mtandao unafanikiwa.[85]

2. Sera ya Utawala Bora ya Mwaka 2011

Sera ya Utawala Bora imeelezea jinsi Serikali inavyofanya kazi zake katika maeneo yake na namna ambavyo inaweka mahusiano na wananchi, asasi za kiraia pamoja na taasisi nyengine, katika utumiaji wa madaraka kwa ufanisi, uaminifu, usawa, uwazi na uwajibikaji katika ngazi tofauti za Serikali.[86]

Sera ya Utawala Bora imepitishwa kwalengo la kuimarisha maendeleo ya kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni nchini. Sera hii imeweka taratibu kwa kuhakikisha kwamba masuala ya utawala bora yanatekelezwa ipasavyo kwa kutilia mkazo misingi mikuu ya utawala bora ambayo ni Uwajibikaji na Uwazi; utawala wa Sheria na Haki za Binadamu, kuzuia rushwa, ufanisi na Tija, ushirikishwaji, kuzingatia Matakwa ya wananchi.

[85]Mwaka 2015
[86]Sera ya Utawala Bora, ukurasa wa 3 ya mwaka 2011

3. Sera ya Mawasiliano ya Habari ya Mwaka 2013

Sera ya Mawasiliano ya habari kwa njia ya mtandao ni kiini cha uanzishwaji wa Serikali mtandao, Sera imeanisha aina mbali mbali za mawasiliano ikiwemo mawasiliano ya teknolojia. Hii itahusisha miundo mbinu, vifaa vya kumputa na vifaa vyengine zinavohitajika kwa ajili ya mawasiliano.

Sera imesisitiza mawasiliano ya kimtandao lazima kupatikane kwa vifaa vya mawasiliano ambavyo vitakuwa vyenye viwango na ubora ambavo vitarahisisha upatikanaji wa mawasiliano nya kimtandao. Mawasiliano ya kimtandao hayawezi kufanikiwa bila ya uwepo wa wataalamu wenye uelewa katika fani ya mawasilino ya kiteknolojia ya kimtandao pamoja na uwepo wa zana madhubuti za mawasiliano kama ambavyo zimeainishwa katika sera ya Serikali mtandao.

4. Sera ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010

Sera ya utumishi wa umma imeanzishwa kwa lengo la kutoa huduma bora kwa Wazanzibari kwa namna yenye tija na ufanisi kwa kiwango cha juu kabisa cha tabia njema na uaminifu. Sera hii inakwenda sambamba na malengo ya Sera ya Serikali mtandao ambayo inakusudia kuleta huduma bora na kwa haraka kwa wananchi, kuzingatia viwango katika utendaji wa kazi, kusisitiza suala la nidhamu na uaminifu.

Pamoja na malengo hayo sera hii inasisitiza utii wa sheria kwa mfano kwa upande wa wananchi wanatakiwa wafuate amri halali zinazotolewa na sheria kwa mfano, kulipa ada mbali mbali, malipo na tozo zinazohitajika katika taasisi za Serikali. Kwa upande wa Serikali kuweza kuwatambua wananchi katika

maeneo yao, kazi zao, uzawa, kustaafu kwao ili iweze kutowa huduma kwa urahisi.

Misingi iliyoainishwa katika sera ni pamoja na kujielekeza katika matokeo mazuri, kuangalia wateja, ushirikishwaji wa wananchi, na thamani ya fedha (value for money).

5. Dira ya Maendeleo ya 2050

Serikali mtandao inakwenda sambamba na malengo ya Dira ambayo inasisitiza juu ya utoaji wa huduma kwa njia ya haraka na kwa ufanisi. Malengo ya kuanzishwa kwa serikali mtandao ni kuhakikisha Dira ya Maendeleo inatekeleza kwa vitendo.

Suala la Serikali Mtandao limeelezwa katika eneo la Utafiti na Ubunifu, ambalo imeeleza katika kufanya utafiti na ubunifu suala la teknolojia ni muhimu katika ukamilishwaji wa shughuli za Serikali.[87] Dira imetaka kuzingatiwa miundombinu ya kisasa, ya hali ya juu, inayofikika na inayotegemewa kwa wananchi, ili kuchochea uchumi wa Zanzibar na mageuzi ya kuimarisha muunganisho wa ndani, kikanda na kimataifa.[88] Aidha Dira imeeleza kwamba huduma za mawasiliano na upatikanaji wa taarifa zitakazowafikia wananchi kwa gharama nafuu zinapaswa kuunganishwa katika maeneo yote ya Zanzibar, kama vile "fiber optic" na miundombinu ya ICT.

[87] Dira 2.2
[88] Pillar 3, Dira 2050

Matumizi bora ya TEHAMA katika huduma za sekta ya uzalishaji ni eneo jengine lililoelezwa katika Dira, ili kuboresha ufanisi katika biashara na kupunguza gharama za manunuzi; na huduma za utangazaji zinazotegemewa, zinazofikiwa na nafuu kupitia upanuzi wa miundombinu ya kidijitali, kwa watazamaji wa ndani na wa kimataifa.

Katika eneo la Utawala bora na Ustawi, Dira imeeleza kwamba mwendelezo wa utulivu wa kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimazingira unapaswa kuendelezwa Zanzibar kupitia utawala unaowajibika, wenye uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika usimamizi wa rasilimali zote za taifa na mifumo ya tathmini.

6. MKUZA III

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) imeonekana kuongezeka kwa kiasi kikubwa matumizi, na mfumo wa kitaasisi upo.[89] Tathmini ya M&E iligundua kuwa nyaraka muhimu katika muundo wa kitaasisi, kwa mujibu wa nyaraka muhimu, miundo na utaratibu wa kubadilishana habari na mifumo ya ICT, iliyopo hautoshi. Zaidi ya hayo, MKUZA umeeleza kwamba uimarishaji wa uwezo wa kitaasisi kiprogramu, pamoja na uhaba wa rasilimaliwatu na vifaa vya ICT vinapaswa kutekelezwa katika ngazi zote ili kubaini udhaifu na kuwa na ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya taifa, kisekta na wilaya.[90]

MKUZA imeeleza umuhimu wa kuwepo miundombinu ya kutosha ikiwa ni pamoja na ICT. Kwa kuzingatia hali ya maendeleo yake, Zanzibar ipo kwenye

[89] Cluster I: Economic Growth and Reduction of Income Poverty, ukurasa wa 4
[90] 1.1.4 Ufuatiliaji na Tathmini ukurasa wa 8

hatua ya uwekezaji, ambayo inamaanisha mahitaji makubwa ya mifumo ya ICT inahitajika.

Huduma za TEHAMA zimeimarishwa kupitia uwekaji wa waya chini ya bahari, hata kama ujenzi wa uwezo unabaki kuwa muhimu ili kuwatia moyo wadau wote kwa kutumia ICT, shuleni na katika biashara. Matumizi ya ICT yatakuwa kupanuliwa katika utumishi wa umma, ikijumuisha mifumo ya malipo ya kielektroniki.[91]

3.3 Sheria

(a) Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984

Katiba ya Zanzibar ndiyo mwongozo mkuu wa sheria zote zinazotungwa na kutumika Zanzibar. Kwa upande wa Serikali mtandao hakuna uhusiano wa moja kwa moja na Serikali mtandao lakini malengo na madhumuni ya kuanzishwa kwa Serikali mtandao yanabainika katika Katiba ya Zanzibar kwenye vifungu mbali mbali vya Katiba hiyo mfano, Uwajibikaji, Uwazi, Utawala bora na faragha. Katiba ya Zanzibar inasisitiza juu ya Serikali iliyopo madarakani kuwajibika kwa wananchi kwa kuwapatia huduma zilizobora, zenye viwango kwa muda na kwa wakati.[92]

Uanzishwaji wa Serikali ya mtandao Zanzibar una lengo la kuifanya Serikali kuwajibikaji kwa wananchi kwa kuwapatia huduma mbali mbali kama vile huduma na taarifa ya njia ya mtandano mfano; kutoa huduma za upatikanaji

[91] A2. Miundombinu Endelevu na inayowezesha Ukuaji Taarifa ya Matokeo
[92]Ibid kifungu cha 8

kwa elimu, afya, huduma za umeme, malipo mbali mbali ya ada na tozo kwa mfano leseni, vyeti vya kuzaliwa na kadhalika. Moja katika msingi muhimu wa uwanzishwaji wa Serikali mtandao ni kuzingatia faragha ya mtu (siri), Katiba ya Zanzibar pia inasisitiza juu ya kulindwa kwa faragha ya mtu.[93]

(b) Sheria ya Wakala wa Serikali Mitandao Nam. 12 ya Mwaka 2019

Sheria hii imetungwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba mifumo ya habari ya mawasiliano inawekwa, inaimarishwa, inaendelezwa kwa mujibu wa sera na viwango vitakavyopelekea kuwa na upatikanaji wa habari, wenye gharama nafuu itakazohusisha shughuli za Serikali.[94]

Sheria hii vilevile itajihusisha na kushajihisha matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma.[95] Sheria itatumika kama kitovu cha utaalamu katika kuandaa na kuendeleza sera, viwango na taratibu nyengine kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utumishi wa umma Zanzibar.[96] Sheria hii imeanzisha Wakala wa Serikali Mtandaokwa ajili ya kuratibu shughuli za Serikali mtandao kwa umma. Vilevile inahusika katika kuimarisha mfumo wa habari za kidijitali. [97]

Vile vile sheria hii itahusika katika kuanzisha na kuendeleza rejista za mfumo wa Serikali mtandao katika utoaji wa huduma. Pia sheria hii ndio itakayothibitisha mifumo ya taarifa inayoendana na mahitaji ya mifumo

[93]Ibid kifungu 15
[94]Nam. 12 ya mwaka 2009
[95]Kifungu cha 5(d) cha Sheria ya Wakala wa Serikali Mitandao namba 12 ya mwaka 2019
[96]Kifungu cha 5 (e)
[97] Ibid kifungu cha 4

mengine na usalama wa taarifa.[98] Katika kuhakikisha malengo ya sheria yanatekelezwa, taasisi imepewa uwezo kisheria ya kuitaka taasisi yoyote kutoa taarifa kinayohitajika katika kazi zake.[99] Taasisi hii vilevile imepewa mamlaka ya kutoa maelekezo kwa taasisi za umma kuhusiana na utekelezaji wa sera za Serikali mtandao.

Wakala imepewa mamlaka chini ya sheria Kuidhinisha uanzishaji na uendeshaji wa huduma na mifumo ya kieletroniki katika utumishi wa umma. Pamoja na uwezo huo pia taasisi imepewa uwezo wakuidhinisha mikakati ya kisekta ya maendeleo ya Serikali ya kieletroniki na kufuatili utekelzeaji wa mipango ya Serikali mtandao.[100]

Kwa ajili ya usimamizi wa kazi zilizoainishwa na sheria hii, wakala imeanzisha Bodi ya ushauri ambayo itakuwa na Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais, na wajumbe wengine watateuliwa na waziri kutoka katika taasisi mbalimbali za Serikali.[101]

(c) Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya Mwaka 2011.

Sheria hii ndiyo iliotoa utaratibu na kuruhusu kisheria juu ya uanzishwaji wa serikali mtandao katika wizara, idara na taasisi Taasisi mbali mbali za Serikali kwa lengo la kuboresha huduma za mawasiliano kwa wananchi.[102] Aidha sheria hii imezitaka Wizara, Idara na taasisi za Serikali kutumia zana za kisasa za kisayansi na teknolojia katika mawasiliano ili kukuza ufanisi katika utendaji wa

[98]Ibid kifungu cha 6
[99]Ibid kifungu cha 7(a)
[100]Ibidi kifungu cha 7(e)
[101]Ibid kifungu cha 8
[102]Nam. 12 ya mwaka 2011

kazi za kila siku.[103] Sheria hii imeruhusu kuanzisha mifumo ya teknolojia ambayo itasaidia urahisi wa upatikanaji wa huduma kwa kupitia mtandao ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa njia rahisi na kwa haraka ili kupelekea mbele maendeleo ya nchi kwa njia ya kidijitali.

Katika utekelezaji wa malengo yaliokusudiwa Sheria hii imewapa mamlaka makatibu wakuu wa Wizara zote za serikali kuhakikisha kitengo kinachohusiana na mambo ya ICT kinaundwa na kinafanyakazi zake ipasavyo na kupatiwa wataalamu wenye sifa na weledi katika kufikia malengo ya Serikali ya kuwasiliana kwa njia ya kimtandao.

(d) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya Mwaka 2016

Sheria hii imeazishwa kwa lengo la kusimamia masuala ya matumizi ya fedha katika wizara zote za Serikali. Kwa ajili ya utekelezaji na ufanisi wa Serikali mtandao Wizara ya fedha chini ya sheria hii italazimika kununua vifaa vyenye viwango ambavyo vitatumika katika mawizara, maidara na vitengo mbalimbali vya Serikali ili kukidhi malengo ya Serikali mtandao na iweze kutekeleza malengo hayo.[104] Suala la uwajibikaji, nidhamu na ufanisi ni miongoni mwa madhumuni ya uanzishwaji wa Serikali mtandao. Sheria hii inagusa moja kwa moja malengo ya kuanzishwa kwa Serikali mtandao Zanzibar. [105]

Sheria hii pia imeeleza wajibu na Mamlaka ya Mhasibu Mkuu wa Serikali katika udhibiti wa fedha na kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa

---

[103] Ibid Kifungu cha 96 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011

[104] Nam. 12 ya mwaka 2016

[105] Vifungu vya 6(a), (b), (c) na (d) vya sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2016

malengo yaliokusudiwa.[106] Sheria hii imeeleza kwa kina juu ya usimamizi wa fedha na kuzitaka taasisi za Serikali kutumia fedha kwa mujibu wa bajeti zilizoainishwa katika wizara husika. Kuanzishwa kwa Serikali mtandao kutasaidia kwa kiwango kikubwa usimamizi wa fedha katika taasisi za Serikali na kupunguza wizi wa fedha za serikali unaoweza kujitokeza kutokana na utaratibu unaofanyika kwa njia za kawaida.[107]

Sheria hii imeeleza kazi na mamlaka ya mkuu wa hazina katika udhibiti wa fedha za Serikali na matumizi. Ili kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali.[108]

(e) Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 11 ya Mwaka 2016.

Sheria hii inasimamia ununuzi na uondoshaji wa mali za umma, ambayo imeanzisha Mamlaka kwa ajili ya kuweka misingi mizuri ya usimamizi wa manunuzi kwa taasisi zote za Serikali kwa bei elekezi inayowekwa na Serikali.[109]

Sheria hii imeweka utaratibu mzuri wa manunuzi ambao utafanywa kwa njia ya uwazi na uwajibikaji na Taasisi za Serikali pindi wanapotaka kuingia katika makubaliano ya kibiashara hasa katika mambo ya ununuzi wa vitu vya ofisi au huduma.[110] Taratibu za manunuzi katika mtandao ni njia pekee inayoweza

[106] kifungu cha 10
[107] kifungu cha 27
[108] vifungu vya 39 (1) (2) (a-f)
[109] Nam. 11 ya mwaka 2016
[110] Kifungu cha 31 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nam. 11 ya mwaka 2016

kusaidia masuala ya uwazi na uwajibikaji katika manunuzi na kuondosha ubaguzi, upendeleo na rushwa katika manunuzi ya vifaa vya Serikali.

(f) Sheria ya Wakala wa Miundo Mbinu ya TEHAMA Nam. 15 ya Mwaka 2020.

Sheria hii imeanzishwa kwa malengo ya kutoa huduma ya TEHAMA yenye nafuu, endelevu usalama na jumuishi yenye kuwezesha kutoa huduma kwa uuma.[111] Vilevile kuimarisha na kuendeleza miundombinu ya TEHAMA na huduma,[112] na kushajihisha na kuimarisha mchango wa miundo mbinu ya TEHAMA kwa maendeleo ya Zanzibar,[113] kufanya tathmini ya kijamii na mazingira kwa ajili ya kuhifadhi na kupata ufumbuzi wa athari zinazoweza kutokea katika miundombinu ya TEHAMA kwa umma.[114]

Kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake, Wakala itakuwa na kazi ya kusimamia na kuendeleza miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano na huduma,[115] na kusimamia na kuendeleza kituo kikuu cha kuhifadhi taarifa Zanzibar.[116] Wakala pia imepewa jukumu la kusimamia na kuendeleza anuani mtandao Zanzibar, kwa ajili ya maendeleo na ulinzi wa wananchi,[117] kutoa miongozo na kuendeleza miundombinu ya TEHAMA Zanzibar.[118]

[111] Kifungu cha 4 (a) cha sheria ya Wakala wa Miundo Mbinu ya TEHAMA Nam. 15 ya mwaka 2020
[112] kifungu cha 4 (b)
[113] kifungu cha 4(c)
[114] kifungu cha 4(d)
[115] kifungu cha 6 (1)(a)
[116] kifungu cha 6(1) (b)
[117] kifungu cha 6(1) (c)
[118] kifungu cha 6 (1) (f)

Katika usimamizi wa kazi za kila siku za wakala imeanzisha Bodi ya ushauri ya Wakala,[119] miongoni mwa kazi zake ni kumshauri Waziri wa Mawasiliano kuhusu usimamizi wa miundo mbinu ya TEHAMA pamoja na huduma[120] kwa kuzingatia malengo yalioainishwa katika Sheria.[121]

Utekelezaji wa malengo yaliowekwa na Sheria hii utasaidia kupeleka mbele harakati za kuanzishwa kwa Serikali mtandao. Kwa kuanzisha, kuweka na kusimamia miundombinu ambayo itasaidia katika mawasiliano ya kimtandao. Miundo mbinu ya kimtandao ambayo inasimamiwa chini ya Sheria hii ndio kichocheo cha kufanikiwa kwa utekelezaji wa Serikali mtandao. Mfano minara, kuwekwa kwa mkonga wa taifa na kujengwa kwa vituo vya kusambazia habari.

(g) Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar Nam. 1 ya Mwaka 2017

Sheria hii imetungwa kwa lengo la kuanzisha Ofisi ya Uchaguzi kwa ajili ya Kusimamia shughuli zote za uchaguzi ambazo zitafanyika katika Zanzibar. Sheria hii imeeleza katika kifungu mbali mbali katika masuala ya uwajibikaji, uwazi, na ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya jamii katika nyanja ya kisiasa na kijamii.[122]

Utaratibu wa uandikishaji wa daftari la kupiga kura kwa njia ya eletroniki ni moja ya katika njia ya kieletroniki zilizotumika katika usajili. Utaratibu huu wa eletroniki umesaidia Serikali kuweza kuwatambua wananchi hasa wapiga kura

---

[119] kifungu cha 7
[120] kifungu cha 8(1) (a)
[121] kifungu cha 8(1)(b)
[122] Nam. 1 ya mwaka 2017

kuweza kujua taarifa zao zinazohusiana na mahala anapoishi, umri, hali ya ndoa, jinsia na kazi.

Kwa kuwa sheria hii inasisitiza suala zima la uwazi, uwajibikaji na ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya watu wa Zanzibar, uanzishwaji wa mawasiliano ya kimtandao kwa njia ya kidijitali utafanikisha zaidi malengo yaliokusudiwa ya kuendesha serikali kwa njia ya mtandao kama ilivoainishwa na Sheria hii.[123]

(h) Sheria ya Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia Nam. 2 ya Mwaka 2009

Sheria hii imeanzisha chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuwasaidia wananchi kuelewa mambo ya sayansi na teknolojioa ili waweze kukuza ufanisi katika utendaji wa taasisi nchini. Taasisi hii ni moja ya taasisi muhimu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi katika suala zima la sayansi na teknolojia.

Pamoja na mambo mengine Sheria hii imeainisha kazi mbali mbali zinazofanywa na chuo hicho kama vile kufanya tafiti za kisayansi, kusomesha masomo ya kisayansi pamoja na kutoa elimu ya kisayansi kwa wanafunzi,[124] kukuza maendeleo ya sayansi na teknoloji katika kiwango cha juu,[125] na kutoa mafunzo katika fani ya teknolojia.[126]

[123] vifungu vya 9(3) na (4) vya Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar Nam. 1 ya mwaka 2017
[124] Kifungu cha 5(a) cha sheria ya Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia Nam. 2 ya mwaka 2009
[125] kifungu cha 5(b)
[126] kifungu cha 5(c)

(i) Sheria ya Makosa ya Kimtandao Nam. 14 ya Mwaka 2015

Sheria ya Makosa ya Kimtandao inahusu makosa yanayohusiana na matumizi ya mfumo wa kompyuta na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Sheria hii pamoja na mambo mengine imeainisha makosa mbali mbali ya matumizi ya kimtandao. Sheria hii inatumika sehemu zote za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.[127] Isipokuwa katika mazingira ambayo mshtakiwa amekiri kosa kwa hiari yake mbele ya Mkurugenzi wa Mashtaka ikiwa kosa hilo limefanyika kwa upande wa Tanzania Bara, kukitokea mazingira kama hayo kifungu hiki hakitotumika Zanzibar.[128]

Makosa hayo yameainishwa katika vifungu mbalimbali vya sheria ikiwemo kukataza mtu yeyote kuingia au kusababisha kuingiliwa kwa mfumo wa kompyuta kwa makusudi,[129] atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana kinyume cha sheria, au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.[130]

Sheria hii imekataza na imetoa adhabu kwa wale wote wataotumia vibaya mfumo wa kompyuta au kuendelea kutumia mfumo wa kompyuta, kinyume cha sheria na kwa makusudi, baada ya kuisha kwa muda ambao aliruhusiwa kutumia mfumo wa kompyut,[131] atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja au mara tatu ya

[127] Kifungu cha 2
[128] kifungu cha 50
[129] Kifungu cha 4 cha sheria ya Makosa ya Kimtandao Nam. 14 ya mwaka 2015
[130] kifungu cha 4(2)
[131] kifungu cha 5

thamani ya faida iliyopatikana au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita au vyote kwa pamoja.[132]

Sheria hii imekataza na imetoa adhabu kwa mtu atakayeingilia mawasiliano kwa njia ya kiufundi kinyume cha sheria, [133] na kuweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni tano au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.[134] Adhabu nyengine ni kwa kosa la kuingilia data kwa kufuta, kuzorotesha, kubadili au kumzuia mtu aliyeidhinishwa kutumia data kinyume cha sheria.[135]

Vile vile sheria hii imekataza na kutoa adhabu kwa mtu yeyote atakaeingilia utendaji kazi wa mfumo wa kompyuta au uendeshaji wa mfumo wa kompyuta, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili au mara tatu ya thamani ya faida iliyopatikana au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.[136]

Sheria imekataza na kutoa adhabu kwa mtu yoyote atakaejihusisha au kumiliki kifaa cha kompyuta ikijumuisha program,[137] kuiingiza, kubadilisha, kuchelewesha, kusambaza au kufuta data katika kompyuta iliyoghushiwa kwa lengo la kutaka itumike bila kujali kama taarifa hiyo inasomeka au haisomeki[138]

[132] kifungu chaa 5 (2)
[133] kifungu cha 6
[134] kifungu cha 6(2)
[135] kifungu cha 7 (1) (a), (b), (c) ,(d), (e) (f) na (g)
[136] kifungu cha 9(a) na (b)
[137] kifungu cha 10(1) (a) na (b)
[138] kifungu cha 11(1)

atakayechapisha taarifa au data katika picha, maandishi, alama au katika namna nyingine yoyote katika mfumo wa kompyuta, akijua kwamba taarifa au data ni za uongo, zinapotosha, zisizo sahihi, na kwa lengo la kudhalilisha, kutishia, kutusi au kwa naamna nyingine kudanganya umma au kuchochea utendaji wa kosa, atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kutumikia kifungo kisichopungua miaka mitatu au vyote kwa pamoja.[139]

(j) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Habari (TCRA) Nam. 12 ya Mwaka 2003

Sheria inaanzisha chombo cha Udhibiti wa Mawasiliano ya simu, matangazo ya radio, huduma za posta na kinachotoa masafa ya urushaji wa matangazo na mawasiliano ya redio, teknolojia za kieletroniki na huduma nyengine za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Sheria pia imeipa chombo hicho pamoja na Bodi ya Wakurugenzi kazi na majukumu ya kusimamia utendaji wa sekta mbali mbali inazozisimamia na zinazohusiana na viwango vya uwekezaji, uwepo wa ubora na viwango katika kutoa huduma,[140] kusimamia viwango na masharti kwa huduma na vifaa, gharama za uendeshaji na ubora katika utoaji wa matangazo na utoaji wa habari, pamoja na kuweka vigezo vitakavyoongoza utoaji wa huduma na bodhaa zinazohusu mawasiliano.[141]

[139] kifungu cha 16
[140] Kifungu cha 5 cha Shera ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Habari Nam. 12 ya mwaka 2003
[141] kifungu cha 6

Baada ya kuangalia kazi na muundo wa sheria hii inaonekana kwamba sheria inalingana kwa kiasi kikubwa na sheria wakala wa Serikali mtandao.[142] Sheria ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano ya Habari imepewa mamlaka ya kuzisimamia sekta nyengine,[143] wakati sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao itakuwa inasimamia taasisi zote za serikali.[144]

Sheria ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano ya Habari inahitaji uwepo wa miundo mbinu ya mawasiliano na kuhakikisha mawasiliano yanafika katika sehemu husika.

[142] Nam.12 ya mwaka 2009
[143] Ibid Kifungu cha 6(a)
[144] Kifungu cha 6 cha Sheria ya Serikali Mtandao Nam.12 ya mwaka 2009

SURA YA NNE

4.0 MAONI YA WADAU

4.1 Utangulizi

Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Nam. 16 ya mwaka 1986 kinaitaka Tume ya Kurekebisha Sheria kushirikisha idadi kubwa ya wadau kadri inavyowezekana wakati wa kufanya mapitio ya sheria ili kupata maoni yao kuhusiana na sheria husika.

Katika kutekeleza masharti ya kifungu hicho cha Sheria, Maoni hayo ya wadau yalikusanywa katika vikao na mikutano mbalimbali vilivyoitishwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar. Aidha Tume ilikusanya maoni kwa wadau wa sheria ya Serikali mtandao ikiwemo taasisi ya Wakala Mtandao, wataalamu kutoka katika Wizara, Idara na Mashirika ya Serikali, taasisi binafsi, Kmapuni mbalimbali, Vyuo Vikuu n.k. Wadau walitoa mapendekezo ambayo yalizingatia maeneo yafuatayo:

4.2 Maoni ya Kisheria

1. **Mazingatio ya Sheria**

Wadau wameeleza kwamba masuala mapya ya kisheria yanahitaji kuzingatiwa katika utekelezaji wa Serikali Mtandao kwani utekelezaji wa Serikali Mtandao mara nyingi huhitaji uundaji na utekelezaji wa sheria na sera mpya, taratibu za uwajibikaji na uwazi kwa kuzingatia utawala bora, viwango vya utendaji, udhibiti na ubora wa taarifa, vyombo vya udhibiti kama vile ulinzi wa mifumo, ukaguzi na uchunguzi.

2. **Kuimarishwa kwa chombo cha usimamizi kisheria**

Wadau wamependekeza kwamba chombo kinachosimamia uendeshaji wa Serikali mtandao Zanzibar kiimarishwe zaidi katika muundo, kazi, uwezo na usimamizi wa taasisi nyengine katika suala la Serikali mtandao. Chombo hicho pia imependekezwa kiwe na wataalamu wenye ujuzi katika mambo ya TEHAMA, vifaa pamoja na usimamizi wa Vitengo vya TEHAMA katika taasisi nyengine za Serikali.

3. **Usalama wa taarifa**

Wadau wameeleza kwamba usalama wa taarifa ujumuishwe katika sheria na ushughulikiwe katika hatua ya ubunifu, ili kuwa na ulinzi wa taarifa za Serikali. Usalama ujumuishe upatikanaji na uhifadhi wa data, ulinzi wa taarifa na uhamishaji wa taarifa kutoka taasisi moja kwenda nyengine. Wadau wamependekeza kuwekwe adhabu kwa mtu atakayeingilia taarifa za mitandao kinyume na taratibu za sheria.

4. **Faragha (Privacy)**

Wadau wameeleza umuhimu wa kuwekwa haki ya faragha kama haki ya msingi kwa jamii yoyote ya kidemokrasia, na ni haki ya kimsingi katika mikataba yote mikuu ya kimataifa na mikataba ya haki za binadamu na katika katiba za nchi nyingi duniani. Imeelezwa kwamba mara nyingi khofu katika faragha kwa Serikali mtandao inajitokeza kwa wananchi iwapo hawajui ni nani ataona taarifa zao za kibinafsi na jinsi zitakavyotumiwa.

Wadau wamependekeza watumishi wanaosimamia huduma za mtandao wawe na ujuzi na udhibiti wa jinsi taarifa za kibinafsi zinavyotolewa, kupitishwa na kutumika na kulinda faragha.

5. **Uwepo wa miongozo**

Wadau wameeleza kwamba ni vyema Sheria ikaweka miongozo maalum kwa taasisi za umma itakayotolewa na Mamlaka kuhusiana na mambo yote yanayohusu matumizi ya elektroniki ikiwemo ununuzi wa mifumo na vifaa vya kielektroniki.

6. **Kutambuliwa kwa nyaraka za kielektroniki**

Wadau wamependekeza Sheria iweke vifungu vya kutambua nyaraka na mikataba iliyofungwa kwa njia za kieletroniki, kwa kufuata masharti yatakayoainishwa na sheria hii ikiwemo, utambuzi wa ombi (offer) iliyopelekwa kwa njia za kieletroniki pamoja na kukubalika kwa ombi kwa njia ya kieletroniki (acceptance of offer). Aidha Sheria iweke vifungu vinavyoainisha kukataliwa kwa ombi kwa njia za kielektroniki (revocation of electronic offer).

7. **Kununua na kuthibitisha vifaa vya TEHAMA**

Wadau wameshauri kuwa majukumu ya kuidhinisha manunuzi ya mifumo/vifaa vikubwa vinavyohusika katika Serikali mtandao ambayo viwe katika ubora unaokubalika na rahisi kwa matumizi ya Zanzibar iwe ni miongoni mwa jukumu la msingi la Taasisi yenye mamlaka ya usimamizi wa Serikali mtandao ili kuepusha ununuzi wa vifaa ambavyo havina tija.

4.3 Maoni ya Kiutendaji

1. Kujumuisha taasisi mbalimbali

Wadau wameeleza kwamba utawala bora kwa ajili ya utekelezaji wa serikali mtandao unawataka wadau wote kutekeleza programu zao kwa namna ambayo uwajibikaji na uwazi hujumuishwa, kwa kuzingatia sheria zote zinazohusika, viwango na utendaji bora, na programu za kutunza kumbukumbu zilizopo katika taasisi mbalimbali.

Wadau wamependekeza kuwe na mashirikiano baina ya taasisi inayokusuduiwa kuanzishwa na taasisi nyengine za serikali kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya taasisi hiyo kwa ufanisi. Pia kuwe na mashirikiano ya karibu baina ya taasisi moja na nyengine katika kutoa, kupekea taarifa mbalimbali za wafanyakazi au jamii.

2. Elimu na kuhamasisha wananchi

Wadau wameeleza kwamba suala la uhamasishaji katika serikali ya kielektroniki lina faida kwa wananchi katika kutumia huduma za serikali mtandao katika maeneo ya vijijini na mijini. Kuna haja ya kuongeza ufahamu wa serikali ya mtandao mapema katika programu na katika hatua ya awali ya utekelezaji wa serikali mtandao. Kwa kuongezea, kipaumbele kinahitajika katika kipindi chote cha utekelezaji wa huduma za kielektroniki ili kutoa elimu ya kutosha na kuwafanya wananchi watumie huduma hizo.

Wadau wamependekeza kutolewa kwa elimu ya kutosha nchi nzima juu ya matumizi ya kieletroniki, elimu hiyo ihusishe matumizi ya vifaa vya teknlolojia, kwa mfano matumizi ya vifaa vyenyewe, namna ya kupata taarifa, umuhimu wa

kuwa na simu za kisasa (smart phone) kwa ajili ya kupakua taarifa mbali mbali zinazotolewa na serikali kwa mfano, kulipa ada za umeme, leseni, benki n.k. Wadau walishauri kuanzishwa kwa vipindi vya redio, television, michezo ya kuigiza nk. na kusambazwa vipeperushi na mabango yatakayoonesha umuhimu wa matumizi ya teknolojia.

3. Uwezo wa watumiaji na wafanyakazi

Wadau wameeleza kwamba wafanyakazi na watumiaji wa huduma za Serikali Mtandao ikijumuisha wananchi na watumishi wa umma wanapaswa kukabiliana na teknolojia mpya.

Wadau wamependekeza uwepo wa wafanyakazi wenye utaalamu wa fani mbali mbali zikiwemo (networking) (programming), (maintenance), (security), (website design), n.k katika taasisi za serikali kwa ajili ya utekelezaji wa serikali mtandao. Aidha walieleza kwamba utaalamu kama wa kusoma na kuandika katika lugha ya kidijitali, mawasiliano ya habari, na usimamizi wa mifumo unasaidia katika ufikiaji wa taarifa za Serikali katika Serikali Mtandao. Imependekezwa utalamu huo ujumuishe kufanya maamuzi (approval), kutatua matatizo, kukusanya na kusambaza taarifa.

Imeelezwa kwa upande wa wananchi, dhana ya Serikali Mtandao inaweza kuwa mpya na baadhi ya watumishi wa umma, Serikali inapaswa kutoa elimu ya kutosha na motisha kwa wadau kusaidia mifumo hii mipya, na ushiriki wa wadau unapaswa kuzingatiwa na kuhimizwa katika kiwango kikubwa.

4. Mafunzo

Imeelezwa na wadau kwamba mafunzo ni eneo muhimu la kuimarisha mafanikio ya jumla ya Serikali Mtandao na kwenda sambamba na mawasiliano na usimamizi wa mabadiliko, pamoja na kukabiliana na teknolojia mpya. Mafunzo yanahusishwa na ustadi au ubunifu, masuala ya kiufundi na usimamizi wa huduma za serikali mtandao katika jamii. Wataalamu hao wapatiwe mafunzo ya mara kwa mara ambayo yatakayoendana na wakati na mabadiliko ya teknolojia. Katika uendeshaji waSerikali mtandao tunahitaji kuwa na wataalamu wa fani mbalimbali zikiwemo (networking) (programming), (maintenance), (security), (website design), n.k.

5. Uwazi

Wadau wamependekeza kuwepo uwazi wa upatikanaji wa taarifa katika mifumo ya TEHAMA. Ukosefu huu wa uwazi huzuia umma kushiriki kikamilifu na kuishauri Serikali katika maeneo ya kuimarisha huduma. Ukosefu wa uwazi unaweza kuficha ufisadi au upendeleo.

6. Kuundwa kwa vitengo vya ICT katika taasisi za serikali.

Wadau wamependekeza kuimarishwa vitengo vya ICT katika taasisi za Serikali ili kuwepo muunganiko wa taarifa na shughuli zinazofanywa katika taasisi za umma na kuhitajika kupatikana katika taasisi ya Wakala Mtandao.

7. Uwekezaji wa vifaa

Wadau wamependekeza taasisi inayosimamia Wakala wa Serikali Mtandao ipatiwe fedha za kutosha ili kuweza kutekeleza malengo ya wakala mtandao ikiwemo kufanywa uwekezaji katika vifaa vya ICT, vifaa vitakavyosaidia

upatikanaji na uunganishaji wa huduma za Serikali mtandao, vifaa vya uhifadhi, mifumo na mafunzo.

8. Kuweka mifumo ya kiteknolojia nchi nzima

Wadau wamependekeza kwa Serikali kuweka na kusimamia mifumo madhubuti ya kitekenolojia (infrustrucure) itakayosaidia upatikanaji wa taarifa katika sehemu mbalimbali za Zanzibar hasa katika maeneo ya vijijini. Aidha wadau walishauri utekelezaji wa Serikali mtandao kuaanza baada ya Serikali kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kuondosha changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa mradi huo. Aidha wadau wamependekeza mifumo itakayowekwa iwe rafiki na isikwaze wananchi katika kuitumia.

9. Vituo vya kusambazia taarifa

Wadau wamependekeza kujengwa kwa vituo vya kusaidia upatikanaji wa taarifa na habari kabla ya kuanza utekelezaji wa Serikali mtandao ili mawasiliano ya kimtandao yaweze kuleta ufanisi na kuwafikia wananchi. Vituo hivyo vitasaidia wananchi ambao hawana simu za kisasa au kompyuta au kupata vikwazo vya upatikanaji wa taarifa.

10. Ulinzi wa mfumo

Wadau wamependekeza kuwe na utaratibu wa ulinzi kwa miundo mbinu itakayowekwa katika kulinda miundombinu ya Serikali mtandao, suala la ulinzi wa mifumo ni la muhimu sana.

SURA YA TANO

5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA NA UZOEFU WA NCHI NYENGINE

5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea Mikataba mbalimbali ya kimataifa, pamoja na uzoefu wa nchi nyengine.

5.2 Mikataba ya Kimataifa

(a) Azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (1948)

Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu si azimio la moja kwa moja kisheria, hata hivyo, baadhi ya vifungu vya Azimio vinazingatiwa kuwa na tabia wa sheria za kimila za kimataifa. Tangu 1948, Azimio la Ulimwengu limepata sana hadhi kwa watu wote na kuna kanuni ambazo Mataifa yote yanapaswa kuzingatia. Azimio inatambua kanuni za kutobagua, haki za kiraia na kisiasa, na kijamii na haki za kiuchumi muhimu kwa utawala bora wa mijini.

Kila mtu ana haki ya uhuru wa maoni na kujieleza; haki hii inajumuisha uhuru wa kushikilia maoni bila kuingiliwa na kutafuta, kupokea na kutoa taarifa na mawazo kupitia yoyote vyombo vya habari na bila kujali mipaka.[145] Kila mtu ana haki ya uhuru wa kukusanyika na kujumuika kwa amani.[146] Kila mtu ana haki ya kushiriki katika serikali ya nchi yake, moja kwa moja au kwa uhuru na Kila mtu ana haki ya kupata huduma ya umma katika nchi yake.[147]

---

[145] Kifungu cha 19
[146] Kifungu cha 20 (1)
[147] Kifungu cha 21

Kila mtu ana wajibu kwa jamii ambayo peke yake maendeleo huru na kamili ya utu wake unawezekana, Katika kutekeleza haki na uhuru wake, kila mtu atakuwa chini yake tu kwa mipaka kama ilivyoamuliwa na sheria kwa madhumuni ya kupata utambuzi unaostahili na heshima kwa haki na uhuru wa wengine na kukidhi mahitaji ya haki ya maadili, umma utaratibu na ustawi wa jumla katika jamii ya kidemokrasia.[148]

(b) Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu

Kuna idadi ya mipango ya kimataifa ili kufaidika kutokana na kutokuwepo kwa mipaka halisi katika mtandao na kukuza ushirikiano wa kimataifa. Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu yaliyopitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UN) mwaka 2015 mambo muhimu yaliyoelezwa ni umuhimu wa ICT.

Umoja wa Mataifa unakuza mipango inayohusishwa na miundombinu kama vile Tume ya Umoja wa Mataifa ya Broadband kwa Maendeleo Endelevu. Shughuli hizi hutoa msaada kwa nchi ili kuziwezesha kupata manufaa ya teknolojia, lakini pia kuna idadi ya mipango ya kimataifa inayonufaika na kile ambacho teknolojia inaruhusu, ikiwemo, EU Digital Market ya Ulaya.[149]

(c) Baraza la Mkataba wa Ulaya wa Ulinzi wa Watu Binafsi kuhusu Uchakataji wa Data ya Kibinafsi na Mkataba wa Uhalifu wa Mtandao

Ufanisi wa kusaidia mifumo ya kimataifa ya teknolojia ya dijiti haiwezi kuwa kipimo kwa viashirio vya kiasi lakini inategemea uchanganuzi wa mtaalam wa Serikali Mtandao. Moja ya kiashiria cha kiasi kilichotumika ni hadhi ya kusaini

[148] Kifungu cha 29 (1) na (2)

[149] the Digital Markets Act (DMA) na the Digital Services Act (DSA)

na kuridhia Baraza la Mkataba wa Ulaya wa Ulinzi wa Watu Binafsi kuhusu Uchakataji wa Data ya Kibinafsi moja kwa moja (automaitc)[150] na Mkataba wa Uhalifu wa Mtandao.[151] Moja ya kiashirio kinachotumika ni kuridhiwa na Baraza la Mkataba wa Ulaya wa Ulinzi wa Watu Binafsi kuhusu uchakataji wa taarifa za Kibinafsi (Data) za moja kwa moja (automatic) na Mkataba wa Uhalifu wa Mtandao.

(d) Serikali za OECD

Serikali za OECD zinafahamu hitaji la muundo kutoa miamala ya kielektroniki inayotekelezeka, katika nyanja ya serikali ya kielektroniki na kwa biashara ya mtandaoni, na wamepiga hatua. Kwa mfano, utambuzi wa kisheria wa sahihi digital ni muhimu ikiwa zitatumika katika serikali ya kielektroniki kwa uwasilishaji wa fomu za kielektroniki iliyo na maelezo nyeti ya kibinafsi au ya kifedha.[152]

Wasiwasi muhimu kwa nchi zinazoendelea itakuwa kutambua masuala ya kisheria. Ni ni rahisi kwao kutoa miongozo ya uhakika nchi zinazoendelea kuhusu ni aina gani ya ulinzi wa kisheria utakaohitajika ili kulinda maslahi ya serikali na kuunda wajibu wa kisheria na unaotekelezeka Serikali. Hata hivyo, nchi zinazoendelea ziko katika hatua au awamu tofauti za Serikali Mtandao, wanatofautiana katika matakwa yao ya kisiasa na katika muundo wao wa Serikali.

---

150 /conventions/treaty/108/signatures?p_auth=eEtCYk9I (2017)
151 https://www.coe.int/en/web/conventions/full-list/-
152 OECD, op cit, note 4. 29 B Krebs 'G8 Nations Mull Digital Divide Task Force Report' (1 June 2001, Washtech.com), online: http://www.newsbytes.com/ . The United Nations has also been concerned. See R Shimmon 'From digital divide to digital opportunity'. Online: http://www.integratedjustice.gov.on.ca/

OECD ilikuwa shirika la kwanza baina ya kiserikali kutoa miongozo kuhusu sera ya kitaifa ya ulinzi wa faragha katika kuchakata data kwa kutumia kompyuta. Mnamo 1980, Miongozo ya Ulinzi wa Faragha na Mtiririko wa Data ya Kibinafsi ilipitishwa kama pendekezo la Baraza la OECD, baadae likafuatiwa na Azimio la mwaka 1985 kuhusu Mtiririko wa Data ya Kuvuka Mipaka, na baadae Tamko la Mawaziri kuhusu Ulinzi wa Faragha kwenye Mitandao ya Kimataifa, lililopitishwa na Mawaziri wa OECD katika mkutano wa Ottawa wa 1998, "Ulimwengu Usio na Mipaka" Kutambua Uwezo wa Biashara ya Kielektroniki ya Ulimwenguni.

Katika mkutano huo, Mawaziri wa OECD walithibitisha tena kujitolea kwao kulinda faragha kwenye mitandao ya kimataifa ili kuhakikisha heshima ya haki muhimu, kujenga imani katika mitandao ya kimataifa, na kuzuia vikwazo vya mishahara visivyo vya lazima kwa mtiririko wa data ya kibinafsi ya kuvuka mipaka.[153]

5.3 Mikataba ya Barani Afrika

(a) Utangulizi

Maendeleo katika nchi za Afrika na pia katika mashirika ya kikanda yanaonesha kuongezeka ufahamu wa jukumu muhimu la teknolojia ya dijitali kwa maendeleo ya nchi na hatari (risk) na changamoto pamoja na fursa zinazoletwa na utandawazi huu. AU kwa mfano imeunda Kamati Maalum ya Kitaalamu ya

[153] E-Government and Developing Countries: An Overview SUBHAJIT BASU, INTERNATIONAL REVIEW OF LAW COMPUTERS & TECHNOLOGY, VOLUME 18, NO. 1, PAGES 109–132, MARCH 2004,, Carfax Publishing, Taylor & Francis Group ukurasaurasa 124

Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, ambayo ilifanya mkutano wake wa kwanza mwezi Septemba 2016.[154]

Mifumo ya kimataifa kwa Afrika ipo pia kwa upande wa wafadhili, Sychelles kwa mfano ina Mfumo wa Cable za chini kwa chini ambao EU imechangia kwa kiasi kikubwa ni mradi wenye athari kubwa. Mipango mengine inayoungwa mkono na EU ni pamoja na Uboreshaji wa Telemedicine Satalaiti na afya mtandao (e-Health) kwa Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara na Soko la Mfumo wa Mtandao la Afrika, unaofadhiliwa kupitia Mfuko wa Udhamini wa Miundombinu wa EU-Africa. EU imeunga mkono na kuoanisha Sera za ICT Kusini mwa Jangwa la Sahara na Mediterania ya Kusini pamoja na miradi ya miundombinu kwa taasisi za utafiti na elimu.[155]

Katika Afrika Mashariki na mataifa ya karibu, nchi nne kwa sasa zina mikakati ya Serikali kwa ajili ya utawala wa kielektroniki ikiwemo Mauritius, Kenya, Rwanda na Zimbabwe. Kenya ina Mpango Mkuu wa Kitaifa wa ICT 2014-2017,[156] Mpango Kabambe wa Rwanda wa SMART Rwanda 2015- 2020,[157] Mkakati wa Kielektroniki wa Serikali ya Mauritius 2013- 2017,[158] na Sera ya Kitaifa ya Zimbabwe kwa ICT.[159]

---

[154] The Convention for the Protection of Individuals with regard to Automatic Processing of Personal Data, 1981 ETS 108, http://www.coe.int/en/web/conventions/full-list/- /conventions/treaty/108/signatures

[155] Commission Staff Working Document SDW (2017) 157 p 8-9. 55 http://reports.weforum.org/global-information-technology-report-2016/P

[156] http://www.ict.go.ke/wp-content/uploads/2016/04/The-National-ICT-Masterplan.pdf (2014)

[157] http://www.myict.gov.rw/fileadmin/Documents/Strategy/SMART_Rwanda_Master_Plan_v2.5.pdf (2015)

[158] http://mtci.govmu.org/English/Documents/eGovStrategyfinalv201393.pdf (2017)

[159] Zimbabwe National Policy for Information and Communications Technology (ICT) (2016)

(b) Mkataba wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa taarifa (Data)

Mwezi Juni 2014, AU ilipitisha Mkataba wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa taarifa (Data) Kibinafsi.[160] Mkataba unalenga kuanzisha mifumo ya kisheria ya kikanda na kitaifa kwa ajili ya usalama wa mtandao, miamala ya kielektroniki na ulinzi wa data binafsi.[161] Hata hivyo, Mkataba, kufikia Juni 2017, umepokea uidhinishaji mmoja pekee (Senegal mnamo Agosti 2016) na kutiwa saini na mataifa mengi.[162]

Umoja wa Afrika umepitisha mikakati katika sekta mbalimbali ili kufikia ushirikiano wa bara hilo ndani ya utaratibu wa kiuchumi wa kimataifa. Katika sekta ya ICT, Bunge la Muungano wa Wakuu wa Nchi na Serikali[163] lilipitisha Mkataba wa Usalama Mtandaoni na Ulinzi wa Data ya Kibinafsi, Hati hii inatoa mfumo wa usalama wa mtandao barani Afrika.

(c)AGENDA 2063

Matarajio ya 3 katika Ajenda 2063 ni Afrika yenye utawala bora ambayo inahitaji ushirikishwaji mkubwa wa watu kupitia Serikali Mtandao, haki za binadamu, haki na utawala wa sheria. Jukwaa la kila mwaka la wadau kukagua maendeleo ya utekelezaji wa Ajenda 2063 kitaifa, ngazi za kikanda na bara. Lengo la 16 la Malengo ya Maendeleo Endelevu limejikita katika kukuza jamii zenye amani na umoja kwa maendeleo endelevu, utoaji wa upatikanaji wa haki kwa wote, na kujenga taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika katika ngazi zote.

---

[160] https://au.int/en/treaties/african-union-convention-cyber-security-and-personal-dataprotection (2017)
[161] UNCTAD p. 35 (2016)
[162] Benin, Chad, Congo, Ghana, Guinea-Bissau, Mauritania, Sierra-Leone, Sao Tome & Principe, Zambia https://au.int/sites/default/files/treaties/29560-slafrican_union_convention_on_cyber_security_and_personal_data_protection.pdf (2017)
[163] http://www.au.int/en/decisions/assembly

5.4 Mikataba ya Kikanda

(a) Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) imeanzisha Mfumo wa EAC wa Sheria za Mtandao, uliopitishwa mwaka 2010, ambao unapendekeza kila mwanachama kutengeneza mfumo wa udhibiti wa ulinzi wa data, lakini hautoi mapendekezo mahususi kuhusu maudhui ya sheria.[164] Jumuiya ya Afrika Mashariki pia inafanyia kazi kuanzisha mfumo wa kisheria kuhusu sheria za mtandao ambao utatoa miongozo juu ya kutunga na kutekeleza sheria zinazokuza uwekezaji wa Serikali Mtandao na huduma za biashara ya mtandaoni.[165]

EAC ina miradi kadhaa inayoendelea kuhusu utawala wa kielektroniki, ikijumuisha Mtandao wa Miundombinu ya ICT wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya "Broadband", mradi unaolenga kuanzisha na kuendesha mtandao wa miundombinu ya mipakani ndani ya EAC.[166]

(b) ECOWAS

(i) Mkataba wa Kuanzisha ECOWAS wa 1975, uliorekebishwa tarehe 24 Julai 1993.

Mkataba wa ECOWAS unatoa miongozo na malengo ya kukuza na kuendeleza mazingira ya biashara. Nchi Wanachama zinaweza kutumia miongozo na malengo si tu wakati wa kutafuta muunganiko kuhusiana na sheria na kanuni, lakini pia katika kuoanisha sera na mikakati ya ICT.

---

[164] UNCTAD (2016) p 35
[165] https://www.eac.int/infrastructure/communications-sector/ongoing-projects
[166] https://www.eac.int/infrastructure/communications-sector/ongoing-projects

ECOWAS imepitisha sheria juu ya ulinzi wa data ambayo ni makubaliano ya kikanda yenye nguvu. Mkataba unabainisha maudhui yanayohitajika ya sheria za ulinzi wa data na inahitaji nchi wanachama kuanzisha mamlaka ya ulinzi wa data. Nchi saba zimetunga sheria katika kufuata makubaliano.[167]

(ii) Shirikisho la Ecowas na Utangamano wa Kanda Katika Eneo la Cyberlaws

ECOWAS, ni wanachama wa Umoja wa Afrika na nchi Wanachama wa Francophone pia ni wanachama wa Shirika la Kuoanisha Sheria za Biashara barani Afrika (OHADA) na Umoja wa Kiuchumi na Fedha wa Afrika Magharibi (WAEMU), isipokuwa Guinea ambayo haitumii sarafu moja.[168] Mashirika haya yote yanafanya kazi kikamilifu katika mfumo wa maendeleo ya biashara ya kielektroniki katika bara la Afrika.

ECOWAS imepitisha sheria juu ya ulinzi wa data ambayo ni makubaliano ya kikanda yenye nguvu. Inabainisha maudhui yanayohitajika ya sheria za ulinzi wa data na inahitaji nchi wanachama kuanzisha mamlaka ya ulinzi wa data. Nchi saba zimetunga sheria katika kufuata makubaliano.

(c) COMESA

(i) Sheria ya Kielelezo kuhusu Miamala ya Kielektroniki na Mwongozo wa Utungaji

COMESA imetengeneza Sheria ya Kielelezo kuhusu Miamala ya Kielektroniki na Mwongozo wa Utungaji mwaka 2010, ambayo ni ripoti kuhusu mpango wa nchi

[167] Supplementary Act A/SA.1/01/10 (2010)
[168] http://www.ohada.com/content/newsletters/1403/Comprendre-l-Ohada-en.pdf

wanachama kuhusu sheria, ili kusaidia nchi wanachama katika kuanzisha sheria zinazofaa kusaidia biashara ya mtandaoni. Utafiti uliofanyika, na kufuatiwa na warsha mbili za utungaji wa sheria kwa njia za kielektroniki (e-Legislation) kwa ujumla na biashara mtandao (e-commerce). Ripoti inajadili masuala yanayohusu ulinzi wa watumiaji, na mambo mengine mengi.[169]

COMESA inafanya kazi ili kukuza matumizi na ufahamu wa ICT kwa lengo la kuchangia katika ushirikiano wa kijamii na kiuchumi, na wametengeneza mfumo wa kikanda kuhusu e-governance, pamoja na portal ya kuoanisha juhudi za Serikali Mtandao katika mikoa na kusaidia Nchi Wanachama katika kutekeleza Serikali Mtandao. Mshirika muhimu kwa COMESA katika utekelezaji wa mpango wa utawala wa kielektroniki ni Umoja wa Mtandao wa Utawala wa Umma wa Mataifa (UNPAN).[170]

(ii) Mradi unaoendelea ni Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS)

Mradi huu una kadi ya Utambulisho wa Biometrik, ambayo itakuwa na chip zinazoweza kubeba vitambulisho vya kidijitali na uwezekano wa kuruhusu utumizi wa sahihi za kidijitali. Katika kikao cha 46 cha ECOWAS kilichofanyika Desemba 2015, Wakuu wa Nchi 15 na Serikali wanachama wa shirika waliidhinisha kuanzishwa kwa mwingiliano wa kitambulisho cha kibayometriki chenye maono ya kuondoa katika siku zijazo hitaji la raia wa ECOWAS katika maeneo mengine ya ECOWAS kuwa na vibali vya kuishi.[171]

---

[169] Information Science Reference, IGI Global) pp. 93-105 at p. 100.
[170] 84 http://www.comesa.int/what-we-do/#information-networking
[171] http://www.ecowas.int/wp-content/uploads/2015/02/46th-ECOWAS-Summit-Abuja-15-Dec 2014 1.pdf (2014)

Kulingana na makubaliano, mfumo wa vipengele vya lazima, vya hiari na vya ziada, vinataka kadi zote kujumuisha "chip" isiyoweza kugusa na maelezo ya kibayometriki yanayojumuisha angalau alama mbili za vidole. Wajibu wa kutoa kadi za Utambulisho wa "Biometric" wa ECOWAS ni kwa kila nchi mwanachama, na Senegal na Benin ndizo nchi ambazo zilijitolea kuanza utoaji huo.[172]

5.5 Uzoefu wa nchi nyengine

Katika kufanya utafiti huu tumeona pia tuangalie uzowefu kutoka katika nchi mbalimbali kuhusiana na masuala ya Serikali Mtandao ili tuweze kujifunza na kupata uzowefu kupitia nchi hizo.Nchi zenyewe ni kama vile:

1. Mauritius;
2. Malaysia;
3. Estonian;
4. Lithuania;
5. Israel;
6. Samoa;
7. Vanuatu;
8. Tonga;
9. Fiji;
10. Kenya; na
11. Tanzania Bara.

[172] http://www.pulse.ng/news/local/ecowas-biometric-ids-senegal-benin-begin-issuance-of-cardsid4651170.html (2016)

5.5.1 Sheria za nchi mbalimbali

1. **MAURITIUS**

(a) Sheria za Kusimamia Wakala Mtandao

Mauritius katika Wakala Mtandao imeweka sheria mbalimbali za usimamizi wa teknolojia ya mawasiliano ikiwemo Sheria ya Habari na Mawasiliano[173] na Sheria ya Huduma za Kielekroniki yam waka 2000.[174]

Aidha Sheria ya huduma za Kielektroniki imeweka wazi mipaka na maeneo ya huduma katika sheria ikiwemo kutambuliwa Nyaraka na Huduma za kielektroniki,[175] uwekaji na usimamizi wa nyaraka za kielektroniki,[176] na saini za kielektroniki.[177]

Aidha, watoa huduma za kielektroniki wamepewa jukumu maalum katika kifungu cha 8 ikiwemo utunzaji na uwekaji taarifa za umma na wananchi na uhifadhi. Suala la mikataba ya kielektroniki limeelezwa katika kifungu cha 10, pamoja na kupokelewa taarifa na kutambuliwa kuwa zimemfika muhusika.[178]

(b) Sera na Mipango kuhusu matumizi ya Wakala Mtandao

Uhifadhi wa taarifa za kielektroniki umeelezwa katika kifungu cha 15, pamoja na utaratibu wa uwekaji saini,[179] na Uhifadhi wa faragha (privacy key) umebainishwa na kuwekewa utaratibu katika kifungu cha 35. Aidha taasisi za

[173] Information and Communication Nam. 44 ya mwaka 2001
[174] The Electronic Transaction Act Nam. 23 ya mwaka 2000
[175] kifungu cha 5
[176] kifungu cha 7
[177] kifungu cha 8
[178] kifungu cha 12
[179] PART VI kifungu cha 18-21

umma zimelazimishwa kuwa na matumizi ya taarifa za kielektroniki[180] na uwekaji wa siri za taarifa umeelezwa katika kifungu cha 41 pamoja na uwezo wa kupata taarifa (access) katika kompyuta.[181]

Wananchi na wafanyabiashara katika Nchi ya Mauritius katika miaka ishirini iliyopita[182] walikuwa wanatumia njia ya kawaida (paper based system) kwa kufanya miamala na kupata huduma mbali mbali za Serikali. Teknolojia za kimtandao kwa wakati huo zilikuwa hazijaanza kutumika.[183]

Hata hivyo Serikali ya Mauritius ilirekebisha tena ajenda ya Serikali Mtandao katika miaka ya 2013 mpaka 2017 kwa kuangalia upya vikwazo vinavyorejesha nyuma maendeleo ya Serikali mtandao na kuandaa mikakati ambayo itapelekea kufanikiwa kwa malengo ya kuanzishwa kwa Serikali mtandao. Serikali ya Mauritius imesisitiza katika kufanyakazi kwa uwazi, ushirikishwaji wa watu na huduma za Serikali zenye kukubalika. Serikali pia ilisisitiza katika kuwapatia wananchi taarifa kwa njia ya mtandao.

Sera na miradi katika maeneo yafuatayo yameimarishwa: upatikanaji wa taarifa, maeneo ya wazi ya vyanzo vya taarifa, ushirikishwaji wa kimtandao, uwezeshwaji wa Malipo ya kimtandao, taaluma za kuweka sahihi za kidijitali, usimamizi wa Hati, manunuzi ya kimtandao, na programu ya simu za mikononi.

---

[180] kifungu cha 40

[181] katika kifungu cha 45.

[182]Central information Beurau Ministry of technology, communication and innovation, digital government transfommation starategy, 2018-2022 ukurasa 8

[183]Ministry of tecnkonology, communication and innovation, central informatics Bereau, Digital Government Trasformation strategy page 8, 2018-2022.

Pamoja na mikakati iliyoanzishwa, Serikali ilibuni mikakati mipya ambayo itatumika ili kuweza kufikia lengo la serikali katika kutekeleza Dira ya Serikali ya 2030 na kwenda sambamba na Mkakati wa Mabadiliko ya Biashara katika Sekta ya Umma (PSBTS) kwa kutumia fursa za mabadiliko ya kidijitali katika Sekta ya Umma. Mikakati hiyo ni kama ifuatayo:

i. Huduma za Dijitali (Digital-by-Default Services)

Huu ni mkakati wa kutoa huduma ya mawasiliano kwa njia ya dharura. Njia hii ilitumika kuwasaidia watumiaji wenye ujuzi mdogo katika masuala ya kidijitali kwa kuwapatia msaada wa matumizi katika vituo maalumu.[184] Kanuni ya usajili wa taarifa binafsi Serikalini (Once-Only Principle), ni utaratibu ambapo wananchi wanapeleka taarifa zao Serikalini pamoja na wadau wengine na Serikali kuzitumia tena data hizo kwa matumizi mengine kwa mfano nakala ya vitambulisho, uthibitisho wa anwani ya sehemu unapoishi, cheti cha kuzaliwa/ndoa/kifo) ikiwa tayari inapatikana Serikalini.

ii. Huduma za moja kwa moja (End-to-end Services)

Mabadiliko ya mfumo wa kawaida (paper based sytem) kwenda kwenye mfumo wa kidijitali ambao mtu binafsi haruhusiwi kufika katika taasisi kwa ajili ya kupatahuduma, kutokana na taarifa zake alizozitoa huduma hizo zitamfuata popote alipo. Mawasiliano yatapatikana kupitia ushirikiano wa wakala mbalimbali wanaoshughulikia na mambo ya mtandao pamoja na mifumo ya kidijitali.

[184] ukurasa wa 3

iii. Ushirikiano katika kutoa huduma (Co-creation of Services)

Utaratibu huu utatumika pale ambapo kutakuwa na ushirikiano baina ya wananchi na wadau wengine katika kutoa huduma kwa urahisi kwa jamii. Ili mfumo wa mawasiliano ya kimtandao uweze kufanikiwa kunahitajika juhudi za pamoja na wananchi, wadau na sekta za Serikali. Mfano Serikali inapaswa kuhakikisha uwepo wa miundombinu ya mawasiliano kwa ajili ya upatikanaji wa habari.

Aidha taasisi za Serikali zinapaswa kuhakikisha zinaweka miundombinu ya mawasiliano kwa ajili ya upatikanaji wa habari, na kuhakikisha wadau wengine wa mawasiliano wanashirikishwa kuhakikisha mfumo wa mawasiliano unakuwa sawa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi.

iv. Utoaji wa taarifa zinazohusu maslahi ya watu (Open Data-by-Default)

Kuanzishwa kwa utaratibu utakaohakikisha kwamba kunakuwa na utoaji wa kawaida wa taarifa zinazohusu maslahi ya watu kwa uwazi na bila ya kutaja jina la mtu. Taarifa hizo zitatolewa na Wizara/Idara kwenda kwa umma kwa ajili ya kuwapa uwezo wa kutumia vifaa vya kidijitali.

v. Utamaduni utoaji wa data (Data Driven Culture)

Kuunganisha matumizi ya data kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi katika utungaji wa sera, ufuatiliaji na kuboresha utoaji wa huduma. Vile vile Serikali inaweza kupima mafanikio na manufaa ya huduma za Serikali kwa kutumia viashirio muhimu vya utendaji kazi na uchapishaji wa takwimu za matumizi ya utumishi wa umma.

vi. **Biashara ya kieletroniki (E-Business Strategies)**

Utaratibu ambao umewekwa kwa kila wizara, idara ambao inatakiwa kukamilisha mipango katika kukamilisha mchakato ya ukamilishaji wa Serikali mtandao kwa mfano kuundwa kwa vitengo, ununuaji wa vifaa, utoaji wa taaluma.

vii. **Ushirikishwaji wa kieletroniki (E-Participation)**

Utaratibu huu utasaidia kuwashirikisha wananchi na wadau wengine kuweza kutoa maoni yao na wadau wengine katika suala zima la ushirikishwaji kufanya maamuzi juu ya vikwazo vinavoikabili utekelezaji wa Serikali mtandao.

viii. **Ununuzi wa kieletroniki (E-Procurement-by-default)**

Serikali ilianzisha utaratibu wa manunuzi kama njia ya majaribio kuelekea manunuzi ya kieletroniki. Utaratibu huu ilikwenda sambamba na utoaji wa elimu kuhusu manunuzi kwa nji ya kidijitali kwa wafanyakazi wa taasisi za Serikali na wasambazaji.

ix. **Ujuzi wa Dijitali (Digital Skills)**

Serikali itafanya mapitio ya propgramm ya mpango wa kitaifa wa utoaji wa taaluma kwa wazawa na wageni ili waweze kutoa huduma za kidijitali kwa ufanisi. Watumishi wa umma wataweza kupata ujuzi wa kidijitali hivyo kuwawezesha kutoa huduma kwa mujibu wa mahitaji ya wananchi.

x. **Utawala kwa kieletroniki(E-Governance)**

Utaratibu ulioanzishwa kuwapatia elimu viongozi wa serikali kuhusu masuala yanayohusu utawala wa kieletroniki, uendeshaji, na namna unavoweza

kufanyika kwa njia za kieletroniki. Utaratibu huu utaisaidia Serikali kuandaa miradi mbali mbali na kubainisha mbinu za kuweza kutekeleza miradi hiyo kwa njia za kieletoniki.

xi. Ushirikishwaji wa Dijitali(Digital Inclusiveness)

Huu ni utaratibu wa utoaji wa huduma za kidijitali mbazo zinahusisha watu wa kawaida na watu wenye mahitaji maalum. Katika utaratibu huu Serikali itatoa utaratibu rahisi wa kimtandao ili watu wenye uwezo tofauti waweze kutumia. Kwa mfano matumizi ya kimtandao kwa watu wasioona, wasiosikia na wengine wenye mahitaji maalum. Kufanikiwa kwa utafiti huo kutawawezesha watu wa aina mbalimbali kuweza kumudu matumizi ya kimtandao na hivyo kuifanya nchi kuwahusisha wananchi wote katika matumizi ya kidijitali.

2. MALAYSIA

(a) Utambuzi wa kisheria wa masuala ya wakala mtandao

Malaysia ina sheria ya Electronic Government Activities Nam. 680 ya mwaka 2007 ambayo inasimamia masuala ya wakala mtandao na kutambua ujumbe mfupi wa maelezo ambao utatolewa kwa njia ya kieletoniki na unatambulika kisheria kama kielelezo mbele ya mamlaka za kisheria, kama vile mahkama.[185] Aidha sheria inakataza kutoitambua taarifa iliyotolewa kwa njia ya ujumbe mfupi kwa msingi kwamba taarifa hiyo haijatolewa katika njia ya kieletroniki.[186] Kwa ufupi sheria ya Malaysia inaikubali na kuipa nguvu ya

[185] Kifungu cha 10(1) cha sheria ya ELECTRONIC GOVERNMENT ACTIVITIES ACT no. 680 of 2007
[186] kifungu cha 10(2)

kisheria taarifa inayotolewa kwa njia ya kieletroniki na ile inayotolewa kwa njia ya kawaida.

(b) Mikataba Kwa njia ya kieletroniki

Sheria ya Malaysia ya eletroniki inakubali mikataba, mawasiliano ya ombi la mkataba (proposals) kukubalika kwa ombi la mkataba (acceptance) na kukataliwa kwa ombi la makubaliano (revocation of contract) na vilevile inatambua mawasiliano yoyote inayofanywa kwa njia ya kieletroniki.[187] Vile vile sheria hii inakataza kutoitambua kisheria taarifa iliyotolewa kwa njia ya kieletroniki.[188]

(c) Kukamilisha mahitaji ya kisheria kwa njia za kielektroniki

Katika sheria ya Malaysia inatambua majibu yatakayotolewa kwa njia ya kieletroniki na mdai ikiwa madai hayo yatatolewa kwa njia ya kieletroniki na yanaweza kutumika kama kielelezo katika ushahidi wa kimahkama.

(d) Saini (signature)

Sheria ya Malaysia ya kieletroniki inatambua kukubalika kwa saini ya kieletroniki ikiwa saini hiyo imeambatanishwa au inahusishwa na ujumbe wa kieletroniki uliotolewa[189] au inamtambulisha mtu ipasavyo na inaonyesha idhini ya mtu huyo kwamba taarifa inahusiana nae[190] na itazingatia madhumuni na mazingira ya saini hiyo.[191]

---

[187] kifungu cha 11 (1)
[188] kifungu cha 11(2)
[189] kifungu cha 13 (1) (a)
[190] kifungu cha 13 (1) (b)
[191] kifungu cha 13 (1) (c)

(e) Kukubalika kwa muhuri (seal)

Sheria ya kieletroniki ya Malaysia inatambua uwepo wa muhuri wa kieletroniki pale ambapo matakwa ya kisheria yanahitaji hivyo.[192] Sheria pia inampa mamlaka waziri kumtaka muhusika kutoa muhuri kwa njia ya kieletroniki.[193] Kwa msingi huo nyaraka yoyote itakayowekewa muhuri wa kieletroniki, itakuwa ni nyaraka halali na inaweza kutumika mahali popote.

(f) Asili (original)

Sheria ya kieletroniki ya Malasyia inatambua uwepo wa hati halisi[194] (original document) iliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki kwa mujibu ya makubaliano ya mkataba uliofikiwa baina ya pande mbili au zaidi za mkataba huo.

(g) Nakala halisi iliyothibitishwa (Certified true copy)

Sheria ya kieletroniki ya Malasyia inatambua uwepo Nakala halisi iliyothibitishwa (Certified true copy) ikiwa hati hiyo itawasilishwa kwa njia ya ujumbe wa kielektroniki na kutimiza matakwa ya kisheria.[195]

3. TANZANIA BARA

(a) Miundombinu ya Serikali Mtandao

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetunga sheria ya Serikali Mtandao.[196] Sheria hiyo inatumika katika Taasisi zote za Serikali. Pamoja na mambo mengine sheria hiyo imesisitiza uimarishaji wa miundo mbinu kwa

[192] kifungu cha 14 (1)
[193] kifungu cha 14(2)
[194] kifungu cha 16
[195] kifungu cha 17
[196] Nam. 10 ya mwaka 2019

taasisi za Serikali na Miundombinu hiyo lazima ithibitishwe na mamlaka husika kwa ajili ya mwasiliano.[197]

Sheria pia imesisitiza katika kuimarisha serikali mtandao katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama vile barabara, majengo na miundombinu mengine ili kuhakikisha mawasiliano ya kiteknolojia kwa njia ya mtandao yanafanikiwa kwa gharama nafuu.[198]

Katika kufikia malengo hayo sheria imetilia mkazo mambo yafuatayo:

1. Uimarishaji wa miradi ya miundombinu ya TEHAMA ambayo itazingatia, masharti, viwango na miongozo itakayotolewa na Mamlaka.[199]
2. Mamlaka ndio itahusika na uthibitisho wa vifaa mbavyo vitatumika katika taasisi za serikali katika uendeshaji wa serikali mtandao.[200]
3. Mamlaka itahakikisha inasimamia uwekaji na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA vitakavotumika katika taasisi za serikali.[201]

Katika kuhakikisha uwekaji na ufungaji wa vifaa vya miundombinu ya mawasiliano ya kimtandao katika taasisi za serikali sheria imesisitiza ufanyike bila ya gharama yoyote.[202]

---

[197] Kifungu cha 23 cha sheria ya Serikali Mtandao namba 10 ya mwaka 2019
[198] kifungu cha 23(2)
[199] kifungu cha 23(2) (a)
[200] kifungu cha 23 (2) (b)
[201] kifungu cha 23(2) (c)
[202] kifungu cha 23 (3)

(b) Miradi ya TEHAMA

Sheria pia imesisitiza Taasisi za Serikali kuanzisha miradi ya TEHAMA ambayo inakidhi viwango na miongozo inayotolewa na Mamlaka ambayo itakayosaidia uendelezaji na uimarishaji wa miundombinu ya serikali mtandao ili kuhakikisha kwamba miradi ya serikali mtandao inakuwa endelevu.[203]

Sheria imezitaka taasisi za serikali ambazo zinakusudia kuendeleza miradi ya TEHAMA kwa ajili mawasiliano kupata ushauri na uthibitisha kutoka kwa mamlaka[204] juu ya hatua za mipango ya utekelezaji wa miradi hiyo,[205] kupata ruhusa kutoka kwa mamlaka kabla ya kutumika kwa fedha kwa ajili ya miradi hiyo.[206] Katika kuhakiksha kwamba miradi ya TEHAMA inafanikiwa katika Taasisi za Serikali. Sheria izmezitaka Taasisi hizo kuunda timu ya wataalamu ambao watasimamia hatua zote za mradi unaokusudiwa kuanzishwa.[207]

Sheria imezitaka taasisi za kuhifadhi nyaraka zote muhimu zinazohusiana na miradi inayohusu Serikali mtandao kuwasilisha ripoti ya mradi ya mawasiliano ya kimtandao kwa Mamlaka kwa mujibu wa muongozo utakaotolewea na mamlaka kwa Taasisi hizo.[208]

(c)Mifumo ya Merikali Mtandao

Sheria imezitaka Taasisi za Serikali kuazisha mifumo ya TEHAMA ambayo itakuwa endelevu (sustainability), zinazofaa (reliability), zenyekuendelezeka

---

[203] kifungu cha 24(1)
[204] kifungu cha 24(2)
[205] kifungu cha 24(2) (a)
[206] kifungu cha 24(2) (b)
[207] kifungu cha 24(2) (b)
[208] kifungu cha 24(2) (d)

(continuity) and zenye kupatikana katika matumizi kwa mujibu wa teknolojia iliopo (availability).[209]

Taasisi za Serikali katika uanzishwaji wa mifumo mipya ya kimtandao katika taasisi zao zimetakiwa kutayarisha mahitaji pamoja na nyaraka ambazo zitafuata viwango na miongozo iliyotolewa na Serikali na kuwasilishwa kwa Mamlaka.[210] Katika uanzishaji wa mifumo mipya ya mawasiliano ya kimtandao taasisi za Serikali zitalazimika kupata ushauri wa wadau wengine wa Serikali mtandao ili kutibitisha ubora na kuhakikisha kwamba hakuna fedha zitakazotumika kwa ununuzi wa vifaa bila ya matumizi.[211]

Sheria imesisitiza mifumo ya kizamani ya kimtandao ambayo bado itakuwa inafanyakazi ipasavyo iweze kuendelezwa baadala ya kutegemea mifumo mipya ambayo utekelezaji wake unaweza kuharibu mfumo mzima wa mawasiliano.[212] Taasisi za Serikali zitalazimika kuunda jopo la wataalamu ambalo litasimamia katika uendelezaji wa mifumo mipya itakayoanzishwa katika taasisi hizo.[213] Taasisi hizo zitalazimika kuwasilisha ripoti ya mifumo mipya ya kimawasiliano kwa Mamlaka.[214]

Sheria imesisitiza katika mazingira ya kuendeleza mifumo iliopo imezitaka Taasisi kuzingatia mifumo iliopo taasisi zimetakiwa kufanya tathmini mfumo na kutoa ripoti ya tathmini kabla ya kupelekwa katika mazingira ya

[209] kifungu cha 25
[210] kifungu cha 25(a) (i)
[211] kifungu cha 25 (a) (ii)
[212] kifungu cha 25 (a) (iii)
[213] kifungu cha 25 (a) (iv)
[214] kifungu cha 25 (a) (v)

matumizi,[215] kuandaa mfumo kwa mazingira yaliyoidhinishwa na Serikali,[216] kuzingatia uendeshaji na matengenezo ya mfumo,[217] kuhakikisha kuwepo kwa wafanyakazi wenye uwezo wa kusaidia shughuli za mfumo huo,[218] kuanzisha utaratibu wa usaidizi wa watumiaji wa mfumo,[219] na kuvifanyia matengenezo ya mara kwa mara ya mifumo kila inapohitajika.[220]

(d) Rasilimali za TEHAMA za Serikali

Sheria imezitaka taasisi za serikali kufanya matumizi sahihi na kusimamia rasilimali za TEHAMA kwa uangalifu na nidhamu.[221] Rasilimali hizo zinatakiwa zilingane na bei na matumizi yazingatie programu inayoanzishwa,[222] sheria pia imeziagiza taasisi hizo kubuni au kutumia programu zilizoidhinishwa kwa ajili ya mawasiliano ya kibiashara.[223] Sheria imesisitiza kuhakikisha rasilimali za TEHAMA zinatumika kwa manufaa ya Serikali katika utoaji wake wa huduma.[224]

Katika kuhakikisha kwamba vifaa vipya na vikongwe vinavyotumika ipasavyo Taasisi hizo zimetakiwa kuanzisha daftari kwa ajili kutunza kumbukumbu ya vifaa hivyo kwa ajili ya uthibitisho kutoka Mamlaka.[225] Sheria imesisitiza matumizi ya vifaa hivyo lazima yafanywe kwa mujibu wa muongozo na maelekezo kutoka Mamlaka.[226]

[215] kifungu cha 25 (b) (i)
[216] kifungu cha 25 (b) (ii)
[217] kifungu cha 25 (c)
[218] kifungu cha 25 (c) (i)
[219] kifungu cha 25 (c) (ii)
[220] kifungu cha 25 (c) (iii)
[221] kifungu 26 (1)
[222] kifungu cha 26(1) (a)
[223] kifungu cha 26 (1) (b)
[224] kifungu cha 26 (1) (c)
[225] kifungu cha 26 (1) (d)
[226] kifungu cha 26 (1) (e)

(e) Utoaji wa Huduma za Serikali Mtandao

Sheria imezipa uwezo Taasisi za Serikali kutumia taarifa (data) kutoa taarifa, au kutoa huduma kwa njia ya mtandao. Katika kuhakikisha taarifa hizo zinatolewa kwa mujibu wa sheria,[227] Waziri amepewa uwezo wa kutoa miongozo juu ya taarifa za kieletroniki zinavyoweza kutolewa.[228] Aina za sahihi za kielektroniki zimeainishwa pale nyaraka hizo zinapohitaji uwepo wa sahihi hiyo.[229]

Sheria pia inasisitiza kwa watu wanaotoa huduma wazingatie weledi katika kutoa huduma, ubinadamu, na udhibiti wa siri katika utoaji wa huduma.[230] Waziri amepewa mamlaka ya kuweka vigezo kwa watu wanaotoa huduma (service provider) katika kuendesha serikali mtandao.[231]

(f) Utambuzi wa Huduma za Serikali Mtandao

Sheria imezitaka Taasisi za Serikali zinazotoa huduma kwa njia ya mtandao kuhakikisha kwamba huduma zinazotolewa zinakwenda sambamba na malengo ya Taasisi.[232] Sheria imesisitiza juu ya uimarishwaji wa utoaji wa huduma za kibiashara kwa njia ya kieletroniki ili kuhakikisha kuwa huduma hizo zinakuwa endelevu na zenye kuboreshwa.[233] Sheria imesisitiza kwamba huduma za kimtandao zinazotolewa zinakuwa bora (reliable) na zenye kuwasaidia wananchi moja kwa moja.[234]

[227] kifungu cha 27
[228] kifungu cha 27 (a)
[229] kifungu cha 27 (b)
[230] kifungu cha 27 (e)
[231] kifungu cha 27 (d)
[232] kifungu cha 28 (a)
[233] kifungu cha 28 (b)
[234] kifungu cha 28 (c)

Sheria imesisitiza njia sahihi na matumizi mazuri ya lugha, ambayo itawezesha watumiaji kuweza kupata huduma zinazokusudiwa kutolewa kwa njia ya mtandao.[235] Sheria imesisitiza huduma zitakazotolewa zizingatie mahitaji ya watu maalum[236] kama vile watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Sheria imesisitiza kwamba huduma zitakazotolewa ziweze kumsaidia mtumiaji wa huduma hizo.[237]

(g) Kupunguza matumizi ya Karatasi

Sheria imezitaka Taasisi za Serikali kuhakikisha kwamba inapunguza matumizi ya karatasi iwezekanavyo kwa kutayarisha mifumo itakayosaidia mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali na kuzifanya Taasisi hizo ziweze kuwasiliana kwa njia ya mtandao katika shughuli zao za kazi za kila siku.[238] Katika kutekeleza hayo Waziri atawajibika kuandaa Kanuni ya utekelezaji wa kifungu hicho.[239]

(h) Ushapishwaji wa Nyaraka kwa njia ya kieletroniki

Sheria imesisitiza kwamba Taasisi za Serikali pale ambapo sheria imetaka kufanya hizo, zinaweza kuwasilishwa kwa njia ya mtandao kutoka Taasisi moja hadi nyengine. Utaratibu huo inaweza kutumika vilevile pale mahitaji yanaporuhusu kuweza kuchapishwa katika gazeti rasmi la Serikali.[240]

[235] kifungu cha 28 (d)
[236] kifungu cha 28 (e)
[237] kifungu cha 28 (f)
[238] kifungu cha 29 (1)
[239] kifungu cha 29 (2)
[240] kifungu cha 33

4. **Tonga**

Tonga imeanzisha Sera ya Mawasiliano ya mwaka wa 2000, na marekebisho ya sera katika eneo la ICT kwa nia ya kujumuisha shughuli za kiuchumi mtandaoni yamefanyika. Mambo mengine ambayo bado yanazingatiwa ni pamoja na mpango mkakati wa IT wa utumishi wa umma, sheria kuhusu sahihi za kielektroniki na uthibitishaji wa utambulisho wa watumiaji wa mtandao na ushirikiano wa kimataifa kuhusu usalama kuhusu masuala ya mtandao.[241]

Katika mwaka 2009 Serikali ya Tonga imeimarisha masuala ya ICT katika elimu, afya, uendelevu wa mazingira, na ukuzaji wa viwanda, aidha Tonga ina kamati ya kitaifa ya ushauri ya ICT na Shirika la Mawasiliano la Tonga linasimamia usimamizi wa DOMSAT ya nchi na mwaka 2013 kwa mara ya kwanza Tonga imeweka Fibre Optic Submarine Cable System.[242]

Aidha mbali ya juhudi hizo, Tonga ilipitisha Sheria ya Mawasiliano Nam. 13 ya mwaka 2015 na marekebisho makubwa yalifanywa kwa sheria ya awali inayohusu redio, telegraph na utangazaji ili kuzingatia matumizi ya teknolojia ya utangazaji wa kidijitali.

Mbali ya sheria hii ya Mawasiliano, Tonga ina sheria maalum ya Makosa kwa kutokutekeleza taratibu za Mawasiliano ya Kielektroniki[243] na Sheria Makosa ya Kompyuta ya mwaka 2003.[244]

---

[241] World Bank Inaternational Development Association Report, PAD2863 Kingdom of Tonga , April, 2019
[242] National ICT Plan 2009
[243] Electronic Communication Abuse Offences Nam. 23 ya mwaka 2020
[244] Computer Crimes Act Nam. 14 ya mwaka 2003

Sheria ya Makosa ya Kompyuta imewekwa kwa lengo la kusimamia makosa ya kompyuta na kukusanya na kutumia ushahidi wa kielektroniki kupitia kompyuta. Aidha sheria hii imeweka makosa ya kuchukua taarifa kinyume na taratibu, [245] kuingilia mifumo ya taarifa kinyume na taratibu, [246] kuziunganisha kompyuta ili zionenane kinyume na taratibu,[247] kutumia vifaa vya kompyuta visivyoruhusiwa,[248] kutengeneza na kutoa taarifa kinyume na taratibu, [249] na usiri wa taarifa.[250]

Aidha Sheria ya makosa ya matumizi ya kielektroniki ya Nam. 23 ya mwaka 2020, imeweka makosa kwa kutoa huduma za kielektroniki isivyotakiwa, [251] kuchapisha na kusambaza taarifa, [252] makosa ya "data production",[253] majukumu ya watoa huduma za kielektroniki na dhabu zao zimeewekwa katika kifungu cha 20 na 21.

5. **Vanuatu**

Kwa sasa hakuna Sera jumuishi ya kitaifa ya ICT, lakini mipango iliyopo inatosha kusaidia tovuti ndogo za serikali (hasa kwa taarifa za kifedha na kibiashara). Muhimu hata hivyo, Vanuatu imepitisha sheria mbili zinazohusu biashara ya kielektroniki. Hizi ni Sheria ya Miamala ya Kielektroniki Nam. 24 ya mwaka 2000 na Sheria ya Biashara ya e-Business Nam. 25 ya mwaka 2000.

[245] Kifungu cha 4
[246] Kifungu cha 5
[247] Kifungu cha 7
[248] Kifungu cha 8,
[249] Kifungu cha 11 na 12
[250] Kifungu cha 17
[251] Kifungu cha 4
[252] Kifungu cha 8 na 9
[253] Kifungu cha 15

Sheria ya Miamala ya Kielektroniki inalenga kudhibiti kasi inayoongezeka ya miamala ya kielektroniki, ambayo ni maarufu leo. Hii kimsingi ni kutokana na mienendo inayoibuka ya matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa shughuli za kibiashara zinazotokana na hadhi ya Vanuatu kama kituo cha baharini.

Sheria inahusika na mahitaji ya kisheria ya kumbukumbu za kielektroniki; mawasiliano ya kumbukumbu za elektroniki; saini za elektroniki; usimbaji fiche na ulinzi wa data; na wasuluhishi na watoa huduma za e-commerce. Vipengele hivi vinavyoibuka vya biashara ya mtandaoni sasa vinadhibitiwa nchini Vanuatu.[254]

Sheria ya Biashara ya Kielektroniki inalenga kukamilisha, kwa maana ya jumla, uendeshaji wa miamala ya biashara ya kielektroniki. Hata hivyo, upeo wa sheria ni mdogo kwa biashara za kielektroniki zinazofanywa na makampuni ya kimataifa. Si ya usaidizi wa jumla kwa aina zote za mikataba au miamala ya mtandaoni. Sheria inahusu mikataba ya mtandao; mikataba ya biashara ya elektroniki; vyumba vya mtandao na akaunti za biashara za kielektroniki.

Kama ilivyoelezwa hapo awali, sheria za Vanuatu si sehemu ya mkakati wa kitaifa wa IT au sera ya e-commerce ya serikali. Kuna maendeleo fulani. Hata hivyo, mpango wa sasa ni mdogo kwa mahitaji ya sekta binafsi, ambayo kwa vyovyote vile pia yamejikita katika sekta ya benki, kamari ya mtandao na kasino za uchumi. Angalau kwa sasa, hakuna usaidizi wa sekta ya umma katika kuhakikisha kuwa msingi wa kiteknolojia unaibuka ili kutimiza sheria katika eneo hili. Lakini kiwango ambacho Vanuatu imetambua haja ya kupitisha sheria

[254] the Electronic Transactions Act 2000 and the E-Business Act 2000

hizi na inajiandaa kuunganishwa katika mapinduzi ya habari ya kimataifa, hata kama hatua kwa hatua inaonesha kwamba nchi inatazamia kuendeleza miundombinu muhimu ya kitaifa ya biashara ya mtandaoni.

6. **Fiji**

Fiji ina mipango ya kitaifa ya ICT, katika ngazi ya Idara ya mawasiliano ambayo inasaidia idadi ya tovuti za taarifa za Serikali. Kuna kituo cha ICT cha Serikali kilicho na vifaa vya kutosha na kinachofanya kazi ambacho kinahudumia mahitaji ya IT kwa Serikali. Waya (cable) za mawasiliano ya Southern Cross fibre-optics inayounganisha Fiji na Marekani, Australia na New Zealand imekamilika, hivyo kuruhusu ubadilishanaji wa data wa kasi ya juu na mawasiliano ya kidijitali kati ya nchi hizi. Kwa sasa kuna sheria ya biashara ya mtandaoni na inayohusiana na ICT ya mwaka 2008.[255]

Sheria ya Huduma za kielektroniki Nam. 26 ya mwaka 2008 imeweka usimamizi wa huduma za kielektroniki, ikiwemo kuthibitsha huduma za kielektroniki,[256] taratibu za kutoa taarifa na uwekaji saini za kielektroniki,[257] kukubaliwa taarifa za kielektroniki, na uthibitisho wake kama ushahidi na matumizi yake Mahkamani.[258] Sheria imeweka utaratibu wa malipo ya kielektroniki na masuala ya mikataba ya kielektroniki,[259] "electronic transation" na taratibu zake zimewekwa katika kifungu cha 17 hadi 20. Suala la usambazaji wa huduma kielektroniki na masharti yake yameelezwa katika

[255] The Electronic Transaction Act Nam. 26 ya mwaka 2008
[256] kifungu cha 6
[257] kifungu cha 7-8
[258] kifungu cha 9-12
[259] kifungu cha 14-15

kifungu 26-30. Mbali ya hayo sheria imeweka utaratibu wa saini za kielektroniki, misingi yake na jinsi ya kuthibitisha.[260]

7. **Samoa**

Samoa imeweka mipango kadhaa katika usimamizi wa Serikali Mtandao, na Kamati ya uendeshaji ya ICT iliundwa mwaka 2002. Sheria kadhaa zinazohusiana zilirekebishwa ili ziendane na mipango hiyo. Mnamo mwaka 1997 ilirekebisha Sheria yake ya Mawasiliano ili kuhimiza utendakazi na ukuzaji wa huduma za mtandao nchini.[261]

Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki ya Samoa (SAMOA Electronic Transactions ACT), Sheria Nam. 15 ya mwaka 2008, imeweka masharti ya kisheria ya huduma za kielektroniki na utaratibu wa maombi katika sehemu ya 2 ya sheria hiyo.[262] Aidha sheria hii imeweka utaratibu wa mawasiliano ya taarifa za kielektroniki,, utambuzi wake, masuala yanayohusiana na taarifa za kielektroniki, pamoja na utaratibu wa kupokea taarifa kielektroniki. [263]

Mbali ya Sheria hiyo kumekuwa na maendeleo zaidi katika mwaka 2019, ambapo Watu katika Samoa, wataweza kufanya na kupokea malipo kwa njia ya kidijitali, badala ya kutegemea pesa taslimu au hundi, katika hatua kubwa ya kusonga mbele kwa mifumo ya malipo, ambayo itafungua njia kwa watu wengi zaidi kupata huduma za kifedha.

[260] kifungu cha 21-25
[261] SAMOA Electronic Transactions ACT- Sheria Nam. 15 ya mwaka 2008
[262] Kifungu cha 6-11
[263] Kifungu cha 12-16

Hatua zilizopangwa katika sekta ya fedha, itachochea uvumbuzi na kuimarisha mifumo ya kidijitali, na kuweza kufanya kazi kwa wakati halisi, ili kuzuia majanga ya ukwasi katika mfumo huo.

Chini ya Mradi wa Malipo ya Pasifiki, wa Shirika la Fedha la Kimataifa, IFC, Mfumo wa Uhaulishaji wa moja kwa moja (electronic) utaanzishwa ili kuruhusu benki kuunganishwa na benki zao kuu na benki nyengine, kwa uhamishaji wa malipo ya kielektroniki.[264]

5.5.2 Uzoefu wa Hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa malengo ya uanzishwaji wa Serikali Mtandao

1. Lithuania

Katika nchi ya *Lithuania* moja ya malengo ya uanzishwaji wa Serikali mtandao yalikuwa yanahusisha mambo ya demokrasia, kukuza biashara kwa njia ya mtandao kuwapa wananchi taaluma ya komputa na matumizi ya mtandao (internent),[265] ujenzi wa Serikali mtandao ni suala gumu linahitaji mipango madhubuti, nyenzo, utashi wa kisiasa na ujenzi wa taasisi za kiserikali katika miundo ya kitekenolojia.[266] Pamoja na kuwaandaa wananchi katika matumizi ya serikali mtandao. Hii ndio sababu nchi tofauti zinafikia maendeleo tofauti katika utekelezaji wa serikali mtandao.

[264] SYDNEY, Machi 4, 2019, https://www.worldbank.org/en/news/press-release/2019/03/04/samoa-solomon-islands-and-vanuatu-to-introduce-digital-payment-systems
[265] Ministry of Interior, information Society Development Committee, State Budget Institution, Konstitucijos av. 15-89,0913 Vilnius, Liuthenia.,2001
[266] Ligita zailskaitic E- government implementation in lithunia, Kauns University of Technology Institute of Europe, Liuthenia

Lithuania ilipitia katika hatua mbalimbali katika utekelezaji wa Serikali mtandao kwa mfano, kukuza uelewa kwa jamii juu ya taaluma ya kieletroniki na Serikali mtandao, kuandaa mifumo ya kisheria na mifumo ya kitaasisi katika kufiki malengo ya Serikali mtandao, kuzitayarisha taasisi za Serikali kwa ajili ya malengo ya utekelezaji wa Serikali mtandao.

2. ISRAEL

Serikali ya Israel imeanzisha mamlaka ya ICT ambayo ipo chini ya Wizara ya Fedha kuanzia 2015. Mamlaka hii imekuwa ikifanya kazi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika kuhakikisha Serikali ya Israel inafikia malengo ya utekelezaji wa Serikali mtandao imeanzisha kituo cha kukuza ubunifu wa kitekenolojia ili kuhakikisha kwamba huduma kwa jamii zinafanika kwa njia ya uwazi, kwa ufanisi na kuokoa muda na fedha kwa wananchi na wafanyabiashara.[267]

Kitengo cha Serikali mtandao kinaajiri zaidi ya wafanyikazi 250 katika ukuzaji, kupokea maombi, kuchuja usalama wa habari, ukuzaji wa mifumo, upangishaji, mawasiliano, utambulisho wa kidijitali, usimamizi wa mradi, usimamizi wa wateja.

Dhamira ya kitengo cha Serikali mtandao katika mamlaka ya ICT ni kuendeleza na kuendesha miundombinu salama ya teknolojia, na kutoa ufumbuzi kwa wateja na washirika katika mashirika ya Serikali, ili kufanya huduma za Serikali zipatikane kwa wananchi, wafanyabiashara na umma kwa ujumla, na

[267]Boaz Chean and David Rashty, e- government in Israel, Ministry of Finance General Acountant Office, September 2002

kuunganisha wizara kwa huduma za mtandao.[268] Mikakati iliyotumika imegawika katika awamu tano kama zifuatazo:

1. Kuimarisha mifumo ya ndani ya mawasiliano;
2. Kuunganisha mifumo ya utendaji katika serikali;
3. Kutafuta miundo mbinu mipya na sahihi;
4. Huduma kwa miundombinu;
5. Kuhakikisha kwamba kunapatikana nyenzo za kiteknolojia kwa ajili ya kutoa taaluma.[269]

3. KENYA

Madhumuni ya jumla ya Serikali mtandao katika nchi ya Kenya ni kuifanya Serikali ya Kenya kuwa yenye kutoa matokeo kwa jamii, yenye ufanisi na inayotilia mkazo maendeleo ya jamii.[270] Madhumuni yanajumuisha:

(a) Kuboresha mashirikiano baina ya taasisi za Serikali kwa kupunguza matumizi ya nguvu nyingi katika uzalishaji na utoaji huduma na kukuza ufanisi kwa kutumia rasilimali zilizopo.

(b) Kuongeza ushindani kwa kutoa taarifa katika wakati muafaka na kutoa huduma kwa jamii.

(c) Kuondoa mzigo wa gharama za uendeshaji wa Serikali, raia na Asasi za kiraia katika uzalishaji wa bidhaa na huduma zinazoweza kutolewa kwa njia za kieletroniki.

(d) Kutoa fursa kwa raia kushiriki katika harakati za kuijenga Kenya kielektroniki.[271]

---

[268] Digital Government in the State of Palestine –United Nations https://www1.undp.org
[269] The Government ICT Authority 2019=2021 Action Plan
[270] Cabinet office, office of the President, e- Government strategy ukurasa 1&2 Machi, 2004
[271] ukurasa 1

(a) Kuanzishwa mfumo wa kimawasiliano ya kieletroniki baina ya taasisi za kiserikali

Katika utaratibu huu serikali ya Kenya ililazimisha taasisi zote za kiserikali kufanya shughuli zake za kila siku kwa njia ya kieletroniki. Taasisi hizo zililazimika kufanya miamala ya kibiashara miongoni mwa taasisi hizo kwa njia ya kieletroniki kwa kutumia "internent". Utaratibu huu ulitumika kwa taasisi hizi katika kubadilishana taarifa za kiserikali kwa njia za kimtandao.[272]

(b) Utayarishaji na uboreshaji wa dhana za mawasiliano katika taasisi za serikali.

Katika kuhakikisha Serikali ya Kenya inafikia malengo yake ya mawasiliano ya kimtandao katika taasisi za Serikali ilifanya maboresha makubwa katika taasisi hizo kwa kuweka mifumo ya uendeshaji katika suala ya mawasiliano ya kieletroiniki ikiwemo kuweka mifumo na mageuzi katika utendaji, Kuweka mifumo ya kisheria na usimamizi, na kubadilisha mfumo wa serikali na kuweka mifumo rafiki ya mawasiliano ya kimtandao.

4. ESTONIA

Estonia ni miongoni mwa nchi zilizoorodheshwa mara kwa mara katika viwango vya kimataifa vya ubora wa maisha, elimu, uboreshaji wa huduma za umma kwa kutumia mfumo wa kikidijitali na kuenea kwa makampuni ya teknolojia. Maendeleo ya Serikali mtandao katika nchi ya Estonia yalitokana na misingi mikuu iliyomo katika Sera ambayo ilipitishwa na Bunge la Estonia iliyoanzisha mageuzi ya kidijitali ili kuongeza ufanisi wa michakato yake pamoja na jinsi itakavyoweza kutoa huduma kwa umma kwa ufanisi zaidi.

[272] ukurasa wa 4

(a) Kuanzishwa kwa kadi za kieletroniki

Mkakati wa kwanza ilikuwa ni kutengeneza kitambulisho cha kidijitali (ID Card), kitambulisho hiki kilifanywa kuwa cha lazima na kilizingatiwa kama njia ya kutambua watu binafsi katika ulimwengu wa kidijitali, na kimefanywa kama ni ufunguo unaoruhusu ulimwengu ulingane na dijitali. Kadi hiyo ilitolewa na Serikali na ilichukuliwa kama hati ya lazima kwa wananchi wa Estonia. Kadi zimesaidia benki za Estonia kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika Benki za Mtandaoni na zilikuwa zikitumia kadi ya kitambulisho cha kielektroniki kama njia ya kupata huduma zao. Serikali ilihakikisha miundombinu inafanyakazi zake vizuri zaidi.

(b) Uboreshaji wa mifumo ya kizamani

Mkakati wa pili ilikuwa ni kuboresha mifumo ya zamani ya mawasiliano kwa kuweka mitambo na dhana za kisasa pamoja na kuandaa wataalamu. Kwa ajili ya uendeshaji wa mitambo hiyo. Katika kufanikisha malengo hayo nchi ya Estonia ilianzisha kituo cha uwekaji wa taarifa (data management infrastructure) ili kuhifadhi taarifa na kuziwasilisha katika sehemu husika.

(c)Kuanzishwa kwa mifumo ya kieletroniki

Katika kuhakikisha kwamba inatokana na mifumo ya kizamani kwenda katika mfumo wa kidijitali, Estonia imezindua kampeni ya matangazo nchi nzima ili kuelezea faida ya serikali mtandao kwa wakulima, wafanyabiashara pamoja na wafanyakazi juu ya umuhimu wa matumizi ya kidijitali. Kwa mfano wakulima walifundishwa namna ya kujaza nyaraka kwa njia ya kidijitali na wakulima wengi walinufaika na mfumo huo.

Kwa upande wa Wafanyabiashara walipata mafunzo juu ya ufanyaji wa biashara kwa njia ya kieletroniki ndani na nje ya nchi kwa njia ya haraka na yenye usalama. Na kwa upande wa watumishi wa umma walipatiwa mafunzo jinsi ya kujaza mikataba mbalimbali ya kazi pamoja na kupata taarifa juu ya mishahara yao, kupandishwa vyeo, maslahi, likizo. Jamii nzima ilifaidika na taaluma ya huduma kwa njia ya kimtandao.

(d) Uwepo wa miundo mbinu imara

Kutokana na miundombinu imara nchi ya Estonia inafanyakazi vizuri katika maeneo la kieletoniki, watumiaji tisa kati ya kumi hubadilishana taarifa mara kwa mara na Serikali mtandao. Kwa ujumla, matumizi ya kielektroniki yamekuwa yakiongezeka katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, na hii imewafanya nchi nyengine wajifunze ujuzi kupitia Estonia.

Kutokana kwa kuimarika kwa teknolojia, wananchi wa Estonia na majirani zake wa Skandinavia, huweza kubadilishana taarifa mara kwa mara na Serikali yao mtandaoni. Kila raia anamiliki utambulisho wa kidijitali na sahihi ya kielektroniki kupitia ugatuzi wa data ambao umefanywa na nchi hiyo ili kuwawezesha wananchi kushughulikiwa maombi yao kwa ufanisi na usalama na kuondoa vikwazo vya kiutawala kwa wananchi na watumishi wa umma. Data nyingi za watumiaji zinapatikana kwa uwazi katika taasisi zote za serikali, vile vile wananchi wanaweza kufuatilia maombi yao yanayohusiana na data zao na pia wana haki ya kutaka ufafanuzi zaidi kuhusiana na matumizi ya data hizo.

5. MAURITIUS

Nchi ya Mauritius imeweka mikakati maalum ya kuhakikisha kuwa wananchi wote wa Mauritius wanatumia mawasiliano ya kimtandao wanapotaka kuwasiliana na Serikali kwa ajili ya kupata huduma hasa wale wenye ujuzi mdogo wa kutumia mtandao, kuwashirikisha wananchi kwa kila hatua na baadae kutafuta maoni juu ya ubora wa mfumo huo mpaka utakapokidhi mahitaji ya wananchi hao.

Serikali ya Mauritius ilianzisha utaratibu wa manunuzi kama njia ya majaribio kuelekea manunuzi ya kieletroniki. Utaratibu huu ulikwenda sambamba na utoaji wa elimu kuhusu manunuzi kwa njia ya kidijitali kwa wafanyakazi wa taasisi za Serikali na wasambazaji wa bidhaa.

5.5.3 Hitimisho la nchi mbalimbali

Kutokana na hali hiyo, utafiti huu umebaini kwamba ni wazi kuwa nchi za visiwa bado zina mengi ya kufanya katika masuala ya sera na uwekezaji ikiwa ni kuweka miundombinu muhimu kwa ajili ya uendeshaji wa biashara ya mtandaoni na uendeshaji wa Serikali mtandao. Isipokuwa kwa Vanuatu, ambapo mfumo wa kisheria umeanzishwa, Samoa, Fiji, Tonga, Estonia na nyenginezo zinahitaji sheria mahususi sana kushughulikia vipengele mbalimbali vya jambo hili jipya. Faida za miamala ya kielektroniki sio tu kwa sekta ya kibinafsi.

Sekta ya umma itakuwa na mengi ya kupata kwa kujihusisha nayo pia. Kwa nchi zilizo na rasilimali chache, msingi wa kiteknolojia na utaalamu, manufaa ya miundo ya serikali ya mtandao katika utawala na demokrasia haiwezi

kupuuzwa. Ili kufikia manufaa haya, nchi katika eneo hili zinapaswa kuzindua mifumo ya kisheria inayoweza kutumika kwa shughuli za kielektroniki.[273]

Aidha utafiti umebaini kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Sheria Nam. 10 ya mwaka 2019. Imezingatia mambo muhimu yafuatayo katika sheria hiyo ambayo ni muhimu kuzingatiwa katika maandalizi ya sheria mpya inayokusudiwa kutungwa. Mambo hayo ni kama yafuatayo:

(a) uundwaji wa miundombinu ya Serikali;
(b) uanzishwaji wa miradi ya TEHAMA;
(c) kuanzishwa mifumo mipya ya serikali mtandao;
(d) utunzaji wa rasilimali za TEHAMA za serikali;
(e) utambuzi wa huduma za seriakli matandao;
(f) utoaji wa huduma za serikali mtandao kwa serikali na jamii;
(g) Upunguzaji wa matumizi ya karatasi na;
(h) uchapishaji wa nayaraka kwa njia za kieletroniki baina ya Taasisi moja kwenda Taasisi nyengine.

Aidha kwa upande wa vyombo vya utekelezaji wa maeneo mengine, sheria za nchi mbalimbali zimeonesha kuundwa kwa mamlaka au chombo ambacho kitasimamia utekelezaji wa uendeshaji wa Serikali Mtandao. Chombo hicho kinakuwa na nguvu ya kisheria ya kusimamia taasisi nyengine za Serikali.

[273] Meiyanti, R., et al.: Systematic review of critical success factors of e-government: definition and realization. In: 2017 International Conference on Sustainable Information Engineering and Technology (SIET), Malang, Indonesia. IEEE (2018)

Pamoja na maeneo yalioelezwa hapo juu, sheria za nchi mbalimbali na mipango imejumuisha na kutambua kutambua mikataba iliyofungwa kwa njia za kieletroniki, pamoja na makosa ya kimtandao pamoja na adhabu zake.

SURA YA SITA

6.0 MATOKEO YA UTAFITI

6.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu unaohusiana na mapitio ya Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Nam. 12 ya mwaka 2019. Matokeo ya utafiti huu yanatokana na sehemu kubwa ya njia za utafiti ambazo zimetumika kukamilisha kazi hii.

6.2 Njia zilizotumika katika Utafiti

Katika utafiti huu, njia zifuatazo zilitumika kukusanya maoni na kupata taarifa zilizoweza kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika utafiti.

1. Kufanya mikutano na wadau walioainishwa kwa ajili ya kutoa maoni.
2. Kuhoji baadhi ya wadau mbali mbali wakiwemo wataalam wa sekta ya mawasiliano ya habari.
3. Kupitia Sheria mbalimbali na Rejea ambazo zinazungumzia masuala ya Serikali mtandao.
4. Kukusanya taarifa mbali mbali za Serikali na taasisi zake zinazohusiana na utafiti huu na kuzilinganisha na malengo ya hadidu rejea za utafiti.
5. Kuangalia uzoefu wa nchi nyengine kuhusiana na masuala ya serikali mtandao.
6. Kupitia mikataba ya kimataifa inayohusiana na serikali mtandao.

Aidha, marejeo ya Sera, vitabu, Makala na nyaraka mbali mbali zinazozungumzia Serikali mtandao zimepitiwa na Tume, kwa lengo la kupata

uelewa wa Serikali mtandao na jinsi inavyofanya kazi, namna ya kuendeleza masuala ya Serikali mtandao, faida za Serikali mtandao, changamoto zilizopo na jinsi ya kuziondoa changamoto hizo na kuja na mapendekezo yatakayoimarisha Serikali mtandao ili itoe mchango mkubwa zaidi katika uchumi na utendaji wa shughuli za Serikali kwa ufanisi zaidi.

Wadau wanaohusika na Serikali mtandao ikiwemo wataalamu wa TEHAMA kutoka katika Wizara na Mashirika ya Serikali, wataalamu wa CAG, wanasheria, watendaji wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, wadau kutoka Makampuni ya Simu za Mkononi, wataalamu wa TEHAMA kutoka Chuo cha Sayansi na Teknolojia, kampuni zinazotoa huduma za mitandao, watumiaji wa mitandao na kompyuta, wadau kutoka taasisi za Serikali na taasisi binafsi walialikwa na Tume ili kutoa michango yao.

6.3 Upeo wa utafiti

Utafiti huu umelenga kuangalia utekelezaji wa sheria ya Serikali Mtandao Nam. 12 ya 2019 na mapungufu yaliyobainika katika sheria hiyo, sambamba na uhalisia wa hali iliyopo pamoja na matakwa ya mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeiridhia, Sera za Zanzibar ikiwemo Sera ya Mawasiliano ya Habari, Sera ya Serikali Mtandao, Dira 2050 na MKUZA III.

6.4 Ukomo wa utafiti

Katika kufanya utafiti huu, mapungufu yafuatayo yamejitokeza:

(a) Kutokuwepo kwa utaratibu na miongozo mizuri inayohusiana na utekelezaji wa shughuli za Serikali mtandao;

(b) Kutokuwepo uelewa wa kutosha kwa jamii na taasisi za Serikali kuhusu Serikali mtandao;
(c) Kukosekana utaratibu mzuri wa kisheria utakaowezesha usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Serikali mtandao.

6.5 Sampuli za utafiti

Kufikia malengo ya utafiti huu, jumla ya makundi tisa (9) yalihusishwa. Makundi hayo yalijumuisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Taasisi za binafsi zinazohusiana na masuala ya Serikali mtandao, viongozi wanaosimamia masuala ya mifumo ya teknolojia ya mawasiliano, maafisa wadhamini wa baadhi ya wizara, Wataalamu kutoka mashirika na wakala wa Serikali, Wadau wanaotoa huduma za mitandao hapa nchini, wadau kutoka Chuo cha Sayansi na Teknolojia, Wanasheria pamoja na wananchi mbali mbali ambao ndio watumiaji halisi wa mitandao kwa shughuli za kila siku.

Vikao vya wadau vilifanyika katika maeneo tofauti ya Zanzibar. Jumla ya wawakilishi wote walioshirikishwa ni 93. Katika idadi hii ya washiriki wanawake walikuwa ni 31 na wanaume walikuwa ni 62.

Wawakilishi kutoka makundi mbali mbali ya wadau ambao wameshiriki katika utafiti huu wametoa mapendekezo tofauti kuhusu Serikali mtandao na malengo yake. Hata hivyo, kila kundi lilikuwa na maslahi tofauti na kwa kila kundi wawakilishi walitafautiana sana na wawakilishi katika makundi mengine ya wadau.
Kwa baadhi ya makundi mengine, hakukuwa na tofauti kubwa katika maoni na mapendekezo. Matokeo yetu, hata hivyo, yanaweza kuwa na athari kwa Wadau

katika usimamizi wa Serikali mtandao. Jadueli Nam. 1 linaonesha washiriki wote wa Utafiti kwa Zanzibar.

Jadueli Nam. 1: Idadi ya washiriki wote wa Utafiti.

Makundi	**Waliohudhuria**	**Walioalikwa**	**Asilimia**
Wadau kutoka Taasisi za Serikali	49	54	90.7
Wadau kutoka Taasisi za Binafsi	7	10	70.0
Wadau kutoka Makampuni ya Simu za Mkononi	2	4	50.0
Wataalamu wa ICT kutoka Chuo cha Sayansi na Teknolojia	2	2	100.0
Kampuni zinazotoa Huduma za Mitandao	4	6	66.7
Wanasheria	7	8	87.5
Wadau kutoka Mashirika ya Serikali	12	27	44.4
Waandishi wa Habari	2	2	100.0
Watumiaji wa Mitandao na Kompyuta	8	12	66.7
Jumla	**93**	125	**74.40**

Chati Nam.1: Mchanganuo wa washiriki kwa Jinsia



Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, asilimia 66.7% ya washiriki walikuwa wanaume wakati asilimia 33.3% walikuwa wanawake. Washiriki wanawake walikuwa wachache kutokana na ukweli kwamba fani ya masuala ya TEHAMA imeshirikisha wanaume wengi kuliko wanawake.

Chati Nam. 2: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu



Matokeo yanaonesha kuwa asilimia (15.1%) ya washirki wana elimu ya sekondari ambao kiujumla ni wananchi wa kawaida ambao ndio watumiaji wa mitandao na asilimia (14.0%) walikuwa na elimu baada ya sekondari, na asilimia (71.0%) walikuwa na elimu ya juu kuanzia Digirii ya kwanza na kuendelea. Lengo kubwa la kufanya uchambuzi huu, ni kuonyesha kwamba mbali ya watendaji wa Serikali waliotoa maoni, uhalisia unaonesha kwamba makundi yanayojishughulisha na masuala ya mtandao yana elimu ya juu. Chati Nam. 2 linaonesha kuwa shughuli za mitandao zinafanywa na wataalam.

Chati Nam. 3: Idadi na asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri



Matokeo ya utafiti huu yanafafanua kuwa, washiriki wengi (73.1%) walikuwa na umri kati ya miaka 25-60, ikifuatiwa na kundi la vijana wenye umri kati ya miaka 15-24 asilimia (20.4%) na kundi la wazee kuanzia miaka 60 na kuendelea ni asilimia (6.5 %).

6.6 Hadidu Rejea

Katika kufanya utafiti huu, Hadidu Rejea zifuatazo zilizingatiwa:

(a) Kufanya utafiti wa kina katika taratibu za usimamizi wa Serikali mtandao;

(b) Kuangalia uzoefu wa sheria za nchi mbali mbali kuhusiana na masuala ya Serikali mtandao na kuangalia namna uzoefu huo huo unavyoweza kutumika kwa mazingira ya Zanzibar;

(c) Kuangalia sera na sheria mbali mbali za Zanzibar zinazohusiana na Serikali mtandao na utafiti wa Serikali mtandao unavyoweza kusaidia kuweka mazingira mazuri ya sheria katika matumizi ya mitandao na maeneo mengine ya TEHAMA;

(d) Kupitia mikataba ya kimataifa na uzoefu wa nchi mbalimbali inayohusiana na eneo hili la utafiti na kuangalia mambo ya msingi yanayoweza kuzingatiwa katika Sheria itakayopendekezwa.

(e) Kutoa mapendekezo yanayofaa ya kisheria na kisera kwa ajili ya kutatua changamoto zinazokwaza na namna ya kuweka mfumo wa kisheria utakaoimarisha masuala ya Serikali mtandao, pamoja na mapendekezo mengine ya kiutendaji.

6.7 Ukomo wa Utafiti

Katika kufanya utafiti huu mapungufu yafuatayo yamejitokeza:

(a) Kutokuwepo kwa uelewa wa sheria miongoni mwa wadau juu ya Serikali mtandao inavyotakiwa kufanya kazi;

(b) Kutokuwepo kwa wadau wa kutosha katika maeneo ya vijijini ambao wanatumia TEHAMA katika shughuli zao za kila siku;

6.8 Matokeo ya utafiti

Baada ya kufanya mapitio katika eneo hili la serikali mtandao, utafiti wetu ulibaini matokeo yafuatayo:

6.8.1 Mapendekezo ya Kisera

Pamoja na umuhimu mkubwa wa sera za usimamizi wa taarifa za kielektroniki, Matokeo ya Utafiti yameonesha kuwa kwa sasa, hakuna sera mahususi za usimamizi wa mifumo na taarifa za kielektroniki katika utumishi wa umma. Badala yake, Serikali inatoa waraka na miongozo mara kwa mara kwa taasisi na kiutendaji ili kuhakikisha kuna mazingatio ya taarifa za umma.

Hii inathibitisha kwamba taasisi za umma nchini zinaunda, kuandaa, kudumisha, na kusambaza taarifa zao za kidijitali kwa kutumia mipango ya kibinafsi bila mwongozo wa kawaida. Hivyo, kuna haja ya kuwekwa utaratibu mzuri wa Kisera ili kulinda usalama wa taarifa za Serikali na taasisi za umma. Zaidi ya hayo, uwepo wa Sera utasaidia kuhakiki taarifa za taasisi za umma kwa uhalisia wake, uaminifu wa taarifa hizo na kuwa na uhifadhi wa taarifa za muda mrefu.

6.8.2 Kisheria

Katika utafiti huu, Tume imebaini haja ya kuwa na Sheria ambayo haitokuwa na upeo mpana na kujikita katika usimamizi wa taasisi za Serikali, pamoja na kuweka wazi huduma ambazo zinaweza kushirikisha taasisi zaidi ya moja. Aidha, wakati wa utafiti huu tulibaini kuwepo uwezekano (risk) wa kutokea utata au muingiliano baina ya Mamlaka ya Serikali Mtandao na taasisi nyengine na hivyo kuwepo haja ya kubainisha kwa uwazi zaidi maana za maneno ili zifahamike zaidi na kuepusha utata huo.

Utafiti huu ulibaini masuala mbali mbali ya kisheria yanayohitaji kuzingatiwa kutokana na mwelekeo na mabadiliko ya teknolojia. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

(a) Utafiti umebaini kuwa Sheria iliyopo sasa haikuanzisha chombo imara cha kusimamia utekelezaji wa uendeshaji wa Serikali Mtandao. Chombo hicho kwa sasa hakina nguvu ya kisheria ya kutosha kusimamia taasisi nyengine za Serikali na hivyo hakiendani na uzito wa majukumu yaliyowekwa katika chombo hicho. Aidha, chombo kilichopo hakina

uhuru wa matumizi kwa kuwa hakina voti (vote) yake yenyewe ili kukipa nguvu chombo hicho kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(b) Aidha, utafiti umebaini kuwa Sheria ilivyo sasa, haina masharti yanayotosheleza kuweka masharti ya kuzibana taasisi za umma kufuata miongozo itakayotolewa na Mamlaka inayosimamia masuala ya Serikali mtandao kuhusiana na mambo yote yanayohusu matumizi ya elektroniki ikiwemo ununuzi wa mifumo na vifaa vya kielektroniki.

(c) Kwa upande mwengine, imebainika kuwa Sheria haina masharti ya kisheria yanayoipa Mamlaka ya Serikali Mtandao, uwezo wa kutoa vibali au ruhusa katika ununuzi wa vifaa vinavyohusiana na Serikali mtandao kwenye Taasisi za Serikali, sifa, viwango, mifumo ya TEHAMA au hata kushauri, kuthibitisha na kubatilisha masuala ya ununuzi wa vifaa vinavyohitajika katika serikali mtandao kwa kuzingatia uweledi na maslahi mapana ya nchi.

(d) Utafiti pia umebaini kuwa hadi sasa hakuna ushirikishwaji wa Dijitali (Digital Inclusiveness) ambao ni utaratibu wa utoaji wa huduma za kidijitali unaohusisha watu wa kawaida na watu wenye mahitaji maalumu. Katika utaratibu huu, ilipaswa kuwepo kwa utaratibu rahisi wa kimtandao ili watu wenye uwezo tofauti waweze kutumia. Kwa mfano matumizi ya kimtandao kwa watu wasioona, wasiosikia na wengine wenye mahitaji maalumu. Kufanikiwa kwa suala hili la serikali mtandao kutawawezesha watu wa aina mbalimbali kuweza kumudu matumizi ya kimtandao na hivyo kuifanya nchi kuwahusisha wananchi wote katika matumizi ya kidijitali.

(e) Pamoja na kupitishwa kwa Sheria inayosimamia masuala ya serikali mtandao na kuanzishwa kwa Wakala wa Serikali Mtandao, bado hakuna

uwazi juu ya ushiriki wa raia katika Serikali na jinsi ya kupata taarifa katika ngazi zote za serikali. Utafiti huu pia umebaini kuwa bado hakuna elimu ya kutosha iliyotolewa kwa wananchi kuonesha kwamba ushiriki wa wananchi hao ni muhimu, kwa kuweka wazi matukio mbalimbali mtandaoni.

(f) Suala jengine ambalo utafiti huu ulibaini ni kutokuwepo kwa uwazi kisheria suala la ukuaji wa teknolojia nchini na mchango wake katika kuimarisha serikali mtandao;

(g) Utafiti huu pia umebaini kuwa pamoja na taasisi nyingi za Serikali kuwa na tovuti zinazoruhusu watumiaji kufanya miamala mtandaoni na kupata taarifa kutoka taasisi za umma kwa muda wote (24/7), bado usalama na udhibiti mzuri wa taarifa haujafafanuliwa kisheria;

(h) Kutokana na maoni ya wadau mbali mbali na utafiti uliofanywa, utafiti umebaini haja kubwa kwa Serikali kuimarisha utoaji wa huduma na taarifa kwa wananchi kupitia matumizi ya serikali mtandao.

6.8.3 Mapendekezo ya Kikanuni

Utafiti pia umebaini kwamba ili Sheria hii iweze kutekelezeka, kuna haja ya kuweka Kanuni zitakazosaidia usimamizi wa taasisi ya Serikali Mtandao kama "regulator" na hivyo kuhitajika miongozo ambayo itaonesha utaratibu unaotakiwa kutumiwa na taasisi za Serikali katika uwekaji wa taarifa, utoaji taarifa na kuratibu masuala yanayohusiana na Serikali Mtandao.

6.8.4 Kiutendaji

Utafiti huu umebaini kuwepo kwa yafuatayo ambayo yanahitaji hatua za kiutendaji ili kufanikisha lengo la Serikali la kuwa na Serikali Mtandao:

(a) Marekebisho ndani ya Serikali

Ndani ya Serikali nyingi, masharti ya wakala mtandao yamesababisha kurekebisha miundo ya taasisi na Wizara za Serikali ili kuweka mifumo ya serikali vizuri kubadilisha majukumu na shughuli zake kidigitali. Baadhi ya Serikali zimeunda Tume au vikosi kazi vya kushauri kuhusu mahitaji ya barabara kuu ya habari (roadmap) na mwelekeo wa uchumi kwa taifa. Mashirika ya udhibiti yamelazimika kushughulikia muunganiko (intergration) wa kiteknolojia na hitaji la kuunda miundombinu ya ziada ya kielektroniki, kama vile ufikiaji wa mtandao kwa njia pana, ili kusaidia mikakati ya kitaifa ya serikali mtandao.[274]

Hivyo Tume inapendekeza baada ya sheria kupitishwa kuangaliwa kwa kina maeneo au taasisi ambazo zitahitaji mabadiliko ya kimuundo au vyenginevyo kuendana na dhana ya Serikali Mtandao.

(b) Kutofautisha usimamizi wa wakala Mtandao na masuala ya ICT

Utafiti umebaini kwamba kuna haja ya kutenganisha majukumu ya msingi ya Wakala Mtandao na Masuala ya TEHAMA, ili Mamlaka ya Serikali Mtandao ishughulikie taasisi za Utumishi wa Umma na kuimarisha huduma za msingi za mawasiliano na uwekaji taarifa za Serikali. Upande wa TEHAMA unajumuisha Taasisi binafsi na Serikali na miundombinu na hivyo kuna haja ya kuweka wazi upeo wa kila taasisi. Imebainika kwamba Mamlaka ya Serikali Mtandao

[274] David Brown "Electronic government and public administration" International Review of Administrative Sciences, 2005 IIAS, SAGE Publications (London, Thousand Oaks, CA and New Delhi) Vol 71(2):241– ukurasa wa 6

inatakiwa kusimamia zaidi matumizi na upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi.

(c)Mipaka ya Utendaji

Tume ya Kurekebisha imebaini kwamba Wakala na Mamlaka za Serikali zinakuwa na majukumu mengi kuhusiana na masuala ya mtandao na pia zinahitaji kushirikiana na taasisi nyengine kupitia majukumu na utaalamu uliopo ktaika taasisi hizo. Kwa mfano, masuala ya ukaguzi na manunuzi ni masuala mtambuka ambayo mbali ya kuwepo Wakala Mtandao, kuna taasisi maalum zinazosimamia masuala hayo. Hivyo Sheria izingatie tahadhari hii ili kuepusha mgongano baina ya taasisi za umma.

(d) Uhusiano kati ya mifumo mbalimbali

Utafiti umebaini kwamba kwa kuwa Serikali mtandao haiwezi kufanya kazi ipasavyo bila miundo inayolingana ya kiteknolojia, ni muhimu kutambua uhusiano kati ya mifumo mbalimbali na kuichunguza. Teknolojia ya mtandao hutoa njia ya msingi ambayo miamala ya kielektroniki iliyoenea inaweza kufanywa kwa urahisi, kutokana na sababu ya eneo lao la kijiografia, makazi yaliyotawanyika na miundombinu midogo. Aidha Mpango wa Kisera kwa watumishi wa umma unapaswa kuwekwa kupitia manufaa na fursa zinazotolewa na taratibu za kielektroniki za utawala bora, ikiwemo uwezekano wa kuunda upya huduma za serikali ili kuhudumia umma. Ofisi zote za serikali inapobidi, zinapaswa kutoa vifaa kwa ajili ya ufikiaji wa umma kwa huduma za kielektroniki.

(e) Upatikanaji wa Huduma za Serikali

Utafiti umebaini kuwepo kwa haja kubwa ya utoaji wa huduma kadhaa za kijamii kwa njia ya serikali mtandao. Huduma hizo za kijamii zinajumuisha huduma za kisheria, Mahakama, huduma za afya, usajili na upigaji kura mtandaoni, ambazo zitasaidia katika kuboresha wigo wa upatikanaji wa huduma za serikali. Aidha, utafiti pia ulibaini kuwa matumizi ya Serikali mtandao katika huduma hizo itaharakisha utumiaji wa huduma hizi kwa umma kwa ujumla kwa kuzingatia kasi ya kushughulikiwa. Miundo ya serikali mtandao ina uwezo wa kuboresha utoaji na utoaji wa huduma za serikali hivyo, hii itakuwa faida katika kukuza utawala bora na uwazi kwa kuunganisha sekta za umma na za kibinafsi mtandaoni.

(f) Usanifu wa Mtandao (Architecture)

Utafiti huu pia umebaini kuwepo kwa changamoto za vifaa vya kusambaza au kubadilishana taarifa, sauti au video kati ya kompyuta zote zilizounganishwa katika mfumo wa mtandao wa mawasiliano wa kitaifa. Kwa mfano taarifa inayotumwa kutoka katika kompyuta moja hadi nyengine kupitia Mtandao husafirishwa kupitia “server” kadhaa bila mpangilio kwa kutumia njia bora zaidi hadi inapofika mahali ilipokusudiwa. Ili taarifa iweze kusafirishwa kupitia mtandao, kuna umuhimu wa kuwa na vifaa na miundombinu rafiki itakayowezesha kazi za Serikali Mtandao kufanyika kwa ufanisi.

Matumizi ya miundombinu hii ya kiteknolojia inamaanisha kuwa wakati wowote, taarifa tofauti zinatakiwa kufika katika eneo husika, udhibiti wa barua pepe kwa kutumia taratibu zilizowekwa, athari za kisheria katika teknolojia na

shughuli zinazohusika zinahitaji kuchunguzwa kwa mtazamo wa msambazaji wa bidhaa au huduma, iwe katika sekta ya umma au ya kibinafsi.

(g) Usalama wa taarifa (security)

Wakati wa kufanya mapitio ya Sheria hii hasa wakati wa vikao vya wadau, utafiti wetu umebaini kuwepo kwa hofu ya usalama wa taarifa za taasisi mbali mbali za umma kuingiliwa na wezi wa taarifa za mitandaoni (hackers). Matumizi ya teknolojia hutegemea miamala na vifaa vinavyohusisha umbali halisi unaotenganisha wahusika na uwezo wa kufanya mabadiliko ya papo hapo kwa hati za kielektroniki bila kugunduliwa kwa kiasi kidogo au bila kutambuliwa kabisa.

Ili kulinda usalama wa taarifa, kuna haja ya kuwa na wakala wa uthibitishaji wa taarifa ambaye ataunganisha, kuimarisha na kuendeleza rasilimali na kupunguza gharama kwa kuwa faragha inahitajika katika matumizi ya taarifa za umma mitandaoni na kuepuka uhalifu unaoweza kujitokeza katika matumizi ya teknolojia.

(h) Uthibitishaji wa Saini za kidigitali

Utafiti huu umebaini kwamba serikali mtandao na ubadilishanaji wa taarifa unahusisha tatizo la kuandika na kuthibitisha saini za kidijitali, jambo ambalo pia ni muhimu sana kwa shughuli za Serikali Mtandao.

Matumizi ya saini na kuthibitisha au kuhalalisha miamala ya kielektroniki kunahitaji kuwa na uadilifu mkubwa wa miamala ya mtandaoni na mikataba ya

biashara. Hivyo sheria zitahitajika ili kusaidia mageuzi kutoka mifumo ya kawaida hadi utaratibu wa kuweka saini katika nyaraka kielektroniki.

(i) Mafunzo

Utafiti wetu umebaini kuwa usimamizi wa Wakala wa Serikali Mtandao unahitaji uwekaji mzuri wa taarifa za kielektroniki na hivyo kunahitajika mafunzo maalum kwa madhumuni hayo. Mafunzo hayo yanajumuisha uweaji wa kumbukumbu za kielektroniki na programu ya usimamizi hasa kwenye moduli za usimamizi wa rekodi za kielektroniki ambazo ni za kinadharia zaidi kuliko vitendo.

Aidha, Tume imebaini kwamba mafunzo hayo yanahitaji kwenda sambamba na upatikanaji wa vifaa vya kuweka kumbukumbu za miamala mbalimbali na kufanya maamuzi. Kwa upande mwingine, tulibaini kuwepo kwa pengo kwa wataalamu wa ICT katika utumishi wa umma kukosa ujuzi wa kutosha unaohitajika kuhusu usimamizi wa kumbukumbu.

(j) Miundombinu ya ICT na Uwezo

Utafiti umebaini kwamba utendaji kazi mzuri wa Serikali Mtandao unahitaji vifaa vya usimamizi wa TEHAMA mifumo ya kielektroniki na uwepo wa fedha za kutosha kununua programu na mifumo mbalimbali.

Mbali ya uwepo wa kompyuta, Mitandao ya Maeneo ya Ndani, vifaa vya intaneti, mashine ya faksi (nukushi), printa, simu, na kuwa na idara za ICT zinazofanya kazi, baadhi ya ofisi za umma zilikuwa na vifaa zaidi katika suala la miundombinu ya kiteknolojia, na vifaa vya ICT, na wafanyakazi wenye uwezo.

Hivyo kuna masuala ambayo yanahitajika kufanywa kwa ajili ya usimamizi wa mifumo na taarifa za kielektroniki.

(k) Viwango vya huduma

Katika kuelekea kwenye Serikali mtandao, utafiti wetu pia umebaini kuwepo kwa changamoto ya viwango na kasi ndogo ya intanenti ambapo wananchi kwa ujumla wanakabiliwa na kikwazo hicho ambacho huzuia upakuaji wa haraka wa data na taarifa na huziba njia na barabara kuu (traffic) za Mtandao na kuongeza muda unaotumika kupata taarifa kwenye Mtandao. Hivyo changamoto hiyo huathiri vibaya upatikanaji wa huduma na bidhaa kupitia serikali mtandao.

(l) Uhifadhi wa takwimu na taarifa (Data)

Utafiti umebaini kuwepo matatizo katika kuunda na kusimamia hifadhi ya taarifa (data) za kielektroniki kwa matumizi ya sekta ya umma au ya kibinafsi. Hivyo ni muhimu kwa taratibu za uhifadhi data kuwa sahihi na kuzingatiwa katika sheria ili kuzuia udanganyifu na ufikiaji wa taarifa usioidhinishwa au matumizi mabaya. Kutokana na matokeo hayo ya utafiti, kuna haja ya kuweka vifaa madhubuti ili kushughulikia uhifadhi wa taarifa kwa ajili ya matumizi ya mifumo ya kidijitali.

SURA YA SABA

7.0 MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

7.1 Utangulizi

Sura hii inazungumzia Mapendekezo ya Tume kutokana na yaliyojitokeza katika utafiti wa mapitio ya Sheria ya Serikali Mtandao. Utafiti huo ulijumuisha uzoefu wa nchi mbali mbali, mikataba ya kimataifa, Sera na Sheria ziliopo na maoni ya wadau. Tume baada ya kukamilisha utafiti huu imeweka mapedekezo haya katika makundi yafuatayo:.

(a) Mapendekezo ya Kisera;
(b) Mapendekezo ya Kisheria;
(c) Mapendekezo ya Kikanuni; na
(d) Mapendekezo ya Kiutendaji.

7.1.1 Mapendekezo ya Kisera

Tume ya kurekebisha Sheria inapendekeza Sera ya Serikali Mtandao ifanyiwe mapitio katika maeneo yafuatayo:

(a) Sera ya Serikali Mtandao pamoja na mambo mengine, iainishe na kutilia mkazo mikakati ya kufikia malengo ya utekelezaji wa Serikali mtandao kama tulivyojfunza uzoefu katika nchi ya Mauritius, Zambia, Estonia, Israel na Lithuania.

(b) Sera ieleze bayana kuwa serikali iandae mikakati ya kitaifa ya kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapata taarifa zinazohusu huduma wanazozihitaji kwa njia ya kieletroniki.

(c) Sera pia ibainishe na kueleza pamoja na kutoa majukumu kwa taasisi mbalimbali za kiserikali kutoa elimu katika maeneo yanayohusika na huduma inazozitoa na namna ya kuzipata huduma hizo kwa njia ya kielektroniki.

(d) Sera iainishe maeneo ambayo yatakubalika katika mawasiliano ya kieletroniki kwa mfano, mikataba ya keletroniki, mapendekezo (offer), mawasiliano (communication), kuvunjika kwa mkataba kwa njia ya kieletoniki (revocation), ujumbe mfupi wa maelezo wa kieletroniki, mashahidi na ushahidi wa kieletroniki, kutambua masuala ya leseni zilizotolewa kwa njia ya kieletoniki, ruhusa, saini za kidijitali (digital signature) na uwasilishaji wa nyaraka kwa njia za kieletroniki.

(e) Sera ya Serikali mtandao iangalie mfumo mzima wa kisheria kuhusu uendeshaji wa shughuli zake juu ya serikali kimtandao. Mfano, Polisi kuanzia ufunguaji wa mashauri, DPP, Mahkama na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

(f) Sera iainishe na kutoa miongozo juu ya uanzishwaji wa vituo vya kieletroniki katika maeneo ya wazi ili jamii iweze kujifunza au kutumia huduma zitakazotolewa na taasisi mbali mbali kwa njia ya kieletroniki.

7.1.2 Mapendekezo ya Kisheria

Baada ya kukamilisha utafiti katika Mapitio ya Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao Nam. 12 ya mwaka 2019, Tume ya kurekebisha Sheria inapendekeza yafuatayo:

1. Kuimarishwa kwa chombo ambacho kitasimamia utekelezaji wa uendeshaji wa Serikali Mtandao. Chombo hicho kiwe na nguvu ya kisheria ya kusimamia taasisi nyengine za Serikali na kitambulike kama

Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-Government Authority) badala ya chombo kilichopo sasa ambacho ni Wakala wa Serikali (e-Government Agency) ambacho hakiendani na uzito wa majukumu yaliyowekwa katika chombo hicho.

2. Sheria itambue taratibu za usalama wa mtandao na udhibiti wa taarifa za taasisi za umma. Sheria ibainishe jukumu la Ulinzi wa mifumo itakayosaidia katika usimamizi wa serikali mtandao.
3. Sheria iweke vifungu vitakavyotoa masharti kwa taasisi za Serikali kufuata miongozo itakayotolewa na Mamlaka inayosimamia masuala ya Serikali mtandao kuhusiana na mambo yote yanayohusu matumizi ya elektroniki ikiwemo ununuzi wa mifumo na vifaa vya kielektroniki.
4. Sheria iainishe vifungu vinavyoipa Mamlaka ya Serikali Mtandao, uwezo wa kuratibu masuala ya ununuzi wa vifaa vinavyohusiana na Serikali mtandao kwenye Taasisi za Serikali, sifa, viwango, mifumo ya TEHAMA. Pia Mamlaka iwe na uwezo wa kushauri, kuthibitisha na kubatilisha masuala ya ununuzi wa vifaa vinavyohitajika katika serikali mtandao kwa kuzingatia uweledi na maslahi mapana ya nchi.
5. Sheria iweke vifungu vya kutambua mikataba yote iliyofungwa kwa njia za kieletroniki, kwa kufuata masharti yatakayoainishwa na sheria hii ikiwemo, utambuzi wa ombi (offer) iliyopelekwa kwa njia za kieletroniki pamoja na kukubalika kwa ombi kwa njia ya kieletroniki (acceptance of offer). Aidha Sheria iweke vifungu vinavyoainisha kukataliwa kwa ombi kwa njia za kielektroniki (revocation of electronic offer).
6. Sheria iweke vifungu vitakavyoainisha kukubalika kwa mashahidi na ushahidi utakaotolewa kwa njia ya kieletroniki ikiwa umekidhi mahitaji

muhimu ya kimkataba baina ya pande mbili kama sahihi ya kieletroniki au muhuri wa kieletroniki kutoka katika taasisi mbili zilizofunga mkataba.

7. Sheria itambue makosa ya kimtandao pamoja na adhabu zake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya Tanzania namba 14 ya mwaka 2015 katika vifungu vya 4 mpaka 29.
8. Sheria ibainishe Ushirikishwaji wa Dijitali (Digital Inclusiveness) ambao ni utaratibu wa utoaji wa huduma za kidijitali unaohusisha watu wa kawaida na watu wenye mahitaji maalum. Katika utaratibu huu serikali itoe utaratibu rahisi wa kimtandao ili watu wenye uwezo tofauti waweze kutumia. Kwa mfano matumizi ya kimtandao kwa watu wasioona, wasiosikia na wengine wenye mahitaji maalum. Kufanikiwa kwa suala hili la serikali mtandao kutawawezesha watu wa aina mbalimbali kuweza kumudu matumizi ya kimtandao na hivyo kuifanya nchi kuwahusisha wananchi wote katika matumizi ya kidijitali.
9. Majukumu na uwezo wa Mamlaka ya Serikali Mtandao uwe mahsusi (specific) ili usiingiliane na majukumu na uwezo wa mamlaka nyengine kama vile Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma na taasisi nyengine.
10. Inapendekezwa kuwa Sheria iweke masharti ya Mamlaka ya Serikali Mtandao kuwa na voti yake (Vote) itakayosimamiwa na Mkurugenzi Mkuu ili kuipa nguvu Mamlaka hiyo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kwa ujumla, Tume inapendekeza Sheria kuwa na masharti mbali mbali katika maeneo yafuatayo:

(i) kuweka misingi ya Serikali mtandao,
(ii) Malipo ya kielektroniki,
(iii) Utunzaji wa kumbukumbu kwa njia ya kielektroniki,
(iv) Upatikanaji wa mafaili ya taasisi mbalimbali na kuunganishwa na mifumo,
(v) taratibu za utawala na taarifa na upokeaji taarifa,
(vi) Taratibu ziliozunganishwa pamoja,
(vii) Utaratibu na mahitaji yanayohusu utoaji wa data na uthibitisho wake,
(viii) Kizuizi cha matumizi ya taarifa za kibinafsi,
(ix) Kutofichua taarifa zinazotolewa kwa shirika la umma,
(x) Usalama wa taarifa,
(xi) Tovuti ya taasisi ya umma,
(xii) Mahitaji maalum ya taasisi ya umma

7.1.3 Mapendekezo ya Kikanuni.

Baada ya kupitishwa kwa Sheria inayopendekezwa, Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza mamlaka husika kuharakisha kutungwa kwa Kanuni za Sheria hii ili zitoe ufafanuzi wa vifungu vya Sheria na Sheria hii iweze kutekelezeka kwa urahisi.

Aidha, inapendekezwa utungaji wa Kanuni hizo uzingatie masharti muhimu katika kutunga Kanuni ili kuepuka kucheleweshwa kwa hatua za kutumika kwa Kanuni hizo.

7.1.4 Mapendekezo ya Kiutendaji

Tume inapendekeza mbali ya masuala ya Kisera, Kisheria na Kikanuni, yafuatayo yawekewe utaratibu ili kutimiza azma ya Serikali ya kuipa nguvu taasisi ya Wakala wa Serikali Mtandao na kuweka utaratibu mzuri wa taarifa kwa taasisi za mumma.

(a) Kuandaliwe Mpango Mkakati kwa ajili ya utekelezaji wa mawasiliano ya kimtandao kwa taasisi za Serikali na jamii. Uzoefu wan chi mbalimbali kama Lithuania, Estonia, Israel, Kenya, Mauritius na nchi nyengine za visiwa ambazo zimeelezwa katika utafiti huu zimepitia hatua kadhaa na kupata mafanikio katika Serikali Mtandao.

(b) kuwekwe miundombinu nchi nzima ili kuhakikisha mawasiliano ya kieletroniki yanawafikia wananchi wote, ikiwemo njia za tovuti, mifumo na utaratibu wa kuendesha shughuli za mkusanyiko moja kwa moja kwa kutumia mfumo wa "zoom" ili kupunguza gharama kwa Serikali.

(c) Kutolewa mafunzo zaidi kwa watendaji wa taasisi itakayoundwa kusimamia utekelezaji wa Serikali mtandao pamoja na watendaji wa taasisi za Serikali wa vitengo vya TEHAMA na wafanyakazi wengine, utaratibu ambao Mauritius wameutekeleza kwa kiwango kikubwa.

(d) Kutenga fedha katika bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa na miundombinu itakayohitajika ili kuimarisha mwasiliano ya kimtandao.

(e) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu na sababu za Serikali kuamua kuwasiliana kimtandao na namna ya kuzifikia huduma mbali mbali kupitia serikali mtandao, na kuwashirikisha kwa karibu ili waweze kutumia huduma kupitia mitandao.

(f) Kutokana na mwitikio mdogo katika masuala ya Serikali mtandao, kuandaliwe programu ya kujenga ushawishi mkubwa kwa wananchi na taasisi za Serikali na taasisi binafsi kuingia kwenye matumizi ya serikali mtandao, na inapobidi, kuweka taratibu zitakazoweka mazingira ya lazima kutumia Serikali mtandao.

(g) kufungwa nyaya za "fiber-optic" tangu mwanzo katika maeneo ambayo bado hayajahudumiwa, ili kuwa na uwezo wa "bandwidth" kwa utoaji wa huduma katika siku zijazo kadri zinavyopatikana, hatua hii pia imesaidia visiwa vya Fiji, Vanuatu na Solomon kuwa na mawasiliano ya karibu na nchi nyengine.

(h) Pamoja na kuwa na miundombinu katika taasisi za Serikali na hasa mashirika, kuna haja ya kufanyia ukaguzi mifumo hiyo ili kujua iwapo inaweza kuunganishwa na mifumo mengine au kusomana ili kurahisisha mawasiliano na upatikanaji wa taarifa kwa pamoja (centralized). Ikiwa taarifa hizi zitaunganishwa vizuri zinaweza kuwa hazina kianzio muhimu kwa wananchi.

(i) Kuwekwa ushirikiano mzuri baina ya taasisi ya Wakala Mtandao na Taasisi za umma, ambao utalenga katika mafunzo na programu ambazo zinaweka wazi sera, mafunzo na ununuzi wa vifaa vinavyohusiana, pamoja na kuhifadhi ushahidi wa kidijitali.

7.2 Hitimisho

Uwepo wa Serikali mtandao kwa ajili ya uboreshaji wa huduma kwa wananchi ni kitu cha lazima ingawa utekelezaji wake ni wa gharama. Kwa hali ya kiteknolojia ilipofikia kwa sasa, suala la uendeshaji wa Serikali hasa katika utoaji wa huduma kwa wananchi kupitia serikali mtandao haliwezi kuepukika

kutokana na faida nyingi za mfumo huu kama zilivyoelezwa katika Ripoti hii. Ili kufikia malengo hayo, Serikali inapaswa kuandaa taasisi ambayo itaratibu utekelezaji mzima wa uwepo wa Serikali mtandao.

Pia taasisi hiyo itakayoanzishwa iwe na wataalamu wa kutosha wa fani ya TEHAMA, wakiwemo wataalamu waliobobea katika masuala ya serikali mtandao, vifaa vya kisasa vyenye ubora unaokubalika kimataifa, pamoja na kuimarisha vituo katika taasisi za Serikali, wataalamu pamoja na wafanyakazi katika taasisi hizo.

Uimarishaji wa miundo mbinu katika utekelezaji wa serikali mtandao ni jambo muhimu sana ambalo linapaswa kuwekewa mikakati ya kisera ili kuhakikisha kwamba nchi inakuwa na Serikali mtandao endelevu kwa maendeleo ya nchi na watu kwa ujumla.

Kwa kuwa uimarishaji wa miundombinu na kiteknolojia ni gharama kubwa, Serikali inapaswa kutoa fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba malengo ya uanzishwaji wa Serikali mtandao yanafanikiwa.

REJEA

MAKALA NA VITABU

Abdulrazaq Kayode Abdulkareem "Challenges of E-Government Implementation in the Nigerian Public Service, Journal Of Creative Writing Volume 1, ISSUE 4 2015, PP 45-56,

Åke Grönlund; "Ten Years of E-Government: The End of History and New Beginning;" Swedish Business School Fakultetsgatan 1, 701 82 Örebro, Sweden

Ali KE, Mazen SA, Hassanein EE. A proposed framework for the organization readiness assessment of IT innovation adoption in e-government environment. *Int. J. Intell. Comput. Inf. Sci.* 2017;17(2):33–50

Anttiroiko, A i-Veikko. and Malkia, Matti. 2006. Encyclopedia of digital government. Hershey, PA: Idea Group Reference (IGI)

Ahn MJ, Bretschneider S. Politics of e-government: e-government and the political control of bureaucracy. *Public Adm. Rev.* 2011;71(3):414–424.

Aziz NAA, Manab NA, Othman SN. Critical success factors of sustainability risk management (SRM) practices in Malaysian environmentally sensitive industries. *Soc. Behav. Sci.* 2016;2016(219):4–11.

Boaz Chean and David Rashty, e- government in Israel, Ministry of Finance General Acountant Office, September 2002

Cook, M., & Harrison, T. M. (2015). Using public value thinking for government IT planning and decision making: A case study. Information Polity, 20(2/3), 183–197

David Brown "Electronic government and public administration" International Review of Administrative Sciences, 2005 IIAS, SAGE Publications (London, Thousand Oaks, CA and New Delhi) Vol 71(2):241

Ebrahim Z, Irani Z. e-Government adoption: architecture and barriers. *Bus. Process Manag. J.* 2005;11(5):589–611. doi: 10.1108/14637150510619902

Gore, Albert (1993). "Reengineering Through Information Technology. Accompanying Report of the National Performance Review" Washington: Office of the Vice President

Gregory G. Curtin, Michael Sommer & Veronika Vis-Sommer (2003), The World of E-Government, Routledge

Heeks, Richard. and Bailur, Savita. 2007. Analyzing e-governmen research: perspectives, philosophies, theories, methods, and practice. Government Information Quarterly, 24(2):243- 265

Hanna NK. Transforming Government and Building the Information Society: Challenges and Opportunities for the Developing World. New York: Springer; 2010
Savoldelli A, Codagnone C, Misuraca G. Understanding the e-government paradox: learning from literature and practice on barriers to adoption. *Gov. Inf. Q.* 2014;

Isabel Bosman (2021) "COVID-19 and E-Governance: Lessons from South Africa" South African Institute of International Affairs Stable

J. Pengur. 2018;2018(53):73–82. doi: 10.17576/pengurusan-2018-53-07

Latifa Alzahrani, Wafi Al-Karaghouli, Vishanth Weerakkody
Analysing the critical factors influencing trust in e-government adoption from citizens' perspective: A systematic review and a conceptual framework, 2016 Published by Elsevier Ltd.

Layne, K. & Lee, J. (2001). "Developing Fully Functional E-Government: A Four Stage Model." Government Information Quarterly. 18, 122

Leon J. Osterweil, Lynette I. Millett, and Joan D. Winston, (Eds)Social Security Administration Electronic Service Provision; A Strategic Assessment; The National Academies Press, 2007, N.W., Washington, DC 20055

Ligita zailskaitic E- government implementation in lithunia, Kauns University of Technology Institute of Europe, Liuthenia

Michael P, et al. e-Government implementation challenges in developing countries: the project manager's perspective. *Int. J. Public Adm. Manag. Res.*
(IJPAMR) 2018;4(3):1–17]

Manjot Kaur1 , Dr. Amitoj Singh, E-Government: Study of Factors significantly affects Adoption and Acceptance in State of Punjab, (IJCSIT) International Journal of Computer Science and Information Technologies, Vol. 6 (5) , 2015, 4542-4548

Melitski, J. (2003). "Organizational Capacity and E- government Performance." Public Performance and Management Review. 26, 325

Meiyanti, R., et al.: Systematic review of critical success factors of e-government: definition and realization. In: 2017 International Conference on Sustainable Information Engineering and Technology (SIET), Malang, Indonesia. IEEE (2018)

Moon, M. J. (2002). "The Evolution of E-government Among Municipalities: Rhetoric or Reality?" Public Administration Review. 62, 42

M Backus "E-governance in developing countries", IICD Research Brief No 1, March 2001, website: www.iicd.org; see also P Norris 'The worldwide digital divide: information poverty, the Internet and development' Harvard University, 2000.

Nancy J. Hafkin "-government in Africa: An Overview of Progress Made and Challenges Ahead" Prepared for the UNDESA/UNPAN workshop on electronic/mobile government in Africa: Building Capacity in Knowledge Management through Partnership, held at the United Nations Economic Commission for Africa, 17-19 February 2009

Naome Rajah; E- Government in Zimbabwe: An Overview of Progress made and Challenges Ahead; Volume 6, No. 12, December 2015; Journal of Global Research in Computer Science, Research Paper,

Napitupulu D, Sensuse DI. (2014) "The critical success factors study for e-government implementation." *Int. J. Comput. Appl.* 2014;89 (16):23–32.,

Pardo TA, Nam T, Burke GB. (2012) E-government interoperability interaction of policy, management, and technology dimensions. *Soc. Sci. Comput.Rev.* 2012;30(1):7–23.

Nkohkwo QN, Islam MS. Challenges to the successful implementation of e-government initiatives in Sub-Saharan Africa: a literature review. *Electron. J. E-Gov.* 2013;11:253–267

Ndou. V, (2004) E-government for developing countres: opportunities and challenges. The Electronic Journal on Information Systems in Developing Countries. Vol. 18 no 1. PP 1-24

OECD ‘The E-government imperative’, in OECD E-Government Studies. OECD, Paris, 2003,

Olowu 2004 Quoted in “Chapter 12 :Elecgtronic Government and Rural Development in Anglophone West Africa, by Kehinde David Adejuwon, Sodhi, Inderjeet Singh (ed) (2014) “Emerging Issues and Prospects in African E-Government, IGI Global.

Olaniyi, E.: (2018) “Digital government: ICT and public sector management in Africa. In: New Trends in Management: Regional and Cross-Border Perspectives,” London Scientific Publishing, London

Othman MH, Razali R. Whole of government critical success factors towards integrated e-government services: a preliminary review

Øystein Sæbø; E-government in Tanzania: Current Status and Future Challenges; University of Agder, Norway,

Prakash, N., Jaiswal, M., & Gulla, U. (2009). A conceptual framework for measuring public value of enterprise applications. Electronic Government, an International Journal, 6(3), 307–326.

Richard Heeks (2001) "Understanding e-Governance for Development, Institute for Development Policy and Management" , Paper No. 11 Understanding e-Governance for Development Richard Heeks1 IDPM, University of Manchester, UK 2001

Richard Amaechi Onuigbo electronic governance & administration in nigeria: prospects &challenges Arabian Journal of Business and Management Review (OMAN Chapter) Vol. 5, No.3; October. 2015

Spinello, R. (2002). Regulating Cyberspace. Westport, CT: Quorum Books

Shareef MA, Yogesh NA, Dwivedi K. Examining adoption behavior of mobile government. *J. Comput. Inf. Syst.* 2012;53:39–49

Siddique W. Critical success factors affecting e-government policy implementation in Pakistan. *E-J. E-Democr. Open Gov.* 2016;8(1):102–126

Thomas A. Horan Introducing e-Gov: History, Definitions, and Issues, volume 15, June 2005

Watson and Mundy, 2001. Watson, Richard. T and Mundy, Bryan. 2001. A strategic perspective of electronic democracy Communication of the ACM 44(1):27-

West, D.M. (2005a). Digital Government: Technology and Public Sector Performance. Princeton, NJ: Princeton University Press

Xu X, Zhang W, Barkhi R. IT infrastructure capabilities and IT project success: a development team perspective. *Inf. Technol. Manag.* 2010;11:123–142.

Yadav J, Saini AK, Yadav AK. Measuring citizens engagement in e-Government projects – Indian perspective. *J. Stat. Manag. Syst.* 2019;22(2):327–346.

Ziemba E, Papaj T, Żelazny R. A model of success factors for e-government adoption – the case of Poland. *Issues Inf. Syst.* 2013;14:87–100

Ziemba E, et al. Factors influencing the success of e-government. *J. Comput. Inf. Syst.* 2016;56(2):156–167

Zoo H, de Vries HJ, Lee H. Interplay of innovation and standardization: exploring the relevance in developing countries. *Technol. Forecast. Soc. Chang.* 2017;118:334–348.

WEBSITE/TOVUTI

LNCS 7443 - E-government in Tanzania: Current Status and Future Challenges (springer.com)

http://rroij.com/global-research-in-computer-science.php

Zanzibar Social Security Fund – Zanzibar Social Security Fund | Key to the future (zssf.or.tz)

Zanzibar eGovernment Agenda - A Way Forward | Mzalendo Mtanzania - Academia.edu

https://www.istor.org/stable/resrep29596

http://pbzbank.co.tz/about-us-2/

https://au.int/en/treaties/african-union-convention-cyber-security-and-personal-dataprotection

https://www.eac.int/infrastructure/communications-sector/ongoing-projects

https://www.eac.int/infrastructure/communications-sector/ongoing-projects

http://www.ohada.com/content/newsletters/1403/Comprendre-l-Ohada-en.pdf

http://www.comesa.int/what-we-do/#information-networking

http://www.ecowas.int/wp-content/uploads/2015/02/46th-ECOWAS-Summit-Abuja-15-Dec 2014 1.pdf

http://www.pulse.ng/news/local/ecowas-biometric-ids-senegal-benin-begin-issuance-of-cardsid4651170.html

http://www.au.int/en/decisions/assembly

http://www.coe.int/en/web/conventions/full-list/-/conventions/treaty/108/signatures

http://reports.weforum.org/global-information-technology-report-2016/P

http://www.ict.go.ke/wp-content/uploads/2016/04/The-National-ICT-Masterplan.pdf

http://mtci.govmu.org/English/Documents/eGovStrategyfinalv201393.pdf

https://www.e-spincorp.com/definition-and-type-of-e-government/

https://www.coe.int/en/web/conventions/full-list/-

http://www.integratedjustice.gov.on.ca/